

USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA *DHARAU YA INI*

JANET WAMBUI

C50/20380/2012

TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU
CHA KENYATTA

OKTOBA 2018

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa madhumuni ya kutuzwa shahada yoyote.

SAHIHI J. Wambui TAREHE 23/10/2018

JANET WAMBUI
C50/20380/2012

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi

1. DKT. MIRIAM OSORE

SAHIHI M. Osore TAREHE 23/10/18

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

2. DKT. JOSEPH GAKUO

SAHIHI J. Gakuo TAREHE 23/10/2018

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

TABARUKU

Naitabarukia tasnifu hii kwa mume wangu Moffat na watoto wangu ambao wamekuwa kichocheo cha ufanisi wangu. Bila uvumilivu wao nilipokuwa nikifanya utafiti, ingeniwia vigumu kufaulu. Mungu awabariki na awajalie maisha marefu ya kuweza kufurahia matunda ya kazi hii.

SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa Mola kwa kunipa nguvu na uwezo wa kuikamilisha kazi hii. Shukrani za dhati pia ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Miriam Osore na Dkt. Joseph Gakuo kwa kujitolea kwa dhati katika kunielekeza na kunikosoa. Mungu awabariki. Nawashukuru sana wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa mafundisho yenu. Mafunzo na maelekezo yenu yalinifaa sana nilipokuwa nikifanya utafiti wangu.

Natoa shukrani nyingi kwa mume wangu kwa ajili ya maombi na msaada wako usiokuwa na kikomo. Ulinitia moyo pasipo kuchoka. Mungu akujalie baraka tele. Vilevile ninawapongeza dada zangu Grace, Susan na Ruth kwa ajili ya maombi yenu na kunitia hamasa za kuendelea na masomo yangu.

Ninapofikia kikomo sina budi kuwahongera wanafunzi wenzangu kama vile, Everlyne, Nanjala, Silvain, Musosi, Oginda, Mwilaria, Rebeka, Eliza, Teresa, Alice, Phoebe pamoja na wengine ambao tulishirikiana pamoja katika safari hii.

IKISIRI

Utafiti ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) ya Kyalo Wamitila. Malengo ya utafiti yalikuwa ni kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi katika riwaya; kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi na kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya naratolojia kwa kuzingatia mwelekeo wa Gennette (1980). Naratolojia ilitumika katika kuchunguza sifa za muundo wa simulizi kwa kugawa vipengele vyake na kuzingatia uamilifu na uhusiano uliopo. Mihimili ya nadharia hii imesaidia katika kuihakiki matini kwa kuchunguza mbinu za usimulizi zinazotumika katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti ulijikita maktabani ambapo vitabu, tasnifu na majarida yaliyoangazia masuala ya nadharia na usimulizi yalisomwa. Mbinu ya sampuli ya kimaksudi ilitumika katika ukusanyaji wa data iliyotokana na usomaji wa riwaya ya *Dharau ya Ini*. Mafungu yanayoonyesha sifa za sauti na viwango mbalimbali vya usimulizi, wakati katika usimulizi na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika yalidondolewa kutoka kwenye matini. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa mbinu ya kimaelezo kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti ulibainisha kuwa riwaya imehusisha msimulizi anayeshiriki kama mhusika katika matukio anayosimulia na katika sehemu zingine anasimulia hadithi akiwa nje ya matukio hayo. Riwaya imehusisha matumizi ya mbinu rejeshi na elekezi katika uwasilishaji wa matukio. Ilitambulika kuwa uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika ni njia muhimu ya kubadili mitazamo ya usimulizi katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti umetoa mchango kwa kuonyesha jinsi nyingine ya kuchanganua riwaya kwa kuhusisha nadharia ya naratolojia. Mapendekezo yaliyotolewa ni kuwa tafiti zaidi zifanywe ili kuchunguza mbinu za usimulizi katika tungo zingine za fasihi ili kuikuza kazi ya fasihi andishi.

ABSTRACT

The study investigated narration in the Kiswahili novel, *Dharau ya Ini* (2007) by Kyalo Wamitila. The research aimed at identifying various narrative voices and narrative levels used in the selected novel; manifesting the role of narrative time in narration and to demonstrate how presentation of speech and thoughts of characters has been used in structuring of the narrative. The research was guided by the theory of narratology as expounded by Genette (1980). The theory was used in investigating the characteristics of narrative structure by dissecting it into various elements and then attempted to determine their functions and relationships. The tenets of the theory have been used to examine the text by interrogating it to reveal the narrative techniques used in structuring of the narrative. The study was carried out in the library. Literary materials related to the topic of research were read for purposes of reviewing literature. The research used purposive sampling procedure in data collection that was obtained through reading of the selected Kiswahili novel. Sentences reflecting the usage of various narrative voices and levels, narrative time and presentations of speech and thoughts of the characters were extracted from the text. Data was analyzed and results presented in form of an informed discourse guided by the objectives of the study. The research findings manifested the presence of a homodiegetic narrator who is a participant in the story he is narrating and in some instances there is a heterodiegetic narrator telling a story without participating in the events. The text employs both analepsis and prolepsis order in presentation of events. It is evident that the presentation of speech and thoughts of characters is an important way of interchanging different modes of narration in structuring of the narrative. This study will benefit other researchers in employing different forms of narrative techniques in the analysis of the novel by applying the theory of Narratology. Recommendations for further research in the analysis of narrative techniques in other written literature has been made in order to enrich written literature.

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Naratolojia:** Nadharia ya uchunguzi wa muundo wa simulizi au hadithi. Nadharia hii hutoa vipengele vinavyoweza kutumiwa katika kuzihakiki simulizi.
- Udondoshi:** Hurejelea pale ambapo maelezo fulani yameachwa katika matini fulani.
- Mtuo:** Huu ni wakati ambao matukio katika hadithi yanakatizwa ili kuachia nafasi maelezo mengine katika hadithi.
- Onyesho:** Usimulizi unaoleta sifa za uigizaji katika matini yoyote ile.
- Idadi-marudio:** Hurejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi na mara ngapi matukio hayo yanasimuliwa.
- Analepsia:** Ni hali ambapo matukio ya wakati uliopita yanahusishwa katika usimulizi wa matukio ya wakati uliopo
- Prolepsia:** Huwa ni usimulizi wa matukio ya wakati ujao kabla ya wakati wake.
- Usemi taarifa huru:** Ni zao la kufanyia mabadiliko usemi taarifa kwa kuondoa maneno yanayoashiria usemi taarifa na kuyawakilisha na yale ya usemi halisi.
- Usemi halisi huru:** Ni uwasilishaji wa maneno kama yanavyotamkwa bila kutumia alama za mtajo.
- Usimulizi kabla:** Ni kipengele kinachorejelea usimulizi wa matukio kabla ya kutokea kwake
- Usimulizi baadaye:** Hurejelea hali ya usimulizi wa matukio baada ya kutendeka kwake.

- Usimulizi sawia:** Ni aina ya usimulizi ambapo matukio yanasimuliwa wakati uo huo wa kutokea kwake, yaani usimulizi sawia.
- Usimulizi zongomezi:** Huu ni wakati ambapo muda wa usimulizi na muda wa utendaji huandamana katika kubadilishana nafasi.
- Usimulizi rudufu:** Ni tukio linalofanyika mara moja na likasimuliwa mara nyingi katika simulizi.
- Muhtasari:** Ni ufupishaji wa muda fulani wa hadithi kwa kauli chache ili kuharakisha na kuufanya wakati hadithi uwe mfupi kuliko wakati matini.
- Usimulizi Ndani:** Huu ni mtazamo wa usimulizi ambapo msimulizi wa hadithi ni mhusika mmojawapo kwenye ulimwengu wa hadithi anayosimulia.
- Usimulizi Nje :** Ni mtazamo wa usimulizi ambapo msimulizi anasimulia hadithi bila kushiriki katika matukio anayosimulia.
- Usimulizi Mosi:** Ni aina ya usimulizi ambapo tukio linaweza kutokea mara moja na kusimuliwa mara moja katika hadithi.
- Usimulizi Banifu:** Hiki ni kigezo cha usimulizi kinachoonyesha kuwa tukio linaweza kutokea mara nyingi kisha mara zote zile zikabanwa kwa maneno machache na kusimuliwa mara moja.
- Fikra Halisi:** Ni mbinu ya usimulizi ambapo fikra za mhusika huonyeshwa kwa kutumia usemi halisi.
- Fikra Taarifa:** Huwa ni mawazo ya wahusika yanayowasilishwa kwa njia ya usemi wa taarifa.

YALIYOMO	UKURASA
UNGAMO	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU	ii
SHUKRANI	iii
IKISIRI	iv
ABSTRACT	v
UFAFANUZI WA ISTILAH	vi
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa Utafiti.....	1
1.1 Suala la Utafiti	6
1.2 Maswali ya Utafiti	7
1.3 Malengo ya Utafiti.....	7
1.4 Sababu za kuchagua Mada.....	8
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti	9
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	10
1.7 Misingi ya Nadharia	14
1.7.1 Sauti ya Usimulizi na Viwango vya Usimulizi.....	18
1.7.2 Wakati katika Usimulizi	20
1.7.3 Uwasilishaji wa Usemi na Fikra	23
1.8 Mbinu za Utafiti.....	25
1.8.1 Muundo wa Utafiti.....	25
1.8.2 Eneo la Utafiti.....	26
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli.....	26
1.8.4 Ukusanyaji wa Data	26
1.8.5 Uchanganuzi wa Data	27
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo	27
1.9 Kiishilio	28
SURA YA PILI	29
UAINISHAJI WA SAUTI ZA USIMULIAJI NA VIWANGO VYA USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA DHARAU YA INI	29
2.0 Utangulizi	29

2.1.1 Usimulizi wa Ndani	32
2.1.2 Usimulizi wa Nje	37
2.2 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza	41
2.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Pili	43
2.2.2 Usimulizi Nafsi ya Tatu	47
2.3 Mahusiano ya Wakati wa Usimulizi	51
2.3.1 Usimulizi Baadaye	52
2.3.2 Usimulizi Kabla	53
2.3.3 Usimulizi Sawia	55
2.3.4 Usimulizi Zongomezi	56
2.4 Viwango vya Usimulizi	57
2.5 Nafasi ya Msimulizi katika Usimulizi wa Hadithi	65
2.5.1 Jukumu la Usimuliaji wa hadithi	65
2.5.2 Jukumu la Kumwelekeza Msomaji	68
2.5.3 Jukumu la Kumshirikisha Msomaji katika Usimulizi.	70
2.5.4 Jukumu la Kuwasilisha Itikadi zake kwa Msomaji	72
2.5.5 Jukumu la kutoa Ushuhuda kuhusu matukio	73
2.6 Kiishilio	75
SURA YA TATU	76
NAFASI YA WAKATI KATIKA USIMULIZI WA RIWAYA YA	
<i>DHARAU YA INI</i>	76
3.0 Utangulizi	76
3.1 Wakati katika Usimulizi	76
3.1.1 Mpangilio wa Matukio	78
3.1.2 Analepsia	79
3.1.3 Prolepsia	83
3.2 Muda wa Matukio	85
3.2.1 Mtuo	86
3.2.2 Muhtasari	89
3.2.3 Onyesho	92
3.2.4 Udondoshi	95
3.2.5 Maoni ya Msimulizi	97

3.3 Idadi ya Utokeaji wa Matukio	101
3.3.1 Usimulizi Mosi	101
3.3.2 Usimulizi Rudufu	102
3.3.3 Usimulizi Banifu.....	107
3.4 Kiishilio	109
SURA YA NNE	111
UWASILISHAJI WA USEMI NA FIKRA ZA WAHUSIKA KATIKA	
UENDELEZAJI WA RIWAYA YA DHARAU YA INI.....	111
4.0 Utangulizi	111
4.1 Uwasilishaji wa Usemi wa Wahusika.....	111
4.1.1 Usemi Halisi	112
4.1.2. Usemi wa Taarifa.....	114
4.1.3. Usemi Halisi Huru	117
4.1.4.Usemi wa Taarifa Huru	120
4.2 Uwasilishaji wa Fikra za Wahusika.....	124
4.2.1.Fikra Halisi	125
4.2.2. Fikra Halisi Huru	127
4.2.3 Fikra za Taarifa.....	130
4.2.4. Fikra za Taarifa Huru.....	133
4.3 Kiishilio	137
SURA YA TANO	139
HITIMISHO.....	139
5.0 Utangulizi	139
5.1 Muhtasari wa Utafiti	139
5.2 Matokeo ya Utafiti	143
5.3 Mchango wa Utafiti	146
5.4 Changamoto Zilizokabili Utafiti.....	147
5.5 Mapendekezo	147
MAREJELEO	149

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) ya Kyalo Wamitila. Suala la usimulizi ni la kimsingi sana katika uwasilishaji wa kazi za fasihi. Usimulizi huwa ni zaidi ya namna hadithi inavyoelezwa au kuwasilishwa. Todorov (1977) anasema kuwa usimulizi ni njia ya mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji na kati ya msimulizi na yule anayesimuliwa katika kazi za kiubunifu. Hii ni njia inayotumiwa na mwandishi katika kupitisha ujumbe pamoja na kutoa mtazamo wa masimulizi kama anavyosema Barthes (1975). Simulizi nayo ni maelezo kuhusu matukio ya kihalisia au ya kubuni ambayo msimulizi huchukulia kuwa ya muhimu katika kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa kwa wasikilizaji. (Gennette, 1980).

Hivyo kama anavyoeleza Gennette (1983), hadithi inapowasilishwa vipengele mbalimbali huwa vimefumbatwa ambavyo kwa jumla vinachangia katika kuujenga muundo wa hadithi. Vipengele hivi vinapochanganuliwa hupelekea katika kuielewa simulizi ifaavyo. Barry (1995) anathibitisha madai haya kwa kusema kuwa kiini cha usimulizi si hadithi yenyewe bali ni jinsi hadithi inavyowasilishwa. Anasema hali hii huweza kumchochea kila msanii kuibua mikakati maalum ya mawasiliano katika kukuza mawazo yanayokusudiwa. Hivyo ni sharti mwandishi ataeue aina ya usimulizi utakaotumika, wakati utakaohusika pamoja na kuzingatia jinsi atakavyouendeleza usimulizi wake katika kuwasilisha matukio katika hadithi.

Kwa mujibu wa Kenan (1983), mwandishi siye msimulizi bali huwaachia wawakilishi kazi ya usimulizi. Hata ingawa uwepo wake hukosa kudhihirika katika kazi za kinathari, itikadi zake hujitokeza katika jinsi anavyogawa majukumu kwa wawakilishi wake ambao ni wasimulizi na wahusika. Stanzel (1984:3) anaafikiana na mtazamo wa Kenan kuwa msimulizi hujitokeza kama mwakilishi baina ya mwandishi na msomaji na baina ya hadithi na msomaji. Anaeleza kuwa msimulizi huweza kuwasilisha mawazo na ujumbe wa mwandishi kwa kuhusisha nafsi mbalimbali.

Ingawa hivyo, Booth (1961) anatoa mtazamo tofauti na kusema kuwa msimulizi na wahusika hawana uhusiano au mwingiliano wowote na mwandishi. Hivyo anaamini kuwa msimulizi ana uhuru wa kuwasilisha simulizi pasipo kuathiriwa na mwandishi na wala si lazima amwakilishe katika usimulizi wake.

Naye Gennette (1980:186) anasisitiza kuwa kila matini ina sauti ya msimulizi inayomwongoza msomaji katika ulimwengu wa maandishi ya kubuni. Sauti hiyo humpitisha katika mpangilio wa matukio, nyakati mbalimbali na kumwingiza kwenye mawasiliano na mawazo ya wahusika. Ni kutokana na mwingiliano huu baina ya msimulizi na hadithi ambapo msomaji hupata ufahamu wa masimulizi yake. Hali hii inadhahirisha wazi kuwa usimulizi ndio njia ya pekee anayoitumia mtunzi katika kuwasilishia ujumbe wake. Usimulizi huweza kutumika kama kigezo muhimu kinachodhihirisha tofauti ya kiasili baina ya mtunzi mmoja na mwingine kuhusu jinsi anavyowasilisha ujumbe katika kazi za kinathari.

Kila matini hudhihirisha chembe cha usimulizi ambao unaweza kuchunguzwa ili kupata ufahamu kuhusu mpangilio wa simulizi kama anavyodokeza Gennette (1983). Anasema kuwa simulizi zote huwa zinahusu uelezaji na uonyeshaji, hali inayoifanya simulizi kuwa halisi na hai. Hivi ni kusema kuwa kila simulizi ni sharti iwe na msimulizi anayeisimulia hadithi na msomaji anayejihusisha na matini hiyo kupitia usimuliaji wa msimulizi.

Ingawa kila matini huweza kudhihirisha chembe cha usimulizi, wananadharia Levesque na Guillimette (2006), wanasisitiza kuwa riwaya pekee ndiyo utanzu wa fasihi unaohusishwa zaidi na matumizi mapana ya mbinu za usimulizi. Hali hii inatokana na sababu kuwa riwaya imesheheni ule uwezo wa kuchukua miundo mbalimbali ya uwasilishaji wa ujumbe. Katika riwaya yoyote ile, uwepo wa simulizi, msimulizi na usimuliaji wa matukio ni sifa maalum inayojitokeza wazi na kwa hivyo ni muhimu hasa katika uhakiki wa kazi za kinathari.

Usimulizi wa riwaya una historia ndefu iliyo na misingi hasa katika usimulizi wa hekaya na visasili vya kitamaduni. Utanzu huu kama anavyodokeza Kurtz (1998) umeweza kupitia mabadiliko mbalimbali ya kimaudhui na kimuundo. Hali hii imechangia katika kuibua mbinu changamano za usimulizi katika ukuzaji wa ujumbe unaokusudiwa.

Mbatia (2016) amehusisha maendeleo na hadhi ya kazi za kinathari hasa za hivi majuzi na mabadiliko katika maisha ya kijamii pamoja na miundo migeni ambayo imeathiriwa sana na fasihi ya kimagharibi ya karne ya kumi na tisa.

Maendeleo haya yamechangiwa zaidi na hali ya kuwepo kwa mwamko mpya katika kazi za kiubunifu hasa zilizo na misingi katika usomi wa kisasa.

Riwaya hizi za kisasa zimeibua changamoto mpya hasa kuhusiana na muundo unaotumiwa katika ukuzaji wa ujumbe. Athari hii imesababisha kuwepo kwa riwaya zenye sifa za usimulizi ambazo zina upya na upekee, kinyume na riwaya za hapo awali hasa zilizoandikwa kabla ya miaka ya tisini.

Maendeleo ya riwaya ya Kiswahili nchini Kenya, kwa mujibu wa King'ei (1999) yanaweza kuainishwa katika vipindi vinne. Kipindi cha kwanza kilikuwa kabla ya kupata uhuru kati ya mwaka 1850-1890; kipindi kilichofuata kilikuwa chenye uhaba wa kazi za kinathari kati ya mwaka 1890-1930; Kipindi cha tatu ni kile cha mapambano ya uhuru kati ya mwaka 1963-1992. Uainishaji wa King'ei ulisaidia katika kupata ufahamu kuwa, kipindi cha hivi majuzi au cha sasa katika utunzi wa riwaya kilianza mwaka 1992 hadi sasa. Hiki kimekuwa kipindi ambacho utanzu wa riwaya umeanza kupata mielekeo mipya ya kimuundo na kimaudhui iliyofungamana na maendeleo na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kiitikadi na kisiasa.

Uainishaji wa King'ei (1999) unadhihirisha kuwa riwaya zilizoandikwa kabla ya miaka ya tisini ndizo zinazoweza kurejelewa kama riwaya kongwe. Baadhi ya riwaya hizi ni kama: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974), *Gamba la Nyoka* (1978) za Euphrase Kezilahabi. Vilevile kuna zingine kama *Asali Chungu* (1978) na *Utengano* (1980) za S. A. Mohamed, *Mpango* (1982) na *Kitanzi* (1984) za Simba Mwene miongoni mwa zingine. Riwaya hizi ni tofauti

na zile zinazotungwa katika kipindi cha sasa hasa katika muundo. Mabadiliko katika utunzi wa riwaya yalianza kudhihirika wazi mwanzoni mwa 1990's.

Kulingana na Khamis (2007), huu ulikuwa muda mfupi tu baada ya neno, 'Utandawazi' kuingia na kuzama akilini mwa watu. Anasema kuwa mtindo katika riwaya ya sasa ya Kiswahili unazidi kubadilika kulingana na wakati. Anatoa madai kuwa riwaya hii mpya inaafiki zaidi kusawiri ule ukosefu wa udhibiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi katika mataifa ya Afrika Mashariki.

Kuzuka kwa riwaya mpya ya Kiswahili katika miaka ya 1990 kunaelezwa kwa viwango mbalimbali na wahakiki wengine kama vile Fokkema (1995), Mbatiah (1997, 2016), Gromov, (2002, 2004), Khamis (1999, 2007) na Wamitila (2007). Khamis anaeleza kuwa miongoni mwa riwaya zinazotambulika kuwa mpya ni zile za Euphrase Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile* (1990), *Walenisi* (1995) ya K. Mkangi, riwaya ya W. E. Mkufya ya *Ziraili na Zirani* (1999), *Nguvu za Sala* (1999) ya Kyalo Wamitila na riwaya ya S. A. Mohamed, *Babu Alipofufuka* (2001).

Riwaya zingine zilizoandikwa baadaye ni kama riwaya ya *Binadamu* (2002), *Wana wa Bundi* (2005) na *Dharau ya Ini* (2007) za Wamitila na nyinginezo kama *Dunia Yao* (2006) na *Mkamadume* (2012) za S.A Mohamed miongoni mwa zingine. Baadhi ya riwaya hizi zimeshughulikia kwa kina matatizo ambayo yanaukabili ulimwengu wa leo kwa kuhusisha ukwasi mkubwa wa mbinu za kisimulizi ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa. Kutokana na misingi hii, usimulizi umedhihirika kuwa kipengele muhimu katika fasihi andishi kinachochangia katika kueleweka kwa ujumbe katika kazi za kinathari.

Hivyo utafiti huu ulinua kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*.

1.1 Suala la Utafiti

Utafiti ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Suala la usimulizi ni la kimsingi sana katika uwasilishaji wa kazi za fasihi hasa za kinathari. Kipengele hiki ni muhimu katika fasihi andishi kwani hujikita katika suala zima la mawasiliano baina ya msimulizi na usimuliaji pamoja na msomaji katika kazi za kiubunifu. Hivyo hutofautisha kile kinachosimuliwa na jinsi kinavyosimuliwa na huchangia pakubwa katika kueleweka kwa ujumbe.

Katika matini kuna sauti ya msimulizi inayomwongoza msomaji katika ulimwengu wa maandishi ya kubuni, ikimpitisha katika mpangilio wa matukio, nyakati mbalimbali, mawasiliano ya wahusika, utendaji wao na mawazo yao. Namna msimulizi anavyoingiliana na hadithi na nafasi yake katika uwasilishaji wa hadithi ndiyo humwelekeza msomaji kuuelewa usimulizi wake. Hali hii inadhihirisha kuwa usimulizi ni kigezo muhimu kinachodhihirisha tofauti ya kiasili baina ya mtunzi mmoja na mwingine katika jinsi anavyowasilisha ujumbe.

Hivyo, kipengele hiki ni muhimu sana na kinafaa kuchunguzwa kwa kina ili kupata uelewa zaidi kuhusu mbinu za usimulizi zinazotumika katika riwaya ya sasa ya Kiswahili. Ijapokuwa tafiti kuhusu usimulizi katika riwaya zimefanywa, hazijashughulikia kwa kina vipengele vyote vinavyohusika katika usimulizi. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi zinazotumika katika riwaya teule. Utafiti ulilenga kutambua

iwapo msimulizi anashiriki katika matukio anayosimulia au yu nje ya matukio hayo akakosa kutambulika wazi mbele ya msomaji. Viwango vya usimulizi vilichunguzwa ili kubainisha iwapo viwango hivyo vinaenda sambamba na viwango mbalimbali vya hadithi.

Vilevile utafiti ulinua kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi ili kuonyesha uhusiano kati ya muda wa kutokea kwa matukio katika hadithi na mpangilio wake. Isitoshe utafiti ulikusudia kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa riwaya. Lengo lilikuwa kuonyesha iwapo njia zinazotumika kuwasilisha usemi wa wahusika ni sawa na za fikra zao. Pia utafiti ulibainisha iwapo uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika ni njia mwafaka ya kubadili mitazamo ya usimulizi katika hadithi.

1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi vinabainika vipi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) ya Wamitila?
- ii. Je, wakati una nafasi gani katika usimulizi wa riwaya teule?
- iii. Je, uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika umedhihirikaje katika uendelezaji wa hadithi.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliofanywa ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo:

- i. Kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi vinavyotumika katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) ya Wamitila.

- ii. Kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya teule.
- iii. Kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi.

1.4 Sababu za kuchagua Mada

Usimulizi una nafasi muhimu katika kazi za kinathari. Bila usimulizi hamna hadithi wala riwaya. Hii ni njia ya pekee anayotumia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa. Riwaya ni utanzu wa fasihi unaohusishwa zaidi na matumizi mapana ya vipengele maalum vya kisimulizi ambavyo vinachangia katika kuujenga muundo wa hadithi (Levesque na Guillimette, 2006). Vipengele hivi vinapochanganuliwa huchangia zaidi katika kuielewa hadithi.

Kulingana na Kurtz (1998), riwaya nyingi za sasa zimedhihirisha mapinduzi katika fasihi ya Kiswahili hasa kuhusiana na upekee katika muundo wake. Anasema miundo hii ina misingi yake katika riwaya za kimagharibi za karne ya kumi na tisa. Riwaya teule inajumuishwa miongoni mwa riwaya za sasa kulingana na uainishaji wa vipindi vya maendeleo ya riwaya ya Kiswahili wa King'ei (1999).

Ingawa kuna riwaya nyingi za kisasa, *Dharau ya Ini* ni miongoni mwa riwaya zinazosheheni ukwasi mkubwa wa mbinu za usimulizi zenye upya na upekee. Hivyo ina data ya kutosha katika matumizi ya mbinu za usimulizi ambayo ingekidhi mahitaji ya utafiti huu.

Hivyo kipengele cha usimulizi ni muhimu na kinafaa kuchunguzwa ili kupata ufahamu kuhusu mbinu za usimulizi zinazotumika katika riwaya ya kisasa ya

Kiswahili. Ni kutokana na misingi hii ambapo utafiti ulidhamiria kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) na Wamitila.

Utafiti utawasaidia wasomaji kuuelewa muundo wa riwaya teule kwa kina hasa kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi. Utawafaidi watunzi wengine wa riwaya hasa kuhusiana na uteuzi wa mbinu za usimulizi zinazoweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia ya naratolojia.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulijikita katika kuichanganua riwaya ya *Dharau ya Ini*. Kazi ya Wamitila iliteuliwa kutokana na uchunguzi na usomaji wa hapo awali. Usomaji huo ulibainisha kuwa Wamitila amehusisha matumizi mapana ya mbinu za usimulizi zenye upya na upekee katika utunzi zake ikilinganishwa na watunzi wengine.

Ingawa kuna riwaya zingine nyingi, mtafiti aliteua hii mahsusi kwa sababu kwanza; ni riwaya iliyotungwa katika kipindi cha sasa (kulingana na uainishaji wa vipindi vya maendeleo ya riwaya King'ei (1999). Hivyo ni miongoni mwa riwaya za kisasa zinazosheheni ukwasi mkubwa wa mbinu za usimulizi katika muundo wake. Na kama asemavyo Khamis (2007) riwaya mpya ya Kiswahili imeibua changamoto mpya katika uandishi wa kazi za kiubunifu kutokana na upekee katika utunzi wake. Hivyo riwaya teule ni kielelezo bora cha riwaya za sasa kutokana na matumizi mapana ya mbinu za kisimulizi.

Usimulizi huhusisha vipengele vingi lakini kazi hii imejikita katika vipengele vitatu; sauti ya usimuliaji na viwango vya usimulizi, wakati na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Vipengele hivi ndivyo vinavyotumika kwa wingi

katika riwaya teule ikilinganishwa na vipengele vingine vya usimulizi. Kwa hivyo kazi iliyoteuliwa ina data ya kutosha katika matumizi ya mbinu mbalimbali za usimulizi.

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Kulingana na uchunguzi wa hapo awali wa mtafiti, hakuna utafiti mwingine ambao umefanywa ili kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Ingawa kuna tahakiki nyingi kuhusu riwaya ya Kiswahili, ni tafiti chache tu ambazo zimeshughulikia suala la usimulizi kama muundo. Tahakiki nyingi ambazo zimefanywa zimehusishwa na usimulizi kwa kuzingatia kipengele cha mtindo katika kazi za kinadhari. Nazo tahakiki ambazo zimeshughulikia usimulizi kama muundo hazijashughulikia vipengele vinavyohusika kwa kina. Kwa kurejelea usimulizi katika kazi za kiubunifu, Khamis (1999) alipokuwa akishughulikia mada kuhusu ‘Riwaya mpya na utandawazi’ anaeleza jinsi riwaya ya Kiswahili inavyoshuhudia mabadiliko katika mtindo kulingana na wakati. Anasema kuwa riwaya mpya anayoizungumzia imezaliwa mwanzoni mwa miaka ya 1990’s. Gromov (2004) anaunga mkono mawazo haya na kusema kuwa riwaya ya Kiswahili imechukua mkondo mpya katika utunzi wake hasa katika kuwasilisha matatizo yanayoukabili ulimwengu wa sasa. Hivyo ni muhimu kuihakiki riwaya ya sasa ya Kiswahili ili kuchunguza mbinu za usimulizi zinazotumika katika uwasilishaji wa ujumbe.

Gaita (1998) alitathmini mbinu za usimulizi katika riwaya za Kezilahabi na S.A. Mohamed za miaka ya 60 na 70, ili kutambulisha ufaafu wake katika uwasilishaji wa ujumbe. Utafiti huo ulichunguza uhusiano uliopo kati ya

muundo na maudhui kwa kuzingatia mbinu za usimulizi katika riwaya teule. Alilenga kutathmini jinsi uhusiano huo ulivyochangia katika kufahamu maana na umuhimu wa riwaya zilizohusika na wala hakushughulikia vipengele vingine kwa kina. Utafiti huo ulijikita katika nadharia ya naratolojia.

Utafiti huu unalenga kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Utafiti unanua kubainisha sauti za usimulizi na viwango vya usimulizi zinavyotumika; kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi na kudhihirisha matumizi ya uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika upitishaji wa ujumbe. Ingawa matini iliyochanganuliwa ni tofauti, kazi hii imetumia nadharia sawa na kazi hiyo na ilikuwa ya manufaa katika utafiti huu.

Uhakiki wa Ong'ondi (2005) ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi. Malengo ya utafiti wa Ong'ondi yalikuwa ni kubainisha matumizi ya mbinu za usimulizi; kuonyesha tofauti baina ya mtazamo uliotokea na usimulizi wenyewe, viwango mbalimbali vya usimulizi, wakati na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Utafiti wake ulijikita katika nadharia ya naratolojia sawa na utafiti huu ingawa matini aliyochunguza ni tofauti. Utafiti huo ulidhihirisha kuwa kuliweza kuwa na viwango vya usimulizi katika hadithi vinavyoenda sambamba na viwango vya hadithi. Utafiti huo ulikuwa wa manufaa kwa kuwa ulitoa mwanga zaidi kuhusu kipengele cha wakati na uwasilishaji wa usemi na fikra kwani ni baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu.

Kinara (2012) alifanya utafiti kuhusu maudhui ya Ukimwi katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) ya W.E Mkufya na *Kala Tufaha* (2007) ya B. Omar. Utafiti

huo ulichunguza usemi uliotumiwa kusawiri suala la ukimwi na kubainisha nafasi ya masimulizi hayo katika kukabiliana na changamoto zake. Matini ya utafiti wake ilikuwa tofauti na utafiti huu. Hata hivyo kazi ya Kinara ilijikita katika nadharia ya naratolojia sawa na iliyotumika katika utafiti huu. Kwa hivyo utafiti wake ulifaa sana kwa upande wa usimulizi hasa katika kubainisha kipengele cha usemi wa wahusika katika riwaya teule.

Shitemi (2011) alishughulikia mada ya usimulizi katika utenzi wa Siri Li Asirali. Utafiti huu ulichunguza mbinu za usimulizi katika utanzu wa riwaya kinyume na wa Shitemi ulioshughulikia utenzi. Ijapokuwa aliangalia usimulizi, malengo ya utafiti wake yalikuwa tofauti. Kazi hiyo ilinua kuonyesha kuwa sifa zinazohusishwa na muundo wa simulizi kama riwaya pia zinaonekana katika ushairi. Utafiti huo ulidhihirisha kuwa vigezo vya naratolojia kama vile hadithi, matini na usimulizi ni vipengele vinavyopatikana katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huo ulikuwa wa manufaa hasa katika kubainisha vipengele mbalimbali vya usimulizi pamoja na sifa zinazohusika.

Utafiti wa Arege (2012) ulitathmini mbinu ya usimulizi katika Utenzi wa Rasi 'IGuli. Malengo yalikuwa kubainisha mbinu za usimulizi zinazotumika na kuonyesha nafasi yake katika kuendeleza utenzi pamoja na kuonyesha athari za matumizi ya mbinu hizo katika utenzi husika. Utafiti ulizingatia vipengele vya viwango vya usimulizi na sauti ya usimulizi, wakati na wahusika na uhusika. Utafiti huo ulidhihirisha kuwa vipengele vya usimulizi vinavyohusishwa na utanzu wa riwaya pia vinaweza kupatikana katika utenzi wa Kiswahili. Utafiti huu unanua kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* na

kuonyesha nafasi yake katika upitishaji wa ujumbe. Ingawa matini ya kazi ya Arege ni tofauti na ya utafiti huu, utafiti huo ulinufaisha kazi hii hasa katika uhakiki wa vipengele vya sauti za usimulizi na viwango vya usimulizi pamoja na wakati kwani utafiti umejikita katika nadharia ya naratolojia.

Jebet (2013) alihakiki mchango wa mbazi za Biblia katika ukuzaji wa fasihi andishi ya Kiswahili. Utafiti huo ulinua kubainisha matumizi ya mbazi za biblia na kuonyesha mchango wazo katika kukuza maudhui ya fasihi andishi ya Kiswahili. Pia ulilenga kuonyesha matumizi ya mbazi kama kipengele cha mtindo katika fasihi. Utafiti huo ulibaini kuwa waandishi wa matini teule za fasihi walihusisha mbazi za biblia katika kuzibuni kazi zao. Uligundua kuwa miundo ya kimbazi ilitumika katika uandishi na uwasilishaji wa ujumbe katika matini zilizoteuliwa. Utafiti wa Jebet ulikuwa wa manufaa katika utafiti huu kwani alitumia nadharia ya Naratolojia.

Uhakiki wa Omutimba (2015) ulichanganua usimulizi katika riwaya za Adili na Nduguze, Walenisi na Babu Alipofufuka. Utafiti ulilenga kuonyesha kwamba riwaya hizi zina miundo maalum ya kifomyula inayotumiwa kuendeleza usimulizi wake. Ijapokuwa utafiti wake umejikita katika mada ya usimulizi, malengo ya utafiti huo ni tofauti kwani alikusudia kuainisha vigezo na sifa za usimulizi katika riwaya tatu tofauti; kuonyesha iwapo kuna utaratibu wa kifomyula unaohusika katika uandishi wa riwaya na kutambua kama vigezo na sifa za usimulizi ni njia bora mojawapo ya kuhakiki kazi ya nadhari. Utafiti wake ulijikita katika nadharia ya Miundo na Maumbo Tengamano tofauti na utafiti huu. Hata hivyo utafiti huo ulichangia hasa katika ufafanuzi wa mada ya

usimulizi pamoja na kutoa maoni mbalimbali ya wahakiki kuhusu kipengele hiki.

1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Naratolojia. Hii ni kwa sababu utafiti ulinuia kuchunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Nadharia hii hutumika katika kuchunguza sifa za muundo wa simulizi kwa kugawa vipengele vya simulizi na kuzingatia uamilifu na uhusiano uliopo.

Gennette (1980) anaeleza kuwa Naratolojia hutoa vipengele vinavyoweza kutumiwa katika kuzihakiki simulizi kwa kuchunguza sifa za ndani za muundo wa hadithi, usimulizi wake, mtazamo unaotokea, usemi wa wahusika pamoja na wakati. Nadharia hii inahusu simulizi na usimuliaji wake na ilikuwa ya manufaa katika uainishaji wa vipengele vya usimulizi katika katika riwaya teule.

Kwa mujibu wa Jones (1994) Nadharia ya Naratolojia imewekewa misingi na mawazo ya mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato (428-348) katika andiko lake, “The Republic.” Nadharia hii ilichipuka kutokana na Nadharia ya Umuundo ya Kirusi iliyoasisiwa na Vladmir Propp (1928) ambaye alichunguza muundo katika hurafa za Kirusi. Propp alihakiki simulizi hizi za jadi akilenga dhima na taratibu za masimulizi yaliyohusika. Katika uchanganuzi wake, alitambua kuwa uwepo wa upekee katika muundo unaohusu dhima unapatikana katika kila aina ya simulizi. Shughuli tofauti kuhusu nadharia ya kimuundo zilianza kuchukua mkondo mahsusi baada ya 1958, hasa baada ya tafsiri ya kazi ya Propp ya, *‘Morphology of Folktale’*.

Naratolojia ilianza kama somo baadaye mwaka wa 1966 baada ya uchapishaji wa makala maalum, “Communications” yaliyotengewa uchambuzi wa muundo wa hadithi. Prince (1982) anasema kuwa makala haya yalikusishwa wachangiaji kama Bremond Claude (1970), Tzvetan Todorov (1977), Roland Barthes (1975), Seymour Chatman (1978) miongoni mwa wengine. Hawa ni baadhi ya waasisi wa Naratolojia, wanaorejelewa kama wanaratolojia wa kirasimi. Kazi yao imejengwa kutokana na misingi ya kazi ya Vladimir Propp (1928). Nadharia hii ilikuzwa na ikatumika zaidi nchini Ufaransa hasa katika miaka ya 1970 kama anavyodokeza Jones (1994).

Nadharia hii ilichangiwa na kuboreshwa na wanaratolojia wengine wa kirasimi kama vile Helmut Bonheim (1982), Rimmon Kenan (1983, 2003), Mieke Bal (2004) miongoni mwa wengine. Genette (1980) ni miongoni mwa wanadharia wa Kirasimi walioweka msingi nadharia hii. Katika nakala yake kuhusu, *‘Diskosi Simulizi’* (Narrative Discourse), anafafanua dhana ya naratolojia kama nadharia ya fasihi inayoweza kutumiwa katika kutoa vipengele vinavyoweza kutumiwa kuzihakiki simulizi kwa kuchunguza sifa za ndani za muundo wa simulizi, usimulizi wake na mtazamo unaotokea.

Genette (1980) anasema kuwa kila simulizi ina chembe za usimulizi zinazoweza kuchunguzwa ili kuelewa mpangilio wa simulizi. Anaorodhesha vipengele vikuu vya usimulizi kama vile mpangilio wa matukio, wakati katika matini, hali ya usimulizi na sauti ya usimulizi, idadi ya utokeaji wa matukio katika hadithi pamoja na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika.

Kazi ya Gennette imeboreshwa zaidi na wananaratolojia wengine kama Kenan (2003), Mieke (2004), Manfred (2005), Guillimette na Levesque(2006) miongoni mwa wengine. Bonheim (1982) amejenga kazi yake kutokana na mtazamo wa Gennette (1980) na ameweza kujadili kuhusu jinsi ya kuwasilisha simulizi katika hadithi fupi. Naye Manfred (2005) amejadili kuhusu hadhi ya vipengele vya Naratolojia kama vile usimulizi na hali ya usimulizi na sauti ya usimulizi, mawasiliano katika usimulizi, viwango vya usimulizi, utendaji na uchanganuzi wa hadithi, wakati wa usimulizi, wahusika na uhusika na uwasilishaji wa usemi na fikra katika hadithi. Uainishaji huu ulikuwa na manufaa makubwa katika ubainishaji wa vipengele vya usimulizi.

Wananadharia wengine waliojenga kazi yao kutokana na kazi ya Gennette ni Kenan (1983,2003). Katika makala yake kuhusu Naratolojia, amejadili kuhusu vipengele kama vile mpangilio wa matukio, wahusika katika hadithi, wakati katika matini, mtazamo katika matini, sauti na viwango vya usimulizi, usimulizi wenyewe. Baadhi ya vipengele hivi kama vile usimulizi na uwasilishaji wa matini, wakati katika usimulizi pamoja na sauti na viwango vya usimulizi vilichangia sana katika kuuboresha utafiti huu.

Ingawa kuna wananaratolojia mbalimbali ambao wamechangia katika kuiboresha nadharia ya naratolojia, utafiti huu ulijikita katika mwelekeo wa Gennette (1980). Kimsingi nadharia hii ilitofautisha kati ya kile kinachosimuliwa na jinsi kinavyosimuliwa. Hii ni nadharia iliyojikita katika simulizi, usimuliaji wenyewe na msimulizi wa hadithi. Hivyo kulingana na

uhakiki wa kinaratolojia, simulizi hutambwa kwa jinsi mbalimbali. Jinsi kuu za kimsingi ni zile za uelezaji na uonyeshaji.

Kulingana na maelezo ya Gennette, Plato ametumia dhana '*Daigesia*' kwa maana ya uelezaji na '*Mimesia*' kwa maana ya uonyeshaji. Anasema kuwa simulizi zote zinahusu uonyeshaji na uelezaji ambao huifanya simulizi kuwa halisi na yenye uhai. Hivyo kila simulizi huhusisha msimulizi ambaye anaweza kushiriki katika hadithi anayosimulia au akawa nje ya matukio hayo.

Gennette (1980) anatoa madai kuwa, katika simulizi ni sharti kuwe na kitendo cha kusimulia hadithi fulani, iwe ni andishi au simulizi. Hivyo masimulizi yanaweza kuundwa kwa njia ya kuonyesha namna ya kusimulia hadithi na mfuatano wa matukio au hali ya kutozingatia mfuatano huo kiwakati.

Hivyo mbinu za usimulizi ni muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe unaokusudiwa kwani msomaji huweza kujihusisha na matini kupitia njia ya usimuliaji wa msimulizi. Naratolojia haihusiki tu na hadithi bali hujumuisha hata usimulizi katika ushairi, drama, vyombo vya habari, mazungumzo na matangazo, tanzia, vibonzo, filamu, kama asemavyo Todorov (1977). Hata hivyo kulingana na mawazo ya Gennette, utanzu wa fasihi unaohusishwa zaidi na nadharia hii ni riwaya hasa kutokana na urefu wake na uwezo wa kuchukua miundo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Gennette (1980), mtazamo wa usimulizi ni muhimu katika usimuliaji wa hadithi. Anaeleza kuwa msimulizi kwa wakati wote huwa na dhamira au mwelekeo fulani ambao anakusudia msikilizaji au msomaji wake

ajishirikishe nao. Anasisitiza kwamba katika uhakiki wa matini ni vyema kutambua ‘ni nani anayeona’ na ‘ni nani anayezungumza’ ili kuweza kupata ni nini hasa kiini cha simulizi yenyewe. Katika uhakiki wa simulizi, yanayosemwa na msimulizi na wahusika mbalimbali yanaweza kuchunguzwa kwa kuwa sauti ya msimulizi ndio inayojenga mawasiliano na anayesimuliwa. Yeye ndiye anayetoa mtazamo wa masimulizi, mfuatano wa matukio na kuchagua wakati atakaotumia katika simulizi.

Kwa ujumla Kenan (1983) anaafikiana na mawazo ya Gennette (1980) kuwa mihimili ya hali ya usimulizi na sauti ya usimulizi, viwango vya usimulizi, wahusika na uhusika katika usimulizi, wakati katika usimulizi, dhamira ya usimulizi, mtazamo wa usimulizi na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika ina umuhimu mkubwa katika uhakiki wa naratolojia.

Ingawa usimulizi una mihimili mingi kama ilivyotajwa hapa juu utafiti ulijikita katika mihimili mitatu ambayo ni sauti ya usimulizi na viwango vya usimulizi, wakati katika usimulizi pamoja na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Utafiti huu ulirejelea mtazamo wa mwananaratolojia Gennette (1980) katika kubainisha mbinu za usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Vipengele vilivyotajwa vilifafanuliwa kwa kina kama ifuatavyo.

1.7.1 Sauti ya Usimulizi na Viwango vya Usimulizi

Kulingana na Gennette (1980), simulizi zote zinahusu uonyeshaji na uelezaji ambao huifanya simulizi kuwa halisi na yenye uhai. Hivyo kila simulizi huhusisha msimulizi ambaye anaweza kutambulishwa kwa njia waziwazi au akakosa kutambulishwa katika matukio anayosimulia. Anasema kuwa

mwandishi siye anayesimulia hadithi bali msimulizi ni sauti anayotumia kusimulia hadithi yenyewe. Hivyo matini huwa na vidokezo vya kuonyesha sauti ya msimulizi ambayo hujenga mawasiliano na anayesimuliwa.

Aidha, Gennette anapendekeza kuwa msimulizi anaweza kuwa ama msimulizi ndani anayeshiriki katika matukio anayosimulia na kuweza kujitokeza wazi mbele ya msomaji au akawa nje ya hadithi anayosimulia akakosa kushiriki katika matukio hayo. Kenan anapinga madai haya na kwa kutoa madai kuwa, kuwa; uwe usimulizi wa nje au wa ndani, wasimulizi wanaweza kuwepo au wakakosa kuwepo katika hadithi wanayosimulia.

Naye Stanzel (1984) ana mtazamo tofauti, kwake usimulizi unaweza kuainishwa kulingana na nafsi tatu kutegemea mfumo wa kisarufi kama vile; usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya pili pamoja na usimulizi wa nafsi ya tatu katika kudhihirisha umbali uliopo kati ya hadithi na msimulizi. Hata hivyo mtazamo huu umezua maswali kuhusu, iwapo kitendo cha usimuliaji kinatekelezwa na msimulizi anayehusisha mojawapo ya nafsi tatu za usimulizi, au ni msimulizi anayewasilishwa tu katika simulizi. Mtazamo wa Stanzel (1984) uliwezesha kuchanganua usimulizi ili kuonyesha iwapo msimulizi amehusiha nafsi zote tatu za usimulizi katika kuonyesha umbali kati ya msimulizi na matukio anayosimulia.

Usimulizi pia unaweza kutokea katika viwango mbalimbali kama anavyodokeza Kenan (1983). Anaeleza kuwa viwango hivi vinaenda sambamba na viwango vya simulizi. Hii ina maana kwamba katika simulizi, msimulizi anaweza kusimulia hadithi na katika hadithi hiyo kukawa na

mhusika mwingine anayesimulia hadithi nyingine ndani ya hadithi hiyo kuu. Hivyo hadithi hizi huweza kujenga viwango vya hadithi kidaraja na kila kijihadithi hutegemea hadithi ambamo kimeegemezwa. Katika hadithi kuna msimulizi wa hadithi kuu ambaye ni wa kiwango cha daraja ya kwanza, msimulizi wa daraja ya pili, kisha kuna wa daraja ya tatu au zaidi kutegemea muundo wa simulizi.

Mhimili wa sauti ya usimulizi ulilenga kubainisha nafsi za usimuliaji, na kubainisha iwapo msimulizi anatambulika waziwazi au hatambuliki kamwe mbele ya msomaji katika matukio anayosimulia. Sehemu hii vilevile ilikusudia kuonyesha majukumu mbalimbali ya msimulizi katika hadithi. Nao mhimili wa viwango vya hadithi ungetumika kuainisha wasimulizi kulingana na viwango mbalimbali vya hadithi wanazosimulia.

1.7.2 Wakati katika Usimulizi

Wakati katika simulizi unaweza kufafanuliwa kama uhusiano wa utaratibu wa kupanga muda wa matukio baina ya simulizi na matini. Wahakiki wa Naratolojia kama vile Gennette (1980) na Kenan (1983) wanabainisha wakati kwa njia mbili; Wakati hadithi na Wakati matini. Wakati hadithi umechukuliwa kuonyesha wakati unaotumika katika hadithi kutokea mwanzo mpaka mwisho wa usimulizi wake. Usimulizi unaweza kuchukua baina ya siku moja au miaka mingi kiasi cha kuhusisha vizazi vingi. Nao wakati matini huchukuliwa kuwa wakati inayochukua matini fulani kusomwa. Muda wa usomaji wa hadithi hutegemea urefu wa matini inayohusika.

Kipengele cha wakati kinaweza kuhakikiwa kwa kuchunguza vigezo vingine kama mpangilio wa matukio, muda wa matukio na idadi ya utokeaji wa matukio. Mpangilio wa matukio hurejelea ule mfuatano wa matukio katika hadithi kulingana na uwasilishaji wake. Gennette (1988) anatambua kuwa katika simulizi ni nadra kudumisha mpangilio wa matukio, hivyo matukio yanaweza kuwasilishwa kulingana na mfuatano kiwakati au yakasimuliwa bila ya uzingatifu wa kaida ya mfuatano huo.

Kulingana na Kenan (2002), uhitilafiano huu huitwa ‘anakroni’ na huweza kuiainishwa kwa namna mbili kama; Analepsia ambapo msimulizi huelezea tukio lililotokea wakati uliopita anaposimulia matukio ya wakati uliopo katika hadithi kuu. Nayo prolepsia huwa usimulizi wa matukio ya wakati ujao kabla ya kutendeka kwake na huweza kutofautishwa na udokezi wa tukio la wakati ujao. Hali hii inadhihirisha hadithi inaweza kusimuliwa kwa kuhusisha mbinu rejeshi au mbinu elekezi. Kenan anasema usimulizi huu wa kielekezi mbele si maarufu sana ila hutumika zaidi katika biblia.

Muda ni kigezo kingine muhimu cha wakati kinachoonyesha muda ambao tukio limechukua, yaweza kuwa kipindi kirefu au kifupi kama asemavyo Kenan (1983). Hali hii huzingatia muda inayochukua matini fulani kusomwa. Muda hudhihirika katika jinsi tano tofauti, mojawapo ikiwa ni muhtasari inayohusu hali ambapo muda wa usomaji wa matini au usemi unachukuliwa kuwa mfupi kuliko ule wa hadithi. Nao Udondoshi hurejelea pale ambapo maelezo fulani yamerukwa au kuepukwa bila kutajwa katika matini ili

kufupisha muda wa usimulizi. Hali hii huweza kuonyeshwa kwa njia iliyo wazi au isiyokuwa wazi katika simulizi.

Kulingana na Toolan (1988:56), mtuo huwa wakati ambapo matukio katika hadithi yanakatizwa ili kuachia nafasi maelezo mengine katika hadithi. Katika hali hii, msimulizi hutoa ufafanuzi kuhusu sifa za mhusika fulani au hata kumrudisha msomaji katika matukio ya wakati uliopita. Anapofanya hivyo hakuna utendaji wowote unaoendelea. Hali hii husababisha muda wa usimuliaji wa hadithi urefushwe, hivyo kuongeza muda wa usomaji wa hadithi.

Isitoshe katika onyesho, muda wa usimulizi wa hadithi huwa ni mrefu kuliko maelezo ya matini. Onyesho hutimiza majukumu sawa na mazungumzo kama anavyoeleza, Bonheim (1982). Anasema kuwa mazungumzo huwa ni mafupi na huweza kuchukua theluthi moja ya simulizi katika kila ukurasa. Msimulizi huhusisha onyesho ili kutoa mtazamo wa wahusika kuhusu ulimwengu wao pamoja na kuonyesha migogoro inayojitokeza miongoni mwao. Hali hii humfanya msomaji kuwaelewa wahusika na hata kujihusisha na hisia zao.

Jinsi nyingine inayodhihirisha muda kama kipengele cha wakati ni uendelezaji. Kulingana na Bonheim (1982) hii ni hali ambapo wakati wa kueleza matini huwa mrefu kuliko wakati wa kuisimulia hadithi. Hali hii hutokea wakati msimulizi anapoangazia zaidi sifa za wahusika wake, ndoto au mazingira yao badala ya kuendelea kusimulia hadithi iliyopo. Usimuliaji wa hadithi hucheleweshwa na kuifanya matini inayohusika kuwa ndefu. Kipengele cha muda pamoja na vigezo vyake viliwezesha kuchunguza muda unaotumika katika usimulizi wa matukio mbalimbali.

Kigezo kingine cha wakati ni kile cha Idadi ya utokeaji wa matukio. Kwa mujibu wa Kenan (2003) kigezo hiki kinarejelea uhusiano kati ya mara ngapi tukio fulani linatokea katika hadithi na mara ngapi tukio hilo limesimuliwa. Uhusiano kati ya matukio hadithini na usimulizi wake hudhihirika kwa njia tatu ambapo; Tukio linalofanyika mara moja linaweza kusimuliwa mara moja; tukio linalofanyika mara moja linasimuliwa mara nyingi au lile linalotokea mara kadha kusimuliwa mara moja. Kigezo cha idadi ya utokeaji wa matukio kingetumika katika kuchunguza uhusiano kati ya matukio na mara ambazo matukio hayo yalitokea na kusimuliwa katika simulizi.

Mhimili wa wakati ulilenga kuchunguza iwapo matukio katika riwaya teule yamefuatana kiwakati au yamekiuka kaida za mfuatano huo katika uwasilishaji wa hadithi. Utafiti ulilenga kutathmini muda uliochukuliwa na matukio yaliyosimuliwa, yaani kudhihirisha iwapo masimulizi yamechukua kipindi kirefu au kifupi kusimuliwa. Hivi ni kusema kwamba matukio yanapochukua muda mrefu kusimuliwa, muda wa usomaji wa hadithi huweza kuongezeka.

1.7.3 Uwasilishaji wa Usemi na Fikra

Usemi unaweza kuwa wa msimulizi unaojulisha matukio yanayosimuliwa au maneno ya wahusika ambao aghalabu huzungumza kwa kuhusisha vitendo fulani kama wanavyodokeza Leech na Short (1981:s.10). Mwandishi anaweza kuwasilisha unenaji katika njia mbili kuu, yaani usemi halisi na usemi wa taarifa.

Usemi halisi kulingana na Short (1991) ni uwasilishaji wa maneno kama yalivyotamkwa moja kwa moja na wahusika kwa kutumia alama za mtajo. Hali

hii hufuatiwa na ushawishi kuonyesha ni nani anayesema maneno hayo. Unenaji huo huhusisha matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza kama ushahidi wa kuwepo kwa msimulizi karibu na wahusika wanaozungumza. Hali kadhalika mwandishi anapowasilisha usemi wa taarifa, maneno yaliyosemwa yanaripotiwa pasipo kuweka alama za mtajo kwa kutumia viwakilishi vya nafsi ya tatu.

Mwandishi pia huweza kuhusisha mifumo mingine ya unenaji ilio huru zaidi kama vile usemi halisi huru na usemi taarifa huru. Usemi halisi huru huonyesha kuwepo kwa msimulizi bila kutumia alama za mtajo na kishazi tangulizi kinachotarifu juu ya hali fulani kama ilivyo katika usemi halisi. Nao usemi taarifa huru kama asemavyo Wamitila (2008) ni zao la kufanyia mabadiliko usemi taarifa kwa kuondoa maneno yanayoashiria usemi taarifa na pengine kuchukua baadhi ya sifa zinazohusishwa na usemi halisi kama vile kuonyesha hisia, kutumia mfumo wa maswali na kunukuu maneno ya msemaji.

Mbali na unenaji mwandishi huwasilisha fikra za wahusika wake kuhusu matukio mbalimbali. Njia zinazotumiwa kuwasilisha fikra hizo ni sawa na zile za kuwasilisha unenaji kama anavyodai Short (1991). Mbinu hii huweza kuangazia mivutano ya kimawazo inayompitia mhusika akilini kuhusiana na hali mbalimbali.

Fikra huwasilishwa kwa njia mbili kuu; Mojawapo ikiwa fikra halisi ambapo mawazo ya mhusika huwasilishwa moja kwa moja kwa kutumia alama za mtajo. Pili fikra halisi huru zinazoonyeshwa bila kutumia alama za mtajo ambapo kishazi tangulizi huwa kimeondolewa. Mwandishi pia hutumia fikra

halisi na taarifa zilizo huru kuripoti anachofikiria mhusika kama njia ya kuendeleza maudhui katika riwaya. Mhimili wa usemi na fikra umetumika katika kubainisha aina mbalimbali za usemi na fikra za wahusika na kuonyesha matumizi yake katika uendelezaji wa hadithi.

1.8 Mbinu za Utafiti

1.8.1 Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumiwa katika utafiti ni wa kuchanganua matini ya riwaya ya *Dharau ya Ini*. Utafiti umejikita katika fasihi andishi hasa riwaya ya Kiswahili. Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ni ya kimaksudi. Sampuli ya mtafiti katika fasihi andishi pia iliteuliwa kimaksudi kuwa riwaya ya sasa ya Kiswahili. Riwaya hii iliteuliwa kwa vile imehusisha matumizi mapana ya mbinu za usimulizi zenye upya na upekee katika muundo wake. Riwaya teule ilisaidia katika kubainisha mbinu mbalimbali za usimulizi kulingana na malengo ya utafiti.

Riwaya ilisomwa kwa kina na mafungu yanayoonyesha sifa za mbinu za usimulizi yalidondolewa kutoka kwenye matini na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo. Utafiti haukuchanganua mbinu zote za usimulizi bali ulijikita katika mbinu mahsusi zinazojitokeza katika sehemu kubwa ya matini. Mfano wa mbinu hizi ni sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi, wakati katika usimulizi na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya kimaielezo.

1.8.2 Eneo la Utafiti

Utafiti ulijikita maktabani, hususan maktaba ya Chuo kikuu cha Kenyatta. Katika maktaba mtafiti alipata makala yaliyoeleza kuhusu misingi ya nadharia ya naratolojia pamoja na yaliyoandikwa kuhusu usimulizi katika kazi za kinathari. Mtafiti alisoma kwa kina majarida, tasnifu na vitabu mbalimbali. Vilevile vitabu-meme na majarida-meme yanayohusiana na usimulizi yalirejelewa.

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli maksudi ilitumiwa katika kuteua utanzu wa fasihi andishi. Sampuli lengwa katika utafiti ni usimulizi. Riwaya ya *Dharau ya Ini* ilitiuliwa kwa mbinu maksudi kwa sababu ina data inayohitajika. Riwaya yenyewe ni ya karne ya ishirini na moja na imetungwa na Kyalo Wamitila ambaye ametunga riwaya zingine nyingi zenye matumizi mapana ya mbinu za usimulizi. Riwaya teule inasheheni ukwasi mkubwa zaidi wa mbinu za usimulizi zenye upya na upekee katika muundo wake miongoni mwa zingine alizotunga.

1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Data ya utafiti ilikusanywa kwa kusoma kwa kina riwaya ya *Dharau ya Ini* kwa kuzingatia malengo na nadharia ya utafiti. Data yenyewe ilihusu usimulizi. Mtafiti alidondoa mafungu yenye sifa za usimulizi kutoka kwenye matini kwa kuzingatia; sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi, wakati katika usimulizi pamoja na uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika.

1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilihusisha ubainishaji wa mbinu za usimulizi. Data ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia maswali, malengo, mihimili ya nadharia, pengo na mipaka ya utafiti. Matini katika riwaya ilichanganuliwa kwa kuzingatia sifa za usimulizi. Data ilipangwa kulingana na aina za usimulizi na matumizi yake. Uchanganuzi wenyewe ulihusisha kwanza; kubainisha matumizi ya sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi, kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi pamoja na kudhihirisha matumizi ya uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa simulizi.

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Baada ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya maelezo ya kinathari. Mafungu yenye sifa za usimulizi na matumizi yake yaliangaziwa. Kazi hii iliwasilishwa kwa sura tano. Sura ya kwanza ina utangulizi, mada ya utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia. Sura ya pili imeangazia matumizi ya sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi. Sura ya tatu imeonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya. Sura ya nne imejikita katika uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika upitishaji wa ujumbe. Sura ya tano imezingatia muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

1.9 Kiishilio

Sura imezingatia usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia. Muundo wa utafiti ambao ni wa kimaelezo pia umerejelewa. Mahali pa utafiti pameangaziwa kuwa maktabani. Sampuli lengwa na jinsi ilivyoteuliwa pia imezingatiwa. Mwisho njia za ukusanyaji data na uchanganuzi wa data zimefafanuliwa na uwasilishaji wa data husika umerejelewa.

SURA YA PILI

UAINISHAJI WA SAUTI ZA USIMULIAJI NA VIWANGO VYA USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA *DHARAU YA INI*

2.0 Utangulizi

Sura hii imeainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi katika matini ya riwaya ya *Dharau ya Ini*. Utafiti umejikita katika nafsi ya usimuliaji, uonekanaji wa msimulizi, mahusiano ya wakati wa usimulizi na nafasi ya msimulizi katika hadithi. Utafiti ulinua kudhihirisha iwapo msimulizi anashiriki katika matukio anayosimulia na iwapo anatambulika wazi mbele za msomaji au anasimulia akiwa nje ya matukio hayo akakosa kuonekana kamwe. Utafiti ulichunguza iwapo msimulizi amehusisha matumizi ya nafsi zote tatu za usimulizi katika hadithi. Mahusiano ya wakati wa usimuliaji wa hadithi yalichanganuliwa ili kubainisha kama msimulizi amehusisha nyakati tatu kuu za usimulizi. Vilevile mtafiti alikusudia kubainisha majukumu mbalimbali ya msimulizi katika hadithi. Sura hii pia ilichanganua viwango vya usimulizi ili kubainisha iwapo vinaenda sambamba na viwango vya hadithi. Sehemu hii imeanza kwa kuangazia uainishaji wa sauti za usimulizi na kuonyesha matumizi yake katika riwaya.

2.1 Sauti ya Usimuliaji

Kulingana na Gennette (1980) na Stanzel (1984) msimulizi wa hadithi huchukua nafasi muhimu katika usimulizi wa matukio, kwani ni sharti aamue njia atakazotumia katika kuwasilisha ujumbe. Gennette (1980) anaeleza kuwa kila msimulizi huzingatia mwelekeo mahsusi ambao anakusudia msomaji wake ajishirikishe nao katika simulizi. Anasisitiza kwamba katika uhakiki wa matini

ni vyema kutambua ‘ni nani anayeona’ na ‘ni nani anayezungumza’ ili kuweza kupata ni nini hasa kiini cha simulizi yenyewe. Katika uhakiki wa simulizi, yanayosemwa na msimulizi na wahusika yanaweza kuchunguzwa kwa kuwa sauti ya msimulizi ndiyo inayojenga mawasiliano na anayesimuliwa. Msimulizi hutumika kama chombo muhimu katika ukuzaji wa ujumbe kwani ndiye anayetoa mtazamo wa masimulizi, mfuatano wa matukio na hata kuchagua wakati atakaotumia katika simulizi.

Gennette (1980) anapendekeza kuwa mwandishi siye msimulizi bali msimulizi ni sauti anayotumia kusimulia hadithi. Sauti hii inaweza kuwa ya mmoja wa wahusika au ikawa ya msimulizi anayejulikana au asiyejulikana. Msimulizi anapotoa maoni yake na kuelezea nia yake kuhusu tukio fulani, kimsingi huwa anaonyesha uhusiano wake na anachokizungumzia au kusimulia. Uhusiano huu ni muhimu kwa sababu huonyesha ni kutokana na mtazamo upi ambapo matukio yanatazamwa au kuhukumiwa.

Hivyo kulingana na Gennette, hadithi huwasilishwa kwa njia maalum inayomfanya msomaji kukumbana na mtazamo fulani wa hadithi. Hali hii huweza kuzua maswali kama, je, ni mtazamo upi unaotumika kusimulia hadithi? Na je, mtazamo huu unatokea wapi? Haya ni baadhi ya maswali yanayoshughulikiwa katika sura hii.

Kwa mujibu wa Gennette (1988) hadithi inaweza kusimuliwa kwa mitazamo miwili mikuu ambayo ni; usimulizi ndani na usimulizi nje. Katika mtazamo wa ndani, msimulizi hushiriki katika matukio anayosimulia kama mhusika na huweza kuonekana wazi mbele ya msomaji. Leech na Short (1981) wanaeleza

kuwa usimulizi huu hujenga uhusiano wa kibinafsi kati ya msimulizi na msomaji. Hali hii humfanya msomaji kupenda kujitambulisha na mhusika katika hadithi hiyo na anaweza kukubaliana na mtazamo wake. Mtazamo wa ndani unaweza kubadilika kutoka mhusika mmoja hadi mwingine. Sauti inayosimulia katika mtazamo wa ndani huchukua kiwakilishi 'ni' cha nafsi ya kwanza.

Kwa upande wa pili matukio yanaweza kuwasilishwa kwa mtazamo wa nje ambapo msimulizi husimulia hadithi akiwa nje ya matukio hayo. Msimulizi huweza kuyatazama matukio anayosimulia akiwa mbali. Hivyo hatambuliki wazi mbele ya msomaji. Katika usimulizi huu kiwakilishi 'a' cha nafsi ya tatu hutumika.

Stanzel (1984) anatofautiana na mawazo ya Gennette (1980) kuhusu mtazamo wa usimulizi. Anasema usimulizi unaweza kuainishwa katika nafsi tatu kutegemea mfumo wa kisarufi. Mtazamo huu umezua mjadala miongoni mwa wananaratolojia ambao wameuchukulia kuwa wa kupotosha. Mjadala huu umezua maswali kuhusu iwapo ni msimulizi anayetenda kitendo cha usimuliaji unaouchukua mojawapo ya nafsi tatu za usimulizi au ni msimulizi anayewasilishwa tu katika hadithi. Sehemu hii ilichanganua na kuainisha usimulizi kulingana na mfumo wa kisarufi kuzingatia matumizi ya nafsi tatu za usimulizi katika kudhihirisha umbali uliopo baina ya msimulizi na hadithi anayosimulia.

Naye Kenan (2003) anatoa maoni tofauti kuwa usimulizi unaweza kuainishwa kupitia viwango mbalimbali vya hadithi. Kuna usimulizi wa kiwango cha

kwanza ambapo msimulizi anasimulia hadithi ya msingi na aghalabu huwa ni hadithi inayotangulia katika simulizi. Msimulizi husimulia kisa kinachomhusu yeye mwenyewe binafsi na wala si kuhusu wahusika wengine. Usimulizi katika kiwango cha pili, msimulizi husimulia hadithi kuu akiwa nje ya matukio anayosimulia. Hii ndio hadithi inayoambatana na ile hadithi ya kimsingi.

Kulingana na Kenan, msimulizi au mmojawapo wa wahusika katika hadithi kuu anaweza pia kusimulia hadithi nyingine ndani ya hiyo kuu. Hivyo kunaweza kuwa na msimulizi mwingine katika kiwango cha tatu au cha nne ikitegemea na muundo wa hadithi. Mhimili huu wa viwango vya usimulizi ulimwezesha mtafiti kuchunguza uainishaji wa wasimulizi kulingana na viwango mbalimbali vya hadithi.

Uchanganuzi kuhusu mitazamo katika usimulizi uliegemea katika maoni ya wananaratolojia, Gennette (1980), Kenan (1983) na Stanzel (1984). Utafiti ulichanganua mitazamo mbalimbali kwa kuzingatia kigezo cha msimulizi ndani, msimulizi nje, nafsi zote tatu za usimulizi pamoja na viwango vya usimulizi katika hadithi. Vilevile sehemu hii ilichanganua mahusiano ya wakati wa usimulizi na ikaonyesha nafasi ya msimulizi katika hadithi ifuatavyo;

2.1.1 Usimulizi wa Ndani

Kulingana na Gennette (1980) huu ni mtazamo wa usimulizi ambapo msimulizi wa hadithi ni mhusika mmojawapo kwenye ulimwengu wa hadithi anayosimulia. Sauti inayosimulia huweza kutumia nafsi ya kwanza inayochukua kiambishi ‘ni’ au kiwakilishi ‘mimi’ wakati msimulizi anaposimulia kuhusu matendo yake na wahusika wake au anapowashirikisha

wahusika hao katika dayolojia. Wahusika hao huachwa wazungumziane hali inayowapa nafasi ya kuwasilisha hisia zao wazi mbele ya wasomaji. Matumizi ya kiambishi 'ni' hudhihirisha kuwepo kwa msimulizi katika matukio anayosimulia.

Usimulizi wa ndani kama anavyosisitiza Gennette (1988) huchangia katika kuyafupisha masafa ya kihisia au ya kiuajumi yaliyopo kati ya mhusika na msomaji. Hivyo ni rahisi kwa wasomaji kujitambulisha na msimulizi na kumwamini kuliko ambavyo ingekuwa katika usimulizi katika nafsi ya tatu. Ni rahisi kujitambulisha na viwakilishi, 'mimi' au 'ni' kuliko 'yeye' au 'a.' Hali hii inaifanya hadithi ifungamane vizuri hivyo kumfanya msomaji anaposoma hadithi amfuatilie msimulizi na kukubaliana na mtazamo wake katika simulizi.

Riwaya husika imehusisha msimulizi ndani katika matukio mbalimbali. Msimulizi katika hadithi ya kimsingi ametambulishwa kama Lila. Anasimulia kuhusu kisa kinachomhusu yeye mwenyewe kwa kuhusisha kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza 'ni.' Hali hii inadhihirisha kuwepo kwake katika hadithi anayosimulia. Msimulizi anatambulika wazi kuwa ni mwanamke na anafanya kazi kama mwandishi wa habari katika shirika la habari la Mpapure, jijini Kitambasye. Anasema ifuatavyo:

Ulikuwa wakati wa likizo yangu fupi baada
ya kuanza kazi kama mrasili wa habari, jijini
Kitambasye... Nilipokuwa nyumbani, ghafla
kumbukumbu ya baba
ilinijia...(uk.3)

Lila anaeleza jinsi kumbukumbu kuhusu babake ilivyomjia akiwa likizoni kwao nyumbani. Matukio haya yanamhusu yeye binafsi na wala sio watu wengine. Matumizi ya kiambishi ‘ni’ katika kauli hii yanadhihirisha uwepo wa msimulizi katika matukio anayosimulia. Msimulizi wa aina hii huweza kuwa na mkabala mmoja tu maalum kwani mawazo anayoyatoa kuhusu tukio, mtu au hali huwa yake tu na wala hayahusu watu wengine kama anavyodokeza Wamitila (2002).

Msimulizi anatawala katika matukio ya hadithi anayosimulia na wala hana uwezo wa kumaizi kila kitu kinachowahusu wahusika wake, mandhari yao na hata mawazo yao. Msimulizi anaendelea kueleza kuhusu mazungumzo yake na mama yake na jinsi yalivyomchochea kusafiri mbali ili kupazuru mahali walipokuwa wakiishi kabla ya kuhama. Anaeleza hivi:

Usimulizi huo nao ukanichochea nikarudi
kwenye hilo jungu la matukio. Hamu ya
kutaka kwenda alikozikwa baba ikanipapa.
Mimi na udaku wa mwandishi wa habari
nikawa sishauriki. Nika-shika njia...(uk. 3).

Msimulizi anaeleza jinsi usimulizi wa mamake kuhusu kifo cha babake ulivyomchochea kwenda mahali alikofia babake. Mamake hangeweza kumzuia asiende kwani kama mwandishi wa habari hangeshuriwa vingine. Katika usimulizi wake, Lila anahusisha usimulizi wa nafsi ya kwanza kwa kutumia kiambishi ‘ni.’ Matumizi ya kiambishi hiki yanadhihirisha kuwa msimulizi ni mshiriki katika hadithi anayosimulia na hivyo ameweza kufupisha masafa ya kiujumi baina yake na msomaji.

Usimulizi kama huu unamfanya msomaji ajihusishe na usimulizi wake na kuelewa hadithi anayoisimulia. Msimulizi anasema kuwa alishika njia na kuelekea upande wa chini kama aliyekuwa akielekea penye mwanamke wa jiwe. Anaendelea kusimulia ifuatavyo:

Nikapita lilipokuwa lango la kuingia kwenye uwanja wa Munene mwenyewe. Nikaya-elekeza macho kwenye ule mlima tena. Nilivyoga kwenye uwanja wa kibanda cha mzee Mbulu...(uk.4)

Msimulizi anajitokeza mbele ya msomaji kama aliye huru katika kutoa maelezo kuhusu safari anayoifunga kuelekea alikozikwa babake. Anapita na kuelekea kwenye lango la Munene na kupenya kwenye uwanja wa mzee Mbulu. Alihitaji kumwona mzee huyu kabla aendelee na safari.

Lila anatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza kueleza kuhusu harakati za safari yake. Msimulizi anamshirikisha msomaji katika usimulizi wake moja kwa moja na kumfanya ajihusishe na hisia zake kama anavyodokeza Gennette (1980:248). Maelezo haya ya msimulizi yanadhihirisha kuwa Lila anayasimulia matukio ambayo yeye ni mshiriki. Kiambishi cha nafsi ya kwanza, 'ni' kimetumika kudhihirisha kuwa, kimtazamo, umbali uliopo baina ya msimulizi na hadithi ni mfupi.

Msimulizi wa hadithi hii ya kimsingi ndiye mhusika mkuu na mshiriki katika hadithi anayosimulia. Msimulizi huyu anatambulika wazi mbele ya msomaji kama Lila. Anamhusisha msomaji katika hisia zake kuhusiana na changamoto anazopitia katika safari hiyo. Anaeleza hivi:

Nikatembea kwa hadhari; mwinuo wa miguu
taratibu kasha chini juu...Chiiiiini; nikauzun-
guka ule mpera uliokuwa na chungu...moyo
wangu ukanituta kwa mapigo ya mfululizo
kama mwili wa chura ...(uk.6)

Lila anasimulia kuhusu changamoto anazokabiliana nazo akiwa safarini akielekea alikozikwa marehemu babake. Anaeleza vile alivyochukua tahadhari ili kuyaepuka madhara yoyote kule njiani. Matumizi ya kiambishi 'ni' yanaashiria kuwepo kwa msimulizi katika matukio anayosimulia. Msimulizi anasimulia kuhusu maisha yake mwenyewe na kuonyesha hisia zake wazi kuhusu hali mbalimbali alizokabiliana nazo katika safari yake.

Zaidi ya mhusika mkuu kuna wahasika wengine mbalimbali wanaosimulia hadithi huku wakishiriki katika matukio wanayosimulia. Kwa mfano mhusika kama Derby pia ni mwanahabari katika shirika la habari la Mpapure na anaonekana akimwambia mwenyekiti wa shirika hilo ifuatavyo:

Nijuavyo mimi kinachohusika hapa ni
uchunguzi na uandishi wa habari; sio
kupigana ati hatuwezi! (uk.117)

Derby anayasema maneno haya baada ya mwenyekiti kumtaka yeye na Lila waachane na uchunguzi kuhusu suala la Madongoporomoka. Silverstein alihisi kwamba walikuwa wanajiingiza matatani kwa kuingilia masuala yanayohusu viongozi wa ngazi za juu serikalini. Derby na mwanahabari mwenzake Lila walikuwa wanachunguza suala la ufisadi lililohusisha viongozi wa ngazi za juu serikalini. Viongozi hao walikikashifu kitendo hicho na kuamua kuwakomesha kwani walionelea kuwa masuala ya kisiasa yalipaswa kushughulikiwa na wanaume pekee.

Msimulizi ni mhusika mjenzi katika hadithi na anashirikishwa katika usimulizi kwa muda mfupi kisha anatoweka machoni mwa msomaji. Msimulizi ambaye ni mmojawapo wa wahusika anaweza kutambulika kuanzia uonekanaji mdogo hadi ule mkubwa kama asemavyo Kenan (1983).

Maelezo yanayotolewa hapa yanadhihirisha kwamba msimulizi anayesimulia hadithi si lazima awe mwandishi bali anaweza kuwa mmojawapo wa wahusika katika hadithi kama Derby. Kenan (1983) anasisitiza kuwa ingawa mwandishi hasimulii hadithi moja kwa moja, huweza kuingiliana na msimulizi wake ambaye humwakilisha katika usimulizi.

2.1.2 Usimulizi wa Nje

Kulingana na Gennette (1988:245-247)) usimulizi wa nje ni mtazamo wa usimulizi ambapo msimulizi hajifungi kwenye ulimwengu wa hadithi bali huwa nje yake. Msimulizi anaweza kusimulia hadithi bila kushiriki katika matukio anayosimulia. Msimulizi huyu hujitokeza nyuma ya matukio na kukosa kutambulika kamwe kwa msomaji. Hata hivyo msimulizi huyu ana uwezo wa kuchunguza masuala na mambo ambayo hayawezekani kwa mtazamo wa ndani. Katika riwaya teule kuna sehemu zinazosimuliwa huku msimulizi akiwa nje ya hadithi. Msimulizi anatambulishwa kwa matumizi ya viambishi vya nafsi ya tatu ambapo mofu {a} imetumika pamoja na kitenzi.

Katika sura ya pili msimulizi anaposimulia kuhusu sifa za Munene anahusisha viwakilishi vya nafsi ya tatu na kusema kuwa:

Alikuwa mwepesi wa kujua njia za mkato za
kumwezesha kuifikia hatima ya safari ya

u hai wake. Moyoni alikuwa mwindaji aliyekuwa na ujuzi wa kujua wakati wa kuwashambulia wanyama wanapofika majini kunywa maji (uk.9)

Msimulizi anasimulia jinsi Munene alivyopenda kutumia njia za mkato kutimiza malengo yake. Anasema kuwa mhusika huyu alijua jinsi ya kukabiliana na watu maishani hasa walipohitaji msaada wake. Usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika kuwasilisha tabia za Munene. Kiambishi ‘a’ katika neno ‘alikuwa’ kimetumika kudhihirisha kuwa msimulizi anasimulia matukio haya akiwa nje ya hadithi anayosimulia.

Msimulizi anayesimulia hadithi akiwa nje ya matukio anayosimulia, huonyesha ujuzi wa kila jambo na ana ufahamu wa kila kitu pamoja na mawazo ya wahusika anaosimulia kama wanavyodokeza Chimera na Njogu (2002). Hali hii inatokana na sababu kuwa msimulizi huyu ana uwezo wa kuyaona matukio hayo akiwa mbali kwani si mshiriki katika hadithi hiyo. Maelezo ya msimulizi yanaonyesha kuwa anafahamu tabia za mhusika wake pamoja na kuyaona mawazo yao kwa kina.

Katika (uk.10) aya ya pili msimulizi anasimulia kuhusu maisha ya utotoni ya Munene kwa kutumia nafsi ya tatu. Anaeleza jinsi mhusika huyu alivyokua huku akiiga tabia na mienendo hasi ya babake kivu. Anaeleza kuwa:

Akiwa na umri wa miaka saba hivi, alishauchonga ulimi kwa lugha ya kuwa-amrisha vibarua waliokuwa wakiitunza bus-tani ya matunda katika shamba lao (uk.11)

Malezi ya Munene akiwa na umri mdogo yamefichuliwa. Vilevile msimulizi amefafanua jinsi mzee Kivu alivyomlea mwanawe kwa kumdekeza. Hakuwa anamwelekeza mwanawe wala kumsuta alipofanya kitendo kisichofaa. Hali hiyo iliyaadhiri maisha na mienendo ya mwanaye baadaye.

Muktadha huu unadhihirisha kuwa usimulizi uliotumika ni wa nafsi ya tatu na unaonyesha wazi kuwa msimulizi anafahamu mienendo ya wahusika wake pamoja na matukio yote yanayowazingira kwa kina. Msimulizi anaendelea kusema kuwa:

Munene alipojiunga na shule ya sekondari aliingia mjini na kuzilimbuka raha za maisha ya huko. Akili yake haikuwa na subira ya kuyafyonza masomo ambayo aliyaona kama udhia mtupu (uk.15)

Munene akiwa katika shule ya sekondari hakutilia masomo yake maanani kama anavyoeleza msimulizi. Aliamua kususia shule na kwenda kustarehe mjini. Msimulizi anatumia mtazamo wa nje wa usimulizi kwa kuhusisha kiambishi ‘a’ katika neno ‘aliingia’ kuonyesha kuwa kisa anachosimulia kinahusu mhusika mwingine na wala si kisa chake binafsi.

Mfano mwingine wa mtazamo wa nje unajitokeza katika (uk.152) msimulizi anaposimulia kuhusu imani na itikadi alizokuwa nazo Munene. Anaeleza kuwa:

Munene hakuwa mtu wa waganga ingawa alikuwa mshirikina ajabu... Alianza kuamini kuwa lazima watu waliokuwa wakimwonea gere kutokana na maendeleo yake walikuwa wanashirikiana kumroga...(uk.152)

Msimulizi anaeleza jinsi Munene alivyokuwa mshirikina wa ajabu ingawa alionyesha hofu kuwa kuna watu waliokuwa wanamwonea gere kutokana na ufanisi wake. Hivyo msimulizi anamfichulia msomaji imani, mawazo na hisia za mhusika wake. Hapa usimulizi wa nafsi ya tatu unatumika kuonyesha kuwa msimulizi hajajifunga kwenye ulimwengu wa hadithi tu bali yu nje ya matukio anayosimulia.

Maelezo haya kuhusu imani na hisia za Munene yanadhihirisha kuwa msimulizi ana uwezo wa kuingia katika akili za mhusika wake na kumfichulia msomaji mawazo ya mhusika huyo kama anavyodokeza Wamitila (2002). Mfano mwingine wa usimulizi nje unajitokeza katika (uk.33). Msimulizi wa nafsi ya tatu anatoa maelezo kuhusu tabia na mienendo ya mzee Mbulu. Anasema kuwa:

Mbulu alikuwa na vioja vikubwa. Watu waliokwenda kisimani walimwajabia. Alishi -nda chini ya munga uliokuwa nje ya kibanda chake, akimsimulia mtu asiye-kuweko visa mbalimbali...(uk.33)

Msimulizi anamweleza msomaji jinsi mzee Mbulu alivyoshinda ameketi chini ya mti nje ya kibanda chake huku akisimulia visa mbalimbali kwa mtu asiyekuwepo. Anasema kuwa vioja vya mzee huyo viliwafanya wapita njia wamwajabie.

Hali hii inaonyesha kuwa msimulizi ana uwezo wa kuyaelewa matendo ya wahusika, mawazo yao na mazingira waliomo kwa kina (Gennette, 1988). Maelezo haya yanadhihirisha kuwa msimulizi anasimulia hadithi akiwa nje ya matukio anayosimulia kwa kuhusisha matumizi ya nafsi ya tatu 'a' katika neno,

‘alikuwa’ na ‘alishinda.’ Msimulizi anapotumia mtazamo huu ana uwezo wa kuona kwa mbali na kuchunguza matukio ambayo hayaweze kani kwa mtazamo wa ndani.

Uchanganuzi huu umeonyesha kuwa riwaya teule imehusisha msimulizi anayeshiriki katika matukio anayosimulia hivyo anaonekana wazi mbele za msomaji. Usimulizi wa aina hii hujenga uhusiano wa kibinafsi kati ya msimulizi na msomaji hali inayomfanya msomaji kupenda kujitambulisha na mhusika katika hadithi hiyo na anaweza kukubaliana na mtazamo wake kama anavyodokeza Short (1991). Katika sehemu zingine amehusisha msimulizi asiyejulikana wazi mbele ya msomaji kwani anasimulia hadithi akiwa nje ya matukio hayo.

Kulingana na maoni ya Short (1991), mtazamo wa ndani unaweza kubadilika kutoka mhusika mmoja hadi mwingine, hali inayotoa picha kamili kuhusu matukio ya hadithi kwa vile inaonyesha jinsi wahusika mbalimbali wanavyoangalia na kuhukumu matukio kwa mwelekeo tofauti.

Utafiti vilevile ulichanganua mtazamo wa usimulizi kulingana na maoni ya Stanzel (1984). Usimulizi uliainishwa na kuchanganuliwa kwa misingi ya kisarufi kulingana na nafsi zote tatu za usimulizi.

2.2 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Kulingana na Stanzel (1984) huu ni usimulizi unaohusisha matumizi ya nafsi ya kwanza. Anasema kuwa usimulizi huu huainishwa kulingana na kiwakilishi kiambishi ‘ni’ au ‘mimi’ katika usimulizi wa matukio. Msimulizi wa nafsi ya

kwanza husimulia kuhusu matendo yake mwenyewe na wala si ya wahusika wengine. Usimulizi huu hauwezi kusawiri hisia, mawazo na hata ndoto za wahusika wengine kama usimulizi wa nafsi ya tatu.

Lanser (1981:161) anaongezea kwa kusema kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza hawezi kuwa mahali kuwili kwa wakati mmoja. Isitoshe hawezi kujua yatakayotendeka siku zijazo wala hawezi kusimulia kisa kuhusu kifo chake mwenyewe. Mawazo haya yanaungwa mkono na Wamitila (2002) anaposema kuwa, msimulizi wa nafsi ya kwanza ana mkabala mmoja pekee wa kuyaona matukio na hana uwezo wa kuyasawiri mawazo na ndoto za wahusika wake.

Usimulizi wa aina hii unadhihirika katika sehemu mbalimbali za riwaya ya *Dharau ya Ini*. Kwa mfano katika (uk.2) msimulizi anasimulia matukio ambayo anashiriki kwa kuhusisha neno ‘nikawa’ anapoeleza kuhusu jinsi kumbukumbu kuhusu sura ya marehemu babake ilivyokuwa imeanza kutoweka akilini mwake. Anasema:

Riwaya ianzapo, miaka mingi ilikuwa imepita tangu baba afe; hata sura ninayo-ikumbuka kutokana na picha ya zamani iliyochakaa, ilikuwa imeanza kunitoweka polepole... (uk.2)

Msimulizi anaeleza kuwa riwaya ianzapo miaka mingi ilikuwa imepita tangu babake afe mpaka alikuwa ameanza kuisahau sura yake. Ametumia kiambishi cha nafsi ya kwanza “ni” katika kusimulia kisa kinachomhusu yeye mwenyewe na wala sio watu wengine. Hali hii inaashiria kuwa yeye ni mhusika katika matukio anayosimulia na anatambulika kama Lila. Anaeleza kuhusu

changamoto za safari yake alipokuwa akielekea mahali alikozikwa babake.

Anasimulia kisa chake hivi:

Nikapenyeza katikati ya mimea; na moyo
ukanipapa; Kichomanguu kikaidata nguo
yangu; nyasi zikanizonga, karibu kunia-
ngusha, lakini sikutaka kukata tamaa (uk.5).

Lila anasimulia kuhusu matatizo anayokumbana nayo katika safari yake anapokwenda kutafuta alikofia babake. Licha ya changamoto anazokabiliana nazo njiani anasema hakukata tamaa. Msimulizi anatumia nafsi ya kwanza “ni” hali inayodhihirisha kuwa amechukua mtazamo wa ndani ambapo anashiriki katika matukio anayoyasimulia. Msimulizi anatambulika wazi kama mrasili wa habari katika shirika la habari la Mpapure. Anahusisha nafsi ya kwanza anapotueleza kuhusu safari yake. Anaeleza ifuatavyo:

Nilipiga hatua kadhaa kuelekea upande wa
chini, kama namwelekea mwanamke wa
jiwe: nikapita lilipokuwa lango la kuingia
kwenye uwanja wa Munene mwenyewe...
(uk.4)

Msimulizi anaendelea kusimulia kuhusu safari yake. Usimulizi huu unadhihirisha kuwa msimulizi anashiriki katika matukio anayoyasimulia kwa kutumia kiambishi vya nafsi ya kwanza “ni” na uwepo wake unatambulika wazi mbele ya msomaji anaposimulia kuhusu safari yake.

2.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Pili

Katika usimulizi wa nafsi ya pili msimulizi humrejelea na kumhusisha msomaji moja kwa moja katika usimulizi wake. Kiambishi kiwakilishi ‘u’ huweza

kutumika katika kujenga uhusiano wa karibu baina ya msimulizi, wahusika na msomaji kama anavyodokeza Raban (1968:31).

Kulingana na Fludernik (1993:s.6) mwandishi hawezi tu kujifunga kwenye usimulizi wa nafsi ya kwanza na ile ya tatu pekee kwani wakati mwingine anahitajika kubadilisha usimulizi wake hasa iwapo anakusudia kubadilisha mtazamo wa usimulizi. Msimulizi anaposimulia matukio katika ulimwengu wa kindoto anaweza kubadilisha mtazamo wa usimulizi. Anaweza kuhama kutoka usimulizi wa nafsi ya kwanza au wa tatu na kuingia katika usimulizi wa nafsi ya pili unaochukua kiambishi ‘u’.

Katika usimulizi wa nafsi ya pili msimulizi humrejelea na kumhusisha msomaji moja kwa moja katika usimulizi wake. Mbinu hii ya usimulizi hutumika kama njia ya kumfanya msomaji aweze kuuona uaminifu wa msimulizi na kuamini kile anachosema. Usimulizi wa aina hii unadhihirika wazi katika riwaya ya *Dharau ya ini*. Katika (uk.7) msimulizi anatumia jinsi mawazo yake yalivyofunguka kama pazia la jukwaa na vile macho yake yalivyofunguka alipokuwa safarini akielekea alikofia na kuzikwa babake. Aliamua kuangalia kila kilichofichuliwa na pazia hilo lakini hata yeye mwenyewe hakuweza kuelewa kilichokuwa kikionekana kwenye jukwaa lenyewe. Msimulizi anamhusisha msomaji katika usimulizi wake kwa kumweleza ifuatavyo:

Ulikuwa katika chumba kilichojaa makabati
ya kila aina. Ukabumburushwa na hatua za
msogeo wa mtu. Akatokeza mwanamume wa
ajabu, hakuwa na macho mawili, moyo
ukakututa, macho pima kwa uoga... (uk.7)

Lila anasimulia kuhusu jinsi mwanaume asiyetambulika alivyokuwa akimwandama na kila alipokabiliana naye alilenga kumwangamiza. Usimulizi huu unatokea katika ulimwengu wa ndoto. Kutokana na maelezo yaliyo hapa juu, mtafiti alitambua kuwa msimulizi amehama kutoka usimulizi wa nafsi ya kwanza na kuingia katika usimulizi wa nafsi ya pili inayochukua kiambishi “u”. Hali hii inatokea kwa sababu msimulizi anatoka katika usimulizi wa kihalisia kuingia katika matukio ya ulimwengu wa kindoto.

Usimulizi huu wa nafsi ya pili unamrejelea msomaji wa hadithi na kumshirikisha moja kwa moja katika usimulizi wa matukio. Usimulizi wa aina hii unamshirikisha msomaji katika hisia za mwanamke na changamoto anazokabiliana nazo katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume. Mfano mwingine unadhihirika wazi katika (uk.7) msimulizi anapoelezea kuhusu mwanaume aliyemjia katika ndoto kwa kuhusisha usimulizi wa nafsi ya pili.

Anaeleza kuwa:

Ghafla mlango wa chumba ukafunguka
kama umesukumwa na upepo. Moyo wako
ukakupiga kwa kasi ajabu, akatokeza
mwanaume wa ajabu. Akatoa jisu na
kulivurumiza ukutani...(uk.7)

Kupitia masimulizi ya kindoto, Lila ameweza kuonyesha jinsi mwanaume aliye na maumbile yasiyo ya kawaida anavyomwandama kwa lengo la kumwangamiza. Mwanaume huyu analenga kumwangamiza kama mwanahabari ili amkomeshe Lila ili asiweze kuufichua ukweli kuhusiana na kashfa ya ufisadi uliohusu unyakuzi wa ardhi ya umma. Kulingana na jamii husika mwanamke hapaswi kujihusisha na masuala ya kisiasa. Katika maelezo

haya msimulizi amehusisha matumizi ya kiambishi cha nafsi ya pili ‘u’, anaposimulia matukio katika ulimwengu wa ndoto. Anamshirikisha msomaji moja kwa moja katika usimulizi wake.

Kwa mujibu wa Manfred (2005), usimulizi wa nafsi ya pili hauwezi kujitegemea ila tu unapohusishwa katika usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Kama ilivyotajwa hapo awali, usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumika katika matukio yanayotendeka katika hali halisi ya maisha na usimulizi wa nafsi ya pili umeingizwa hasa wakati masimulizi ya kindoto yanapohusishwa katika usimulizi. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Dharau ya ini* ambapo msimulizi wa nafsi ya tatu anaingiza usimulizi wa nafsi ya pili katika usimulizi wake. Anaeleza:

Huwezi kukumbuka ulikokuwa; unachokumbuka kwa sasa ni kuwa palikuwa na karamu moja kubwa iliyowahusisha watu wengi; uliketi pembeni, ukifurahia... ukash-tukia umepaa angani...(uk.110)

Msimulizi alikuwa amelala mapema usiku uliotangulia baada ya shughuli nyingi. Usingizi wake ulimpaa muda mfupi baada ya usiku wa manane lakini ulikatizwa na ndoto. Msomaji anahusishwa moja kwa moja katika usimulizi wa matukio ya kindoto hali inayomfanya kujihusisha na hisia za mhusika katika hadithi. Hapa msimulizi ametumia usimulizi wa nafsi ya pili kana kwamba anarejelea au kuizungumzia hadhira iliyo hai katika matini kama anavyosema Kesero (1997).

Msimulizi amehusisha kiambishi cha nafsi ya pili ‘u’ katika maneno, ‘unachokumbuka’, ‘uliketi’ na ‘ukapaa’ pamoja na vitenzi. Hii ni ishara

kwamba msimulizi anamshirikisha msikilizaji katika hali inayompata katika ulimwengu wa ndoto. Mfano mwingine wa usimulizi wa nafsi ya pili unajitokeza wazi katika (uk.145) msimulizi anapokuwa akimshirikisha msikilizaji katika mtazamo wake kuhusiana na usomaji wa riwaya anayoisimulia mwenyewe. Anamweleza kuwa:

Riwaya imefikia pale ambapo nilikuwa karibu kukata tamaa. Umewahi kufanya jambo mara kadhaa kama kuuparaga mti, kufuatia matunda yanayokualika, na kila unapoyakaribia, unakwenda chini mchangani tifu! (uk.145)

Msimulizi anasimulia kisa hiki kuashiria jinsi alivyosafiri mara tatu kumtafuta kijana Yungi lakini hakumpata. Yungi alikuwa amefukuzwa kutoka chuo cha 'The Kenya School of Law.' Msimulizi anatumia maneno 'nilikuwa karibu kukata tamaa' kuashiria kuwa mwishowe alifaulu kumpata kijana huyo. Kwa hivyo usimulizi huu unamhusu msimulizi na matendo yake binafsi hasa ya anapomsaka Yungi na wala si ya wahusika wengine. Msimulizi anamhusisha msomaji katika hisia zake alipokosa kumpata Yungi kwa mara kadha. Anatumia usimulizi wa nafsi ya pili kuonyesha hisia zake. Sehemu inayofuata ilichanganua kigezo cha usimulizi wa nafsi ya tatu na kuonyesha matumizi yake katika riwaya teule.

2.2.2 Usimulizi Nafsi ya Tatu

Usimulizi wa nafsi ya tatu kama anavyodokeza Stanzel (1984) hutambulishwa kwa kiambishi cha mofu 'a'. Usimulizi huu huonyesha kuwa msimulizi amejitenga na matukio anayosimulia katika hadithi. Huu ndio usimulizi

uliozoeleka sana katika maandishi ya fasihi. Msimulizi husimulia kuhusu mtu mwingine wala si yeye mwenyewe.

Wamitila (2002:40) anakubaliana na maoni ya Stanzel (1984) kwamba msimulizi wa nafsi ya tatu anapoyasimulia matukio huwa anaonyesha ujuzi wa kila jambo na anafahamu kila kitu kinachowahusu wahusika. Msimulizi huyu ana uwezo wa kuingia katika akili ya mhusika fulani na kumfichulia msomaji mawazo yanayompitia mhusika huyo.

Ingawa hivyo, Wamitila (2002:42) anaeleza kuwa wazo hili kimantiki linazua ukweli kinzani kwa kuwa mwandishi ambaye anaweza kusimulia hadithi kama (msimulizi-mwandishi) ndiye anayeibuni na lazima anajua kila kitu kuwahusu wahusika wake. Usimulizi wa aina hii unapatikana katika sura ya pili ambapo msimulizi anasimulia kuhusu kisa kuhusu Munene. Anaeleza kuwa:

Alijulikana sana ingawa watu wengi hawa-
kumjua kwa jina la ubatizo, Ken, Jina
alilopata zamani alipokuwa akifanyakazi
katika shirika la reli la 'African Railways'
kabla kuamua kustaafu na kujitosa katika
biashara (uk.10)

Msimulizi anaonyesha kuwa ana ufahamu kuhusu maisha ya hapo awali ya Munene. Anaeleza jinsi alivyojulikana sana na kutoa habari kuhusu kazi aliyokuwa akifanya hapo awali kabla ya kujihusisha na biashara. Maelezo haya yanadhihirisha wazi kuwa msimulizi huyu wa nafsi ya tatu ana ufahamu mzuri kuhusu maisha na historia ya mhusika wake. Msimulizi anatumia viambishi vya nafsi ya tatu 'a' katika kumrejelea mhusika mkuu katika hadithi

anayosimulia. Msimulizi pia anasimulia kuhusu maisha ya awali ya Munene na uhusiano wake na babake, mzee Kivu. Anasema ifuatavyo kumhusu Kivu:

Alimwoa mke wa pili ambaye aliishi kumzalia watoto sita. Kati ya watoto hao, Kivu alikuwa wa kuchanjiana damu na Munene; wakafungwa pamoja kwa fundo la hisia ambalo lisingeweza kuyeyushwa ...(uk.10)

Kivu alioa mke wa pili aliyemzalia watoto wengine sita. Ndoa hiyo ilitokea baada ya kifo cha mamake Munene. Msimulizi anasema kuwa kati ya watoto hao wote Munene ndiye aliyekuwa na uhusiano wa karibu sana na babake. Matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya tatu 'a' yanadhihirika katika maneno 'alimwoa' na 'alikuwa' kuonyesha kuwa msimulizi wa nafsi ya tatu anafahamu kuhusu historia na uhusiano kati ya Kivu na Munene. Masimulizi haya yanadhihirisha wazi kuwa msimulizi wa nafsi ya tatu ana uwezo wa kuyaona yote kinyume na msimulizi wa nafsi ya kwanza na ile ya pili. Msimulizi wa nafsi ya tatu anaendelea kusimulia kuhusu ndoa ya Munene ya hapo awali na jinsi alivyompenda mkewe wa kwanza, Kasina. Anaeleza yafuatayo kuhusu uhusiano wao wa awali kabla ya ndoa yao kuvunjika. Anasema:

Walipendana sana watu hawa. Munene alikuwa amekwea ngazi za ufanisi alipomwoa Kasina, msichana mrembo mwenye mwanya wa neno, hakuvutiwa na Munene kwa sababu ya mali yake...(uk.35)

Msimulizi anasimulia kuhusu uhusiano kati ya Munene na mkewe Kasina na jinsi walivyopendana punde tu baada ya kuoana. Anaonyesha vile Kasina alivyokuwa mrembo akiwa mchanga na vile alivyompenda mumewe kwa dhiti kwa kutumia nafsi ya tatu. Masimulizi haya yanaonyesha wazi kuwa msimulizi

wa nafsi ya tatu ana uwezo wa kuyaona yote na anafahamu matendo na hisia za wahusika wake katika mazingira wanamoishi kama anavyoeleza Stanzel (1984). Msimulizi huya huwafuata wahusika wake unyounyo katika kila wanalolitenda ili kuyasimulia matukio hayo bila kuonekana mbele ya msomaji kama ilivyotajwa hapo awali.

Usimulizi wa nafsi ya tatu unaweza kuingiliana na wa nafsi ya pili hasa pale ambapo msimulizi anapokusudia kumshirikisha msomaji wake katika hisia zake. Msimulizi ana uwezo wa kuvuka kutoka usimulizi wa nafsi ya tatu na kuingia katika ule wa pili kama anavyodokeza Fludernik (1996). Isitoshe usimulizi wa nafsi ya tatu huweza kuingiliana na ule wa nafsi ya kwanza kupitia kwa viambishi ‘ni’ jinsi inavyoshuhudiwa msimulizi akieleza kuhusu maisha ya Munene kuwa:

Aliamini kuwa alikuwa na kitu cha kumtuliza
mkewe na kumwonyesha ukweli wa aliyoyas
ema asubuhi. Haya yote nayafanya kwa ajili
ya kesho yetu na watoto ninaowapenda...
(uk.67).

Usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika kuonyesha mawazo yanayompitia Munene hasa baada ya kugombana na mkewe Deborah asubuhi hiyo. Deborah alimtaka Munene afuatilie suala la shule ya mwanawe John lakini Munene hakutaka kukosa kuhudhuria mkutano wa kibiashara uliohusisha waziri Kingo na Wazungu watatu.

Msimulizi ameubadilisha usimulizi wake kutoka nafsi ya tatu hadi nafsi ya kwanza kwa kutumia kiambishi ‘ni’ na ‘na’. Matumizi ya kiambishi ‘ni’

yanadhihirika katika neno ‘ninaowapenda’. Nafsi hiyo ya kwanza imetumika kutoa madai kuwa yote aliyoyafanya Munene yalikuwa kwa manufaa ya familia yake. Mukstadha huu unadhihirisha hali ya mwingiliano baina nafsi zote mbili, yaani ya tatu na ile ya kwanza katika mukstadha mmoja.

Usimulizi nafsi ya pili unaweza kuhusishwa na usimulizi wa nafsi ya kwanza au ukaweza kuingiliana na wa nafsi ya tatu msimulizi anaposimulia matukio katika miktadha mbalimbali kama anavyodai Fludernik (1996). Mbali na kushughulikia aina za usimulizi, sehemu hii ilianguzia mahusiano ya wakati wa usimulizi unaohusisha vigezo kama vile; usimulizi baadaye; usimulizi kabla; usimulizi sawia na usimulizi zongomezi.

2.3 Mahusiano ya Wakati wa Usimulizi

Matukio yanayosimuliwa katika matini yotote ile huweza kudhihirishwa au kuwasilishwa kwa jinsi mbalimbali. Arege (2012) akimnukuu Gennette (1980) anadokeza kuwa hadithi inaweza kutambulishwa katika wakati fulani kuhusiana na kitendo cha usimuliaji. Anasema kuwa hali hii husababisha kuwepo kwa aina tatu za usimuliaji wa matukio ambazo ni; wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao.

Wakati wa usimulizi ni kigezo muhimu katika usimulizi kwani ni vigumu kuwepo na simulizi pasipo na kutambulisha umbali kati ya hadithi na msimulizi. Matukio katika hadithi yanaweza kusimuliwa baada ya kutokea, kabla ya kutokea kwao ama yakasimuliwa wakati uo huo yanapotokea kama inavyojadiliwa hapa chini.

2.3.1 Usimulizi Baadaye

Usimulizi baadaye kulingana na Gennette (1980) ni matukio yanayosimuliwa baada ya kutokea kwake. Kiambishi “li” hutumika katika kudhihirisha kuwa matukio yalitendeka wakati uliopita usiokuwa dhahiri na kisha yakasimuliwa. Katika riwaya ya *Dharau ya Ini* mwandishi amemteua msimulizi anayedhihirisha kuwa matukio yanayosimuliwa yalitangulia kutendeka kabla kusimuliwa. Lila anapomtembelea babu yake katika (uk.24) anasimulia ifuatavyo kumhusu babu yake:

Alipotokeza alikuwa amebeba mkungu wa ndizi zilizokuwa zimeiva. Aliutua mkungu wake juu ya kichaga kidogo kilichokuwa mbele ya alipokuwa ameketi kabla. Alinia-ngalia na kukenua meno ... (uk.19)

Lila anasimulia kisa kuhusu vile alivyokuwa amekwenda kumtembelea babu yake katika harakati za kutafuta alikofia na kuzikwa babake. Alipofika alimsubiri babu yake ambaye alichukua muda mrefu kabla ya kufika. Matukio haya yamesimuliwa baada ya kutokea kwake. Kiambishi cha wakati uliopita ‘li’ kimetumika kudhihirisha matukio haya yalitokea wakati uliopita. Mfano mwingine unaodhihirisha kuwa matukio yanasimuliwa baada ya kutendeka kwake yanapatikana katika (uk.91). Msimulizi anaeleza ifuatavyo kuhusu matendo ya Munene:

Munene alimtuliza mkwe wake macho, akasogea na kumshtukiza Kingo kwa mpigo mkubwa begani. Mpigo huo ulifuatwa na shuti kali lililompata kwenye kitokono na kumtuma huko chini...(uk.91)

Msimulizi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu katika kusimulia matukio ambayo yamekwisha tendeka. Maelezo haya yanazuka baada ya Munene ambaye ni mwajiri wa King’o kutambua kuwa King’o alikuwa ameachilia mifugo wakaingia shambani kula mahindi. Kitendo hiki kinamfanya Munene kumpiga King’o teke hadi akaanguka. Haya yanadhihirisha kuwa Munene kama mwajiri hakuwa na utu wala uhusiano mwema na wafanyikazi wake.

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa kuna wakati baina ya matukio mawili yanayogawa muda wa usimulizi kutoka kwa muda wa hadithi. Umbali kati ya matukio ya hadithi na usimulizi yanategemea aina ya usimulizi au matini inayohusika kama asemavyo Kenan (1983). Mbali na kigezo cha usimulizi baadaye utafiti ulichanganua usimulizi kabla kama kigezo kingine cha mahusiano ya wakati katika usimulizi.

2.3.2 Usimulizi Kabla

Kulingana na Manfred (2005) usimulizi kabla hurejelea usimuliaji wa matukio kabla ya kutendeka kwake na aghalabu huweza kuchukua sifa za ubashiri au ndoto. Usimulizi wa aina hii haujaoelewa sana na hutumika zaidi katika bibilia. Usimulizi huu huweza kuhusisha kiambishi cha wakati ujao ‘ta’ au ‘ki.’ Riwaya ya *Dharau ya Ini* imehusisha namna ya usimulizi unaotokea kabla ya matukio kutendeka katika sehemu mbalimbali. Viambishi kati ‘ta’ na ‘ki’ vimetumika katika kudhihirisha kuwa matukio yanayosimuliwa hayajatokea. Kwa mfano:

Jamaa zake walikuwa wamefurahi alipoolewa
na mtoto wa Kivu kwa matumaini ya kuwa

atawasaidia shida zitakapopiga kambi kwao...
(uk.76)

Kauli hii inamhusu Deborah, mkewe Munene. Msimulizi anaeleza kuwa Deborah alipoolewa, jamaa zake walikuwa na matumaini makubwa ya kupata msaada kutoka kwake katika maisha ya baadaye. Waliambulia patupu kwani Deborah alikuwa anayajali masilahi yake mwenyewe na familia yake binafsi. Kiambishi ‘ta’ katika neno, ‘atawasaidia’ na ‘zitakapopiga’ ilitumika kuashiria kuwa matukio hayo yalitarajiwa kutokea siku za baadaye. Mfano mwingine unajitokeza katika (uk. 52) Kasina, mkewe Munene alipokuwa akijiambia:

Mumewe atamrudia baada ya kuhangaika
huku na huku; atatapatapa huku na kule kama
kongoni aliyepotelewa na wenzake lakini
hatimaye atamjia, tena mbio baada ya
kuwaona duma (uk 52)

Mawazo haya ya Katumbi yanasababishwa na hali kwamba alikuwa ametalikiwa na mumewe kwa kukosa kumzalia mumewe mtoto wa kiume ambaye angemrithi. Mumewe aliamua kuoza mke mwingine ambaye angemzalia mtoto wa kiume. Kasina alikuwa na matumaini kuwa mumewe angemrudia tena. Hali hiyo ilimwathiri sana na kumwingiza katika lindi la mawazo.

Kutokana na maelezo haya msimulizi ametumia kiambishi cha hali ya wakati ujao ‘ta’ kuonyesha matukio yanayosimuliwa hayakuwa yametendeka. Kulingana na simulizi matarajio ya Kasina hayakutimia kwani mumewe hakuwahi rudi nyumbani.

2.3.3 Usimulizi Sawia

Usimulizi sawia ni aina ya usimulizi ambapo matukio yanasimuliwa wakati uo huo wa kutokea kwake. Kama asemavyo Wamitila (2002) usimulizi wa aina hii hupatikana katika sanaa za kiutendaji kama drama au filamu. Sifa hizi zinaonekana katika sehemu mbalimbali za riwaya husika. Usimulizi huu unajitokeza msimulizi anaposimulia kisa kuhusu Munene. Anaeleza kuwa:

Kijana mmoja mfanyikazi wa pale nyumbani
amemwona Munene na kuamua kurudi
kinyumenyume na kupotelea nyuma ya banda
la mabua ya mahindi...(uk.15)

Msimulizi anaonyesha vile mfanyikazi wa Munene anavyohepa baada ya kumwona mwajiri wake akija alipokuwa. Kuhepa huku ni ishara kuwa uhusiano baina yake na Munene haukuwa mzuri. Alimuogopa kutokana na ukatili wake na kila alipomwona alipatwa na hofu isiwe angepatikana na kosa lolote ambalo lingemfanya apewe adhabu.

Msimulizi amehusisha kiambishi; 'na' cha wakati uliopo pamoja na kiambishi, 'me' kinachodhihirisha hali timilifu kuashiria kuwa matukio yalikuwa yakisimuliwa wakati uo huo yalipotendeka. Matumizi ya viwakilishi hivyo vya wakati yanachangia katika kuufupisha umbali wa wakati kati ya matukio yanayosimuliwa na msomaji.

Usimulizi sambamba pia umedhihirika wakati msimulizi anaposimulia kuhusu Munene hasa anapoonekana ameketi kwenye baraza la jumba lake akiyatuliza mawazo yake na kuyaburudisha macho yake kwenye mandhari iliyo mbele ya nyumba yake. Msimulizi anaeleza kuwa:

Munene anakiinua kikombe cha chai kwa nia ya kupiga fundu, analizungusha hilo tama la chai kinywani kama anaitathmini ladha yake, midomo inachezacheza, kikombe bado ana-cho... (uk.13)

Munene anakunywa chai huku akiyatuliza mawazo yake na kuyatazama mandhari yaliyokuwa mbele ya nyumba yake. Anaitathmini ladha ya chai huku midomo ikimchezacheza. Hali hii inamrejelea Munene hasa katika maisha yake ya baadaye anapoanza kukonga na kuishiwa na nguvu kutokana na umri wake mkubwa. Msimulizi anamwingiza msomaji katika kuyashuhudia maisha ya mhusika wake katika siku za baadaye atakapoanza kukonga ili apate taswira kuhusu jinsi mambo yatakavyokuwa katika siku zake za usoni.

Msimulizi amehusisha matumizi ya kiambishi cha wakati wa sasa “na” kuonyesha kuwa kitendo kimesimuliwa wakati uo huo kinapotendeka. Pia kiambishi “ki” kimetumika katika neno, “akiangalia” kuashiria kuwa matukio yanasimuliwa huku yakiendelea kutendeka.

2.3.4 Usimulizi Zongomezi

Huu ni wakati ambapo muda wa usimulizi na muda wa utendaji wa matukio huandamana na kubadilishana nafasi katika hadithi kama asemavyo Gennette (1988). Anautaja usimulizi zongomezi kama usimulizi ulio changamano zaidi kwani huhusisha matumizi ya hali na nyakati mbalimbali za usimulizi hivyo kuifanya hadithi na usimulizi wenyewe kuingiliana. Usimulizi wa aina hii huhusisha mchanganyiko wa usimulizi kabla, usimulizi sambamba na usimulizi baadaye katika muktadha fulani. Mfano huu unadhihirika katika (uk.48) msimulizi anapoeleza kwamba:

Deborah anahisi kuwa maisha yanamwendea vizuri na wanavyosema watu kijijini, ‘amefika alikokuwa akienda’. Alishafanikiwa kumdhibiti mumewe na kijijini watasema kuwa hapo ndiye anayesema chakula kipakuliwe...(uk.48)

Maelezo haya yanamrejelea Deborah ambaye ni mke wa tatu wa Munene aliyeolewa baada ya Munene kuwataliki wakeze wawili, Kasina na Katumbi. Deborah na mumewe Munene wanaishi maisha ya kifahari. Mumewe alimridhia kwa chochote alichohitaji hasa kutokana na sababu kuwa aliweza kumzalua mtoto wa kiume ambaye angemrithi kinyume na wake zake waliotangulia.

Msimulizi amehusisha vigezo vyote vitatu vya wakati ambavyo vinachukua kiambishi; ‘li’, ‘na,’ ‘ta’ kinachoashiria usimulizi kabla katika usimulizi huu. Hali hizi tatu za wakati wa usimulizi zinabadilisha nafasi moja baada ya nyingine katika kukuza ujumbe. Msimulizi amehusisha usimulizi ambao ni changamano kwa lengo la kuwajenga wahusika wake katika uendelezaji wa matukio. Sehemu ifuatayo hapa chini imeshughulikia viwango vya usimulizi na kuonyesha matumizi yake katika hadithi.

2.4 Viwango vya Usimulizi

Usimulizi unaweza kutokea kwa viwango mbalimbali kama anavyodokeza Kenan (1983:91-94). Kuna ‘simulizi ndani ya simulizi.’ na hali hii hutokea wakati msimulizi anaposimulia hadithi inayomhusu na kisha akaibuni hadithi nyingine ndani ya hadithi hiyo kuu. Msimulizi anaposimulia hadithi ndani ya

hadithi huweza kubuni ulimwengu mpya na wahusika wengine wapya ambao pia huweza kushiriki katika kusimulia hadithi zao.


Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa kunaweza kuwa na hadithi asili na ndani yake kukaegemezwa hadithi nyingine ambayo huwa ni hadithi kuu. Vilevile kunaweza kuwa na hadithi zingine zinazoegemezwa kwenye hadithi hiyo kuu. Bal (1981:43) anakubaliana na mawazo haya kwamba kunaweza kuwa na viwango vya hadithi katika simulizi na anaeleza kuwa viwango hivi vinaenda sambamba na viwango vya usimulizi. Hii ina maana kuwa katika simulizi, msimulizi anaweza kusimulia hadithi na katika hadithi hiyo kukawa na mhusika mwingine anayesimulia hadithi nyingine ndani ya hadithi hiyo kuu.

Msimulizi pia huwapa nafasi wahusika wake kusimulia hadithi nyingine iliyo tofauti na hadithi kuu. Hivyo usimulizi wa hadithi mbalimbali unaweza kuchukua mtazamo tofauti kutegemea umbali wa msimulizi na hadithi anayosimulia. Hadithi tegemezi hubuniwa katika ulimwengu mpya na wahusika wapya kinyume na wahusika katika hadithi kuu.


Hadithi hizi huwa zinajenga viwango vya hadithi kidaraja, kila kijihadithi hutegemea hadithi ambamo kimeegemezwa. Kwa hivyo katika usimulizi kuna msimulizi wa hadithi ya kimsingi ambaye ni wa kiwango cha daraja ya kwanza na msimulizi wa daraja ya pili anayesimulia hadithi ambayo imeshenezewa katika hadithi kuu. Isitoshe kunaweza kuwa na msimulizi wa daraja ya tatu na hata zaidi kutegemea na muundo wa simulizi kama anavyoeleza Kenan (1983: 91).

Gennette (1988:85) ametoa mchoro unaohusisha muundo wa kimsingi wa hadithi zinazoshehenezwa kwenye simulizi kuu kama ifuatavyo:

Mchoro 2.1



Mchoro 2.2



Katika mchoro (2.1) hadithi A ndiyo kuu na B ni sehemu ya hadithi A. Kwa hivyo msimulizi wa hadithi A ni wa daraja ya kwanza na B ni wa daraja ya pili. Katika mchoro wa pili (2.2) hadithi A ndiyo hadithi kuu, B1 na B2 ni hadithi katika daraja ya pili na C ni hadithi katika daraja ya tatu.

Katika riwaya ya *Dharau ya Ini* kuna viwango mbalimbali vya hadithi vinavyoenda sambamba na viwango vya usimulizi. Riwaya inapoanza msimulizi anasimulia hadithi ya kimsingi ambayo ni ya kiwango cha daraja ya kwanza. Kisha baada ya hadithi hiyo kuna hadithi ya daraja ya pili inayoshehenezwa kwenye hadithi hiyo ya kimsingi. Hadithi hiyo ya pili ndiyo hadithi kuu. Hadithi hizi mbili zina uhusiano na zinabadilishana nafasi moja baada ya nyingine zinaposimuliwa.

Isitoshe ndani ya hadithi hizi kuna vijihadithi vingine vidogovidogo ambavyo vimeegemezwa ndani ya hadithi kuu. Hadithi ya kimsingi ndiyo inayotangulia na inasimuliwa na msimulizi wa daraja la kwanza ambaye anajulikana kama Lila ambaye ni mwandishi wa habari katika Shirika la Habari la Mpapure. Hadithi hii inasimuliwa katika nafsi ya kwanza umoja.

Lila anasimulia kuhusu safari yake ya kwenda kutafuta alikofia na kuzikwa babake na kueleza mambo aliyokabiliana nayo katika safari hiyo. Pia anasimulia kuhusu changamoto zinazomkabili kama mwandishi wa habari wa kike. Haya yanatokea baada ya Lila kutoa taarifa kuhusu kashifa ya ufidadi inayowahusisha viongozi wa kiume wa ngazi za juu serikalini. Alitekwa nyara na watu wasiojulikana na kupelekwa hadi katikati ya msitu akiwa amefungwa macho kwa kitambara. Katika harakati za kutafuta njia ya kurudi alikotoka, anakumbuka hadithi aliyosimuliwa na mwanafunzi mwenzake katika chuo kikuu alichosomea hapo awali.

Hadithi hiyo ilihusu '*Mlima wa Adamu*'. Lila anasimulia hadithi hii kwa nafsi ya tatu. Hadithi hiyo inahusu fisi mkubwa ajabu aliyeishi mlimani kwenye pango. Karibu na mlima huo paliishi wakulima wanyonge pamoja na jamaa zao. Watu hao walimwogopa fisi huyo sana na kwa hivyo walimtembelea mara kwa mara wakimpelekea zawadi nyingi.

Siku moja pakatokea mtu aliyeshangazwa na kitendo hicho cha kumpa fisi zawadi. Aliamua kwenda mlimani na kwa bahati mbaya fisi wakamkamata na kumtia ghalani walimoweka chakula ili wamle hatimaye. Kutoka siku hiyo hakuonekana tena. Wanakijiji walimsihi fisi amwachilie na baada ya muda akatokeza, jambo lililowashangaza sana. Hawakuwahi kumwona fisi huyo tena. Tangu siku hiyo mlima huo ukawa mlima wa Adamu kama jina la hadithi yenyewe.

Kijihadithi hiki kina uhusiano na maisha ya msimulizi wa hadithi ya kimsingi kwani kinaashiria mambo anayokumbana nayo kama mwanahabari wa kike

katika shirika la habari la Mpapure. Hali hii inalenga kuwafanya wasomaji wake kupata ufahamu zaidi kuhusu kisa anachosimulia katika hadithi hiyo ya kimsingi.

Riwaya teule pia imehusisha hadithi katika daraja ya pili inayoshehenezwa kwenye hadithi ya kimsingi. Hii ndiyo hadithi kuu inayoifuata ile ya kimsingi. Hadithi hiyo inahusu historia na maisha ya Munene. Hadithi hii inasimuliwa na msimulizi asiyetambulika kwa kutumia nafsi ya tatu. Msimulizi anasimulia kuhusu malezi mabaya ya Munene alipokuwa mdogo. Alidekezwa sana na babake mzazi, hali iliyoyaathiri maisha yake ya baadaye hasa akiwa shuleni, chuoni na hatimaye akiwa mtu mzima.

Msimulizi anasimulia kuhusu ndoa baina ya Munene na wakeze watatu. Munene alikuwa amementaliki mke wake wa kwanza na wa pili kwa kukosa kumzalia mwana wa kiume. Maisha yake akiwa mwanasiasa yamedhihirisha kuwa alikuwa fisadi na laghai aliyejaa kiburi. Msimulizi pia ameonyesha maisha ya Munene ya uzeeni hadi kufa kwake. Hadithi ya kimsingi kuhusu Lila inabadilishana nafasi na hadithi kuu inayohusu Munene.

Isitoshe kuna kijihadithi kingine kilichosimuliwa katika daraja ya tatu. Kijihadithi hiki kimesimuliwa na mmoja wa wahusika katika hadithi kuu kwa kutumia nafsi ya tatu na inapatikana katika (uk.131). Msimulizi anasimulia kisa kuhusu '*Fisi na asali*'. Fisi huyu kwa tamaa nyingi kala asali nyingi; akaiona tamu sana na kuamua kuwa lazima atafute njia za kuizuilia asali hiyo isitoke mwilini. Kwa hivyo akawekewa kizibo na mwenzake. Hakuweza kuhimili hali hiyo kwani tumbo lilivimba ikabidi kizibo hicho kizibuliwe na rafikiye,

sungura. Basi msimulizi anaeleza kuwa kilichotapakaa si asali bali ni kinyaa cha kukera pua.

Msimulizi wa hadithi ni mwanasiasa aliyefukuzwa kutoka chama tawala. Kisa chake kinarejelea jinsi tamaa na ufisadi ulivyokithiri miongoni mwa viongozi wa chama cha serikali. Viongozi hao wa serikali walitetea madai hayo vikali na wakawa wanasimulia kijihadithi kingine vilevile kwa kuhusisha nafsi ya tatu ili kupinga shinikizo hilo.

Kijihadithi walichosimulia kinahusu '*Sungura aliyekosa zabibu*'. Katika kisa hicho sungura alikosa kufikia zabibu juu ya mti na kutoa kisingizio kuwa zilikuwa chungu. Hali hii inamlenga mwanasiasa huyo aliyeanza kuwakashifu viongozi hao wa chama punde tu baada ya kutimuliwa kutoka chama hicho. Wakati alipokuwa mshiriki wa chama alikuwa akiunga mkono ufisadi huo. Kijihadithi hiki pia ni cha daraja ya tatu kama kile cha '*Fisi na asali*' kwa kuwa kimeshehenezwa kwenye hadithi kuu na kimesimuliwa na mhusika wala si msimulizi mwenyewe.

Kuna kijihadithi kingine pia kinachosimuliwa na msimulizi wa kiwango cha daraja ya tatu na kimeegemezwa katika hadithi ya kimsingi. Msimulizi wa hadithi ya kimsingi ndiye anayekisimulia kama njia moja ya kuikamilisha simulizi katika riwaya yake. Kijihadithi hiki kinahusu '*Nyarubanja na wanakijiji cha Kinaa*.' Hiki kimesimuliwa kwa nafsi ya tatu ambapo kiwakilishi 'a' kimetumika. Nyarubanja alikuwa mgeni wa wanakijiji wa Kinaa na alikuwa ametokea upande wa pwani kwenye bahari ya Hindi. Aliwabebea

zawadi za kila aina, hali hii iliwafanya kumkaribisha na hata kumpa nyumba nzuri.

Siku moja Nyarubanja aliwaomba wazee wa kijiji hicho ruhusa ya kuandamana na vijana wenye nguvu ili wapeleke pembe za ndovu na vipusa vya vifaru sokoni. Alipewa ruhusa na wakaelekea upande wa Bahari ya Hindi na baadaye Nyarubanja akarudi kuchukua vijana wengine na pembe zaidi. Lakini walipoenda hawakuonekana wala kurudi tena.

Kisha siku moja kukatokeza mwanamme wa ajabu aliyekuwa mrefu kama Nyarubanja na aliyewaleta zawadi kama za Nyarubanja. Wazee walimkaribisha na wengine walimkataa. Alipewa ardhi na akajenga kibanda chake na kupewa jina 'Mzungu' kwa vile alifanana na Nyarubanja. Lakini cha ajabu ni kuwa kibanda chake kiliendelea kupanuka kila kukicha hadi kikameza kijiji kizima.

Mzungu alichukua ardhi iliyokuwa bora na kuwalazimisha wanakijiji wamtumikie. Baada ya mashauriano ya muda mrefu wenyeji wakaamua kujiandaa ili waipigane ardhi yao. Silaha za pekee walizokuwa nazo ni mishale, panga na mikuki ilhali mzungu alikuwa na bakora ya ajabu iliyokuwa ikitoa moto.

Ingawa hivyo wenyeji hawakukata tamaa, waliendelea kupigana na mzungu ingawa kuna wenyeji wachache waliowasaliti Wafrika wenzao. Mzungu alipoona atashindwa akarudi kwao. Baada ya Mzungu kuondoka wenyeji wakamchagua Abumama awe kiongozi na watu wakawa na matumaini ya

maisha mazuri. Matumaini yao yalibaki kuwa ndoto kwani waliofaidika ni wale waliokuwa na uhusiano wa karibu, waliotoka katika kabila moja na Abumama na walioweza kuzungumza kizungu. Chakaramu alipowaonya wenyeji kwamba maisha si kitu cha kuchezeza walimwona kama mzushi anayependa kulalamika.

Kulingana na hadithi ya Nyarubanja Wamitila anaeleza kimafulano jinsi wazungu walivyoingia Afrika. Waafrika waliwakaribisha kwa moyo safi hali iliyowafanya wazungu kunyakua mashamba yao na kuanza kuwatumikisha. Mwandishi anatupitisha katika vipindi mbalimbali kuanzia pale Nyarubanja anapofika mara ya kwanza kijijini (Afrika) na jinsi alivyorudi kwao akiwa amebeba vijana wengi na pembe. Vijana hao hawakurudi tena.

Nyarubanja aliporudi kwao, wanakijiji walitembelewa na mgeni mwingine aliyefanana na yeye. Mgeni huyu vilevile alianza kuwatumikisha. Anasimulia kuwa kuna wazungu waliotangulia na wengine wakaja baadaye. Tatizo kuu ni kwamba kuna waafrika waliomuunga mzungu mkono na waliompinga. Waliompinga walizinduka na kupigana na mkoloni hadi wakamtimua. Hivyo kijihadithi hiki kinadhihirisha athari za ukoloni na ukoloni mambo leo katika nchi za Afrika.

Msimulizi anasimulia kijihadithi hiki kama njia ya kuwahusisha na kuwahamasisha wasomaji kuhusu umuhimu wa kupokezana hadithi hii kwa kizazi kijacho kwani ngano huwa na mafunzo kuhusu maisha. Kijihadithi hiki kina uhusiano na hadithi ya kimsingi kwani inahusu viongozi fisadi na laghai wanaosaliti juhudi za kupigania haki ili kujenga jamii bora. Uchunguzi huu

umedhihirisha wazi kuwa kupitia viwango mbalimbali vya hadithi, mtazamo wa usimulizi huweza hubadilika. Hali kama hii hutoa ule uzoefu wa kuwepo kwa msimulizi mmoja katika matini na kuifanya simulizi kuwa na mvuto kwa msomaji. Mitazamo tofauti ya usimulizi huweza kurutubisha muundo wa simulizi na kumfanya msomaji kuelewa ujumbe uliokusudiwa.

2.5 Nafasi ya Msimulizi katika Usimulizi wa Hadithi

Kwa mujibu wa Levesque na Gullimette (2006) msimulizi aghalabu huhusishwa katika kitendo cha usimulizi wa hadithi kwani kimsingi huu ndio wajibu wake. Wanasisitiza ya kwamba msimulizi huchukua nafasi muhimu katika mawasiliano kati ya simulizi, usimulizi na msomaji. Mbali na usimuliaji wa hadithi msimulizi huwasilisha ujumbe kwa msomaji na kumgawia maarifa aliyonayo kuhusu matukio.

Majukumu ya msimulizi kama anavyodokeza Kenan (1983) ni usimuliaji wa hadithi, uelekezaji wa msomaji, uendelezaji wa mawasiliano, uwasilishaji wa itikadi za mwandishi pamoja na kutoa maoni kuhusu usimulizi wake. Katika riwaya ya *Dharau ya Ini* msimulizi amedhihirika akitekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatayo;

2.5.1 Jukumu la Usimuliaji wa hadithi

Kwa mujibu wa Gennette (1988) jukumu la usimuliaji wa hadithi ndilo la kimsingi katika kazi ya fasihi na pasipo msimulizi hamna usimulizi. Yeye hutumika kama chombo cha kuratibu na kuwasilisha hadithi. Jukumu lake kimsingi ni kuteua matukio atakayohusisha katika hadithi na kuratibu jinsi matukio hayo yatakavyowasilishwa moja baada ya lingine.

Katika simulizi kuna wasimulizi mbalimbali wanaosimulia hadithi. Vilevile kuna mhusika mmoja mkuu ambaye hushiriki katika usimuliaji na huweza kuwapa wahusika wengine fursa ya kusimulia hadithi kabla ya kuirejesha nafasi hiyo kwa msimulizi mkuu. Katika riwaya teule kuna msimulizi wa ndani ambaye anasimulia hadithi huku akishiriki katika matukio anayosimulia na msimulizi anayesimulia hadithi akiwa nje ya matukio hayo. Msimulizi ndani ametambulishwa kuwa Lila ambaye ni mwandishi wa habari. Anasimulia kisa kuhusu maisha yake mwenyewe kama mrasili wa habari katika shirika la habari la Mpapure. Hadithi inapoanza anasimulia jinsi alivyofunga safari ya kwenda kutafuta alikofilia na kuzikwa babake pamoja na matatizo aliyokabiliana nayo safarini.

Lila anasimulia kisa kuhusu maisha yake kama mwanahabari na jinsi alivyokabiliwa na changamoto nyingi kama mwanahabari wa kike. Anaeleza jinsi alivyotolewa chumbani na watu wasiojulikana na kufungwa kitambara usoni kabla ya kuingizwa kwenye gari geni kwake. Anaeleza kuwa:

Gari liliendeshwa kwa kipindi kirefu hadi liliposimamishwa ghafla. Kisha Nikaamrisha! “Mjinga toka nje.” niliachwa katikati ya msitu peke yangu...(uk.209)

Hadithi hii inahusu maisha ya msimulizi mwenyewe. Anaeleza jinsi alivyotekwa nyara na kupelekwa hadi katikati ya msitu na watu wasiojulikana. Gari lililombeba lilikuwa linaendeshwa mbio na baada ya kipindi kirefu likasimamishwa ghafla na akaamrisha ashuke. Alijipata katikati ya msitu peke yake.

Lila alitekwa nyara muda mfupi tu baada ya kuchapisha magazetini kisa cha ufisadi kilichowahusisha viongozi wa ngazi za juu serikalini. Mvutano uliokuwepo ulidhihirisha wazi kuwa wanawake hawakupaswa kujihusisha na masuala ya kisiasa katika jamii husika. Kazi kama hiyo iliaminika kuwa ya wanaume pekee.

Msimulizi huweza kuhusisha mbinu mbalimbali za usimulizi katika kuwasilisha matukio mbalimbali katika hadithi. Msimulizi wa nafsi ya tatu anaanza kwa kusimulia kuhusu kisa cha Munene tangu utotoni, jinsi alivyolelewa, ujana wake hadi kuajiriwa kwake katika shirika la Railways. Baadaye anatueleza kuhusu mhusika huyo akiwa mfanyibiashara mkubwa na hatimaye alipojitoma katika ulingo wa kisiasa kijijini Kitambasye. Anasimulia kuhusu maisha yake ya ndoa na wake zake watatu; Deborah, Kasina na Katumbi na uhusiano wao hadi anapokonga na kuaga dunia.

Vilevile mfano mwingine unaonekana katika (uk.199) msimulizi anapoeleza kuhusu uhusiano wa ndoa baina ya Munene na mkewe Deborah. Anasimulia ifuatavyo:

Ugomvi uliendelea kwa muda mrefu hadi Munene alipoamua kutumia silaha yake ya mwisho, aliyojua tangu hapo, akamkandika mkewe makofi kumnyamazisha (uk.199)

Uhusiano wa ndoa kati ya Munene na mkewe Deborah na jinsi walivyokuwa wakizozana kuhusu mwanao John unadhihirishwa. Deborah alikuwa amemweleza mumewe jinsi John alivyokuwa ameanza kubadilisha mienendo yake hasa baada ya kujiunga na shule ya Magnar Star. Munene aliyapuuza

haya yote na mkewe alipoendelea kumsisitizia aliamua kumtandika makofi kumnyamazisha.

Msimulizi anaeleza kuwa Munene alifanya hivyo kwa imani kuwa anapogombana na mkewe huwa hagombani ili kuufuata ukweli bali hufanya hivyo ashinde. Katika akili yake anaamini kuwa lazima dhamira ya kila mwanaume iwe ni iyo hiyo. Ingawa msimulizi amesimulia kuhusu maisha ya mhusika mkuu tangu utotoni hakuzingatia kaida ya mfuatano wa matukio, ametumia mbinu rejeshi na kielekezi mbele mtawalia.

2.5.2 Jukumu la Kumwelekeza Msomaji

Kwa mujibu wa Kenan (1983:95-96) msimulizi hutekeleza jukumu la kuwaelekeza wasomaji hasa kwa kukatiza hadithi anayosimulia kwanza ili aweze kutoa maoni yake aidha kuhusu mpangilio wa matini au kuhusu kile anachokisimulia. Msimulizi katika riwaya husika anatoa mwelekeo kuhusiana na mambo mbalimbali. Kwa mfano katika sura ya kwanza anamwelekeza msomaji katika usomaji wa riwaya husika. Anamhamasisha msomaji kuhusu usomaji wa riwaya yake iliyo na muundo mpya wa usimulizi ulio tofauti na muundo uliozoelewa hapo awali. Katika kufanya hivyo anamwandaa katika kukabiliana na mbinu mbalimbali za usimulizi zinazotumika katika riwaya teule. Anamhusisha msomaji kwa kumwambia:

Jifunge masombo, maana ngoma hii yataka matao. Jiandae. Ni ngoma inayokusihi uya-tupilie mbali mawazo ambayo umekuwa nayo kuhusu riwaya ya Kiswahili! Mtindo wake, sura yake na usimulizi wake ... (uk 1).

Msimulizi anajitokeza waziwazi na kumhusisha msomaji katika kazi yake. Anamwandaa katika usomaji wa simulizi. Hali hii imemfanya msimulizi kufupisha masafa yaliyopo kati ya hadithi na msomaji ili aweze kumchochea kuhusu mbinu mpya za usimulizi zinazotumika katika riwaya. Uelekezaji huu humfanya msomaji kuelewa kwa kina maana ya ujumbe unaokusudiwa katika hadithi.

Mfano mwingine unajitokeza katika sura ya mwisho. Hii ni baada ya msimulizi wa hadithi ya daraja la tatu kuhitimisha kijihadithi chake kuhusu "*Nyarubanja na watu wa kijiji cha Kinaa.*" Anahitimisha hadithi kwa kumhamasisha msomaji kuwa asisahau kuizingatia ngano aliyoisoma na kwamba asije akalidharau ini kwa kuwa ini huweza kumsonga mtu kooni. Anawakumbusha wasomaji wake kuwa:

Hii ni ngano ambayo mnapaswa kuipokezana kama chambi. Ni ngano yenye mafunzo. Na mkumbuke jingine; msidharau ini, humsonga mtu kooni. Isimulieni ngoma ya *Dharau ya Ini...*(uk.27)

Msimulizi anawasiliana na msomaji moja kwa moja na kumshirikisha katika kazi yake. Anamhamasisha kuhusu umuhimu wa kuisoma hadithi na kuyazingatia mafunzo yanayojitokeza. Isitoshe anamkumbusha umuhimu wa fasihi simulizi na kutoa madai kuwa ndio fasihi yenye uhai na ndio tunaishi. Zaidi ya kuwaelekeza wasomaji, msimulizi ana jukumu la kuwasiliana na msomaji moja kwa moja katika kazi ya fasihi.

2.5.3 Jukumu la Kumshirikisha Msomaji katika Usimulizi.

Msimulizi huweza kuchukua jukumu la kuwasiliana na hadhira moja kwa moja ili kuanzisha na kudumisha maingiliano kati yao katika simulizi kama anavyodokeza Kenan (1983). Katika (uk.1) msimulizi anajihusisha na hadhira moja kwa moja kwa kusudi la kumwanda katika usomaji wa hadithi inayofuata. Anamweleza msomaji:

Unachojua ni kuwa hapa pana kisa!
Na uko tayari kukifuata!
Nawe msomaji, uko tayari? Haya!! (uk.1)

Msimulizi anazungumza na hadhira moja kwa moja na kumhusisha katika usimulizi wa kijihadithi kinachofuatia baada ya usimulizi wa hadithi kuu. Kisa kinachosimuliwa katika sura ya pili kinahusu, “*Shujaa wa kifaru.*” Mawasiliano haya ni muhimu kwani yanatumika katika kumhamasisha na kuivuta makini ya msomaji ili kumwanda katika kukisoma kisa kingine tofauti kilicho ndani ya hadithi kuu.

Vilevile katika (uk.270) msimulizi anapotamatisha riwaya yake, anampongeza msomaji kwa ustahamilifu wake alipokuwa akiisoma riwaya husika na kumwambia:

Hukukata tamaa ya kuendelea kusoma?
Umesoma mpaka ukafika huku? Hongera
hata! Riwaya inapoisha huenda msomaji
unilaumu kuwa sijakusimulia kile kisa
ulichosimuliwa na babu ... jiandae...
(uk.277)

Msimulizi anampongeza msomaji kwa sababu ya kuisoma riwaya hadi anapokaribia tamati. Anaona labda msomaji huenda akamlaumu kuwa hajamsimulia kisa alichokuwa amesimuliwa na babu. Msimulizi anamwanda msomaji katika kukisoma kisa kingine tofauti na anachosimulia ili kuiteka

makini yake. Maneno kama vile ‘hukukata tamaa’ na ‘umesoma’ yanadhihirisha kuwa msimulizi anamshirikisha msomaji moja kwa moja katika usimulizi wake. Msimulizi anamwandaa kukisoma kijihadithi kinachohusu “*Mzungu na wanakijiji wa Kinaa barani Afrika*”

Mfano mwingine ambapo msimulizi anamhusisha msomaji katika usimulizi wa hadithi unadhihirika katika wimbo unaoimbwa na mmoja wa wahusika katika hadithi. Mwimbaji anawakumbusha wanakijiji umbali walikotoka kabla ya ujio wa wageni Wazungu. Anaimba:

Tulitoka Kinaa, tukawa kinyaa, chenye
unyarafu,
Tulitoka Kinyaa, tukawa Kenyaa, furaha
timilifu,
Tusitoke Kenyaa, tuwe kinyaa, chenye
uchafu...(uk.278)

Wanakijiji wanaonywa dhidi ya kuvuruga amani na kuzua machafuko katika kijiji chao. Wimbo huu unadhihirisha wazi kuwa msimulizi anaihusisha hadhira moja kwa moja katika usimulizi wake. Maneno; “Tusitoke Kenyaa, tuwe kinyaa, chenye uchafu”, inajumuisha hadhira pamoja na msimulizi. Baada ya kuikamilisha hadithi yake, msimulizi anawasiliana moja kwa moja na wasikilizaji kwa kuwahimiza kuipokezana ngano hii kwani ni ngano yenye mafunzo muhimu. Hatimaye anawashauri wasomaji wasilidharau ini kwani huenda likawasakama kooni wakilidharau. Anawapa changamoto ya kuicheza, kuiimba na hata kuisimulia ngoma ya *Dharau ya Ini*.

2.5.4 Jukumu la Kuwasilisha Itikadi zake kwa Msomaji

Jukumu la kiitikadi kama anayodai Kenan (2003) hujitokeza katika simulizi wakati msimulizi anapokatiza usimuliaji wa hadithi ili kutoa mafunzo ya hekima au maoni fulani kuhusu hadithi anayosimulia. Hali hii inadhihirika wazi katika (uk.171) Lila anaposema kuwa alikuwa tayari amemweleza mwanahabari mwenzake, Derby, kuhusu kifo cha babake pamoja na ushahidi aliokuwa nao wiki iliyotangulia. Anaendelea kusema kuwa alikuwa amemwona wakili ingawa hakumweleza mambo yote kwa kuwa alishindwa kumwamini mara moja. Anamweleza:

Usinilaumu, nimekulia katika nchi ambayo
imenifunza kuwa si vyema kumwamini mtu
kabisa. Hofu? Woga? Unafiki? Sijui riwaya
yenyewe inakuelekeza wapi kama msomaji!
Uk (171)

Msimulizi anaonyesha wazi kuwa hawezi kumwamini wakili aliyekuwa akishughulikia kesi kuhusu kifo cha babake kwa kumpa habari zote mara moja. Lila anatoa sababu kuwa amekulia katika nchi iliyomfunza kutoamini mtu kabisa kwa hofu ya usaliti. Hali hii imeijenga imani yake ambayo anaiwasilisha mbele za msomaji. Kauli hii ya Lila inaonyesha kuwa amekatiza maelezo ya hadithi kutokana na ripoti ya uchunguzi wa kifo cha babake na kisha akatoa maoni yake kuhusiana na uwasilishaji wa ripoti hiyo kwa wakili wake.

Mfano mwingine unajitokeza katika (uk.232) Lila anapoandamana na Derby katika safari ya kumtembelea babu yake. Wanapoingia katika makao yake huko kijijini, wanakutana na kijana aliyekuwa akimsaidia pale shambani. Yule kijana ndiye aliyejitokeza kwanza. Babu yake hakuwa amejitokeza wakati huo

wote na hiyo haikuwa tabia yake. Hali hiyo inamfanya Lila kukatiza hadithi na kuanza kusema:

Papara ni za vijana; wazee huwa wame-shatambua, hamna cha kukimbilia tena. Fimbo ya maisha huwa imewachapa vya kutosha na kuifanya miili yao iishiwe na nguvu za kurukaruka kama wana-mbuzi (uk. 232)

Lila anayasema maneno haya baada ya kutambua kuwa babu yake alikuwa amejikokota sana alipokuwa akitoka shambani hadi akakawia sana kufika pale nyumbani. Kijakazi wake alikuwa ametangulia mapema. Msimulizi anasitisha usimulizi wake ili kuyaweka maneno haya wazi mbele ya msomaji. Anayatoa maneno ya hekima kuhusiana na hadithi anayosimulia, hali inayomfanya msomaji kupata funzo fulani kuhusu maisha.

2.5.5 Jukumu la kutoa Ushuhuda kuhusu matukio

Kwa mujibu wa Kenan (2003), msimulizi anaposimulia matukio fulani katika hadithi, huweza kuthibitisha ukweli wa hadithi yake na kuonyesha uhakika kuhusu matokeo na chanzo cha habari anayoisimulia. Masimulizi huweza kuzua maswali kama; Je, msimulizi ni wa kuaminiwa? Je, anaonyesha anajua mengi kuhusu hadithi anayosimulia? Je, maadili ya usimulizi wake yanaoana na hadithi yake bila kuibua uhitilafiano kati ya maelezo yake na anachosimulia?

Kulingana na Kenan, msimulizi wa kutegemewa ni yule anayewasilisha hadithi na kutoa maoni kwa wasomaji kwa njia ya ukweli na ubunifu ili msomaji aweze kumwamini na kumtegemea katika usimuliaji wake. Msimulizi wa hadithi kuu ambaye anatambulishwa kama Lila, anatoa ushuhuda kuhusu kisa anachosimulia kama mwanahabari. Kisa chake kinahusu jinsi yeye na

mwanahabari mwenzake Derby walivyotekwa nyara na watu wasiojulikana kisha wakafungwa macho kwa vitambaa na kuelekezwa hadi katikati ya msitu wa Marimba na kuachwa huko. Baada ya kutafuta kijia kilichojitokeza katika njia kuu walibahatika kupewa lifti kwa gari la watalii.

Lila anaendelea kusema kuwa, mmojawapo wa watalii waliokuwemo ndani ya gari hilo alikuwa anasoma gazeti lililokuwa linaeleza kuhusu kisa cha kupotea kwao. Msimulizi anaposimulia kisa hiki anawasiliana na msomaji moja kwa moja na anamwambia:

Hata wewe unayeisoma riwaya hii unaweza kukisia hisia nilizokuwa nazo kuwa watu wa kwanza wa kukijua kisa hiki walikuwa wageni...(uk. 216).

Lila anamjulisha msomaji kuwa hata wageni waliokuwa katika gari lililowabeba walikuwa wamesoma habari kuhusu kupotea kwao. Anaeleza kuwa kisa hiki kinamkumbusha methali aliyoipenda babu yake, “Ngozi ya kulala haitolewi nje wafikapo wageni”. Ilimbidi ayamezee mambo fulani ili asiwape wageni wale nafasi ya kufahamu mambo yao kama wanahabari kwa undani. Kutokana na maelezo haya, msimulizi anamfanya msomaji kumwamini kuwa kisa anachosimulia ni cha kuaminika ingawa ni cha kiubunifu.

Kutokana na muktadha huu, msimulizi anadhihirisha ukweli wa hadithi yake kwa msomaji kuhusu chanzo cha matukio anayosimulia. Hali hii inamfanya kutegemewa na msikilizaji na kuweza kuaminiwa kutoa ukweli katika kisa anachosimulia. Mfano mwingine unajitokeza katika (uk.219). Lila alipokuwa akizipiga nguo zake pasi kwa maandalizi ya kuelekea kazini, alikumbuka jinsi walivyokuwa wakizipiga nguo zao pasi wakiwa shuleni. Walikuwa wakisema

kuwa hiyo ilikuwa njia ya kuviua vidudu vyovyote katika nguo hizo. Katika harakati za masimulizi hayo Lila anamfahamisha msomaji kuhusu hali ya maisha yake alipokuwa shuleni. Anamweleza ifuatavyo:

Sijui kama riwaya hii imekutajia kuwa nimekulia mashambani. Nywele tulitengeneza kwa makopo yaliyotiwa motoni. Tukiwa shuleni niliosha gauni langu nikalikausha kwa moto. Asubuhi likawa lanuka moshi (uk.219)

Lila anaonyesha kuwa asili yake ni sehemu za mashambani, hivyo hajazoea kufanya mambo kama watu wa mjini. Maelezo haya yanamfanya msomaji aweze kumwamini msimulizi kuwa kisa anachosimulia ni cha ukweli ingawa ni cha kiubunifu. Ametoa ukweli kwa njia ya kiubunifu, hali inayomfanya awe msimulizi wa kutegemewa na kuaminiwa na wasomaji wake.

2.6 Kiishilio

Sura hii ilichanganua sauti ya usimulizi na viwango vya usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Utafiti ulijikita katika nafsi za usimuliaji, uonekanaji wa msimulizi, mahusiano ya wakati wa usimulizi, nafasi ya msimulizi na viwango vya usimulizi. Ilidhihirika kuwa msimulizi ametambulishwa kwa njia iliyo wazi katika sehemu kubwa ya simulizi na sehemu zingine amejificha akakosa kuonekana wazi mbele ya msomaji. Msimulizi amehusisha nafsi zote tatu katika ukuzaji wa ujumbe. Utafiti ulionyesha mahusiano ya wakati wa usimuliaji kwa kuzingatia nyakati zote tatu kuu. Ilibainika kuwa mwandishi amehusisha viwango mbalimbali vya hadithi ambavyo vinaenda sambamba na viwango vya usimulizi. Sura inayofuata imechanganua nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya teule.

SURA YA TATU

NAFASI YA WAKATI KATIKA USIMULIZI WA RIWAYA YA *DHARAU YA INI*

3.0 Utangulizi

Sura hii ililenga kuchanganua nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya ya *Dharau ya Ini*. Utafiti ulijikita katika vigezo vitatu ambavyo ni mpangilio wa matukio, muda wa utokeaji wa matukio, na idadi ya utokeaji wa matukio hayo. Sehemu hii ililenga kubainisha uhusiano baina ya usimuliaji wa hadithi na wakati katika matini ili kuonyesha jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka kwao moja baada ya lingine. Kazi hii ilinua kudhihirisha iwapo matukio katika hadithi yamefuatana kiwakati au yamekiuka kaida ya mpangilio huo. Vilevile ililenga kuchanganua uhusiano kati ya utokeaji wa matukio na mara ambazo matukio hayo yamesimuliwa. Lengo lilikuwa kubainisha iwapo miundo ya sentensi huweza kubadilika matukio yanapotokea na yakasimuliwa mara kadha au miundo hiyo hubaki vilevile. Utafiti ulichanganua vigezo vya wakati kwa kina na kudhihirisha nafasi yake katika riwaya teule.

3.1 Wakati katika Usimulizi

Wakati kulingana na Kenan (1983) ni uhusiano wa kronolojia kati ya hadithi na matini na huonyesha jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka kwao moja baada ya lingine. Matukio yoyote hutendeka katika wakati fulani katika hadithi kama wanavyodokeza Gennette (1980) na Kenan (1983). Wahakiki hawa wamebainisha wakati kwa njia mbili; wakati hadithi na wakati matini.

Kwa mujibu wa Gennette (1980) wakati hadithi katika simulizi ni kipimo cha kasi au mwendo katika usimulizi wa hadithi. Kasi huwa ni matokeo ya uainishaji baina ya wakati wa usimulizi wa hadithi na urefu wa matini katika simulizi. Anasema kuwa wakati wa kusimulia hadithi unaweza kucheleweshwa au kuharakishwa kutegemea urefu wa matini iliopo. Kenan (1983) anakubaliana na mawazo ya Gennette kwamba wakati hadithi umechukuliwa kuonyesha wakati inayochukua hadithi kusimuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wake. Wakati huu unaweza kuwa siku moja au miaka mingi kiasi cha kuhusisha vizazi vingi.

Hadithi ya *Dharau ya Ini* imehusisha kipindi kirefu kusimulia matukio mbalimbali. Msimulizi anaeleza kuhusu maisha ya Munene tangu alipokuwa na umri wa miezi kumi. Msimulizi anasimulia kuhusu elimu ya mhusika huyu, kazi alizofanya na maisha yake ya ndoa. Anaeleza kuhusu maisha yake kama mfanyibiashara na mwanasiasa mkubwa jijini Kitambasye na pia anaonyesha maisha yake akiwa mzee aliyekonga na hatimaye anapoaga dunia. Msimulizi hajazingatia kaida ya mfuatano wa matukio kiwakati, hali inayoifanya hadithi kuchukua kipindi kirefu kusimuliwa.

Wakati matini kama anavyodokeza Kenan (2003) ni muda inayochukua matini fulani kusomwa. Anasema kuwa wakati-matini huweza kuhusisha swali kama, Je, inachukua muda gani kuisoma matini? Hivyo inaweza kuchukua kikao kimoja au vikao vingi kuisoma hadithi jinsi asemavyo Gennette (1980). Anaeleza kuwa wakati matini unaweza kupimwa kulingana na idadi ya maneno, mistari au kurasa za kitabu.

Gennette (1980) ameanisha wakati kwa vigezo vitatu muhimu kama vile mpangilio wa matukio, muda wa matukio, idadi ya utokeaji wa matukio na mara ngapi matukio hayo yanasimuliwa katika hadithi. Sehemu hii imechanganua vigezo hivi vya wakati na kuonyesha nafasi ya kila kimoja katika riwaya.

3.1.1 Mpangilio wa Matukio

Mpangilio wa matukio kwa mujibu wa Gennette (1980) ni mfuatano wa matukio katika hadithi kulingana na uwasilishaji wake. Matukio katika hadithi yanaweza kusimuliwa kulingana na jinsi yanavyotokea kiwakati. Hali ikiwa hivyo basi msuko wa hadithi na mpangilio wake huwa sawa. Kwa upande mwingine anasema kuwa hadithi inaweza kusimuliwa bila ya kuzingatia kaida ya mfuatano wa matukio kiwakati.

Kulingana na Kenan (1983) mfumo usiozingatia kaida ya mpangilio wa matukio huzua uhitilafiano kwani unaonyesha hali ya ukosefu wa mapatano kati ya jinsi matukio yanavyoonekana katika msuko na jinsi yanavyopatikana katika hadithi. Anasema kuwa hali hii humfanya msimulizi arudi katika matukio ya nyuma ili kufafanua maelezo kuhusu wahusika katika usimulizi uliopo. Uhitilafiano huu kama anavyodokeza Kenan, huitwa anakroni na huweza kuainishwa kwa namna mbili; analepsia na prolepsia. Utafiti ulichanganua kila kigezo na kuonyesha jinsi kinavyodhihirika katika riwaya ya *Dharau ya Ini*.

3.1.2 Analepsia

Analepsia kwa mujibu wa Kenan (1983) ni hali ambapo msimulizi anasitisha hadithi na kuyarudia matukio ya nyuma kwanza. Msimulizi anaposimulia hadithi hurejelea matukio ya wakati uliopita ili kutoa msingi na kufafanua matukio ya wakati uliopo kama anavyodokeza Toolan, (1988). Anasema kuwa hali hii humfanya msomaji kutafakari yaliyotokea na kubainisha tofauti zilizopo kati ya jana na wakati uliopo au kati ya msimulizi au mhusika kijana na alivyo kama mtu mzima.

Katika riwaya ya *Dharau ya Ini* mbinu rejeshi imedhihirika katika sehemu kubwa ya hadithi. Mbinu hii ni muhimu katika simulizi hasa katika kuunganisha au kuhusisha sura na matukio katika hadithi. Kwa mfano katika sura ya kwanza (uk.4) msimulizi ambaye ni mwandishi wa habari katika shirika la habari la Mpapure anasimulia kisa kuhusu safari yake ya kwenda kutafuta alikofia na kuzikwa babake. Anamrudisha msomaji nyuma katika matukio ya wakati uliopita na kueleza jinsi maisha yake kama msichana mdogo yalivyokuwa.

Lila anasimulia matukio yake ya nyuma akiwa msichana mdogo tofauti na alivyo kama mtu mzima. Anaeleza vile wasichana walivyokuwa wakichunwa sikio na kuonywa kila wakati. Mila na desturi zao zilimfunga msichana katika utaratibu fulani hivi kwamba walikuwa wanakumbushwa kila mara kuwa msichana hapaswi kukaa hivi au vile wala hacheki ovyo...(uk.4). Hali hii ilimjia Lila mawazoni alipopigwa na upepo mkali mpaka gauni yake ikainuliwa na kupeperushwa hadi kumuacha nusu uchi. Lila anaona kuwa hali

ingekuwa tofauti iwapo wazazi wake wangukuwa karibu wakati huo kwani wangemsuta vilivyo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), analepsia huweza kutoa msingi wa sababu zinazowafanya wahusika kutenda mambo fulani katika simulizi. Katika (uk.11) msimulizi anaturudisha katika matukio ya nyuma na kutuonyesha jinsi maisha ya awali ya mhusika Munene yalivyokuwa. Anasema:

Munene alikuwa yai la kuengaengwa; mtoto
huyu alikuwa mboni ya jicho la babake na
yeyote aliyethubutu kumkanya lolote alikuwa
akijichongea (uk.110)

Muktadha huu unadhihirisha jinsi Munene alivyolelewa kwa kudekezwa na alipofanya makosa hakuadhibiwa wala kuonywa. Hapa msimulizi anamrudisha msomaji katika matukio yaliyotendeka wakati uliopita ili kumweleza sababu zinazochochea kuwepo kwa matukio yanayosimuliwa wakati uliopo. Msimulizi anaposimulia matukio ya wakati uliopita kumhusu mhusika wake, anamfanya msomaji kupata ufahamu zaidi kuhusu usuli wa mhusika na jinsi maisha yake ya nyuma yanavyoathiri hali iliyopo kama anavyosisitiza Toolan (1988). Usimulizi wa aina hii humfanya msomaji apate ufahamu zaidi kuhusu matukio yanayosimuliwa katika hadithi.

Kudekezwa kwa Munene kunachangia kitendo cha kumbaka msichana wa darasa la saba kijijini kwao. Msichana huyo alikuwa akipitia katika ardhi yao huko Kitambasye, Munene alipomnyemelea na kumbaka huku akimziba mdomo kwa kitambaa ili asitoe sauti yoyote. Msimulizi anapoyasimulia matukio yaliyopita anamfanya msomaji kupata ufahamu zaidi kuhusu matendo

ya awali ya mhusika na jinsi yanavyoathiri maisha yake ya wakati uliopo. Msimulizi anaeleza kuwa Kivu, babake Munene, alitoa madai kuwa mwanawe alisingiziwa hali iliyoifanya kesi hiyo itupiliwe mbali. Hali hii ilimchochea Munene kukirudia kitendo hicho baadaye kama inavyoelezwa kuwa:

Alikirudia kitendo hicho akiwa mwanafunzi
na kuhongerwa na babake; akampiga miereka
kiumbe aliyekuwa akipiga usiahi; akamtia goe
huku anamzomea kwa sauti kama fisi (uk.11)

Munene alishiriki kitendo cha kumnajisi msichana fulani kijijini mwao. Msimulizi anaeleza kuwa tabia hizo zilichochewa na ukosefu wa malezi bora. Mhusika alikua huku akidekezwa na wazazi wake hivi kwamba alipofanya makosa alihongerwa badala ya kukashifiwa. Hali hiyo iliathiri sana mienendo yake ya baadaye na kumfanya akirudie kitendo kile cha unajisi alichokuwa ametenda hapo awali.

Mbinu rejeshi imetumika ili kutoa msingi wa sababu zinazomfanya Munene atende yale aliyoyatenda. Msimulizi anamrudisha msomaji nyuma ili kumuonyesha tabia za awali za mhusika huyu.

Mbinu rejeshi huweza pia kutumika katika kutoa taswira kuhusiana na masuala ya kijamii yanayomzingira mhusika na kutoa sababu zinazowafanya kutenda mambo fulani (Manred, 2005). Msimulizi anamrudisha msomaji wake nyuma ili kumuonyesha jinsi maisha ya Munene yalivyokuwa kabla ya kupata mali. Anatoa taswira kwa msomaji ili aweze kuyalinganisha Maisha ya mhusika ya wakati uliopita na sasa. Kuna ushahidi kuhusu mabadiliko katika mienendo

yake hasa baada ya kuimarika kifedha na kuanzisha duka kubwa la biashara katika soko la kijijini. Msimulizi anaeleza kuwa:

Zamani alikuwa na umbo jembamba, gofu la mtu na sasa aliujaza mwili wake huo kwa ulaji mzuri. Tabia yake nayo ilikuwa imebadilika akajaa kiburi na dharau (uk.10)

Munene sasa alikuwa na siha nzuri akilinganishwa na hali iliyokuwepo awali kutokana na ulaji mzuri. Tabia yake nayo ilikuwa imebadilika akawa mwenye kiburi na dharau tangu alipoanza kuimarika kifedha. Msimulizi anarejelea matendo yaliyotokea wakati uliopita ili kuyalinganisha maisha ya Munene ya awali na ya wakati uliopo.

Kwa mujibu wa Kenan (1983) msimulizi anaweza kuhusisha matukio ya wakati uliopita ili kutoa taswira kuhusu maisha ya awali ya mhusika fulani. Anasema kuwa hali hii humfanya msomaji kupata ufahamu wa kina kuhusu maisha ya awali ya mhusika na kuyalinganisha na hali iliopo. Tabia ya Munene ya kujisifu pia inathahirika wazi katika ndoa yake hasa anapobishana na mkewe Katumbi hasa anapokosa kumzalia mtoto wa kiume (uk.38). Katumbi alikataa kupata mtoto wa nne kwani aliona mambo ya kupata watoto wengi ili kutafuta mvulana yamepitwa na wakati. Naye Munene hakukubaliana na mtazamo wa mkewe. Anamjibu kwa kiburi:

Unaweza kuwazaa watoto idadi yoyote mradi
una uwezo wa kiuchumi, na huo ninao...
(uk.38)

Munene anajivunia hadhi aliyonayo kiuchumi na haelewi ni kwa nini mkewe hataki kumzalia watoto wengi kwa lengo la kutafuta mvulana ilhali ana uwezo

wa kifedha. Msimulizi anamrudisha msomaji katika maisha ya nyuma ya Katumbi kabla mumewe kumtaliki. Kwa sasa Munene amekwisha kuoza mke mwingine atakayemzalia mvulana. Chanzo cha kiburi hicho ni malezi mabaya pamoja na uwezo wa kifedha aliokuwa nao kwa sasa.

Maelezo haya yanadhihirisha wazi matumizi ya mbinu rejeshi ambayo hutoa msingi wa kuonyesha jinsi matukio ya wakati uliopita yanavyoathiri maisha ya wakati uliopo. Analepsia inapotumika kwa wingi huweza kuchelewesha usimulizi wa hadithi, yaani haipeleki hadithi mbele. Hali hii huufanya muda wa usomaji wa hadithi uendelee kuongezeka kama anavyoeleza Toolan (1988).

3.1.3 Prolepsia

Kulingana na Gennette (1980), prolepsia ni hali ya usimuliaji wa matukio yajayo kabla ya kutendeka kwake. Hivyo ni matukio yanayotarajiwa kutokea katika siku zijazo. Hali hii huleta matukio ya baadaye katika hadithi kabla matukio ya sasa kusimuliwa. Matukio haya yanaweza kutokea kama yanavyotarajiwa au wakati mwingine yakakosa kutendeka kamwe kama asemavyo Kenan (1983: 46-51). Anasema kuwa mbinu hii ni nadra sana ikilinganishwa na mbinu rejeshi. Ingawa hivyo mbinu hii imetumika katika katika (uk.13) msimulizi anaposimulia kuhusu maisha ya baadaye ya Munene akiwa mzee aliyekonga. Anaeleza kuwa:

Munene analizungusha tama la chai kinywani huku midomo ikimchezacheza. Anauchukua mkongojo wake wa kutembelea, anakohoa na kuvuta hatua mbili-tatu kufikia langoni...(uk 13)

Munene anakunywa chai kwa shida huku midomo ikimchezacheza. Anatembea kwa mkongojo huku akijivuta ili afikie mlangoni. Msimulizi anatoa taswira kuhusu maisha yake ya siku za usoni akiwa amekonga na akiwa dhaifu mwilini. Mwandishi ameanza kwa kusimulia kisa cha kumaliza hadithi wakati matukio ya sasa yanaposimuliwa.

Usimulizi huu unazua uhitilafiano kati ya jinsi matukio yanavyoonekana katika msuko na jinsi yanavyopatikana katika hadithi kama asemavyo Kenan (1983). Anasema matumizi ya prolepsia inaweza kuzua taharuki kwa msomaji kuhusu yale yatakayotokea baadaye kumhusu mhusika. Vilevile ni njia ya kumpa mhusika matumaini kuhusu matarajio yake katika maisha ya baadaye hasa kutokana na hali yake ya sasa.

Usimulizi wa aina hii pia unaweza kujitokeza wakati ambapo viwakilishi vya wakati ujao vimetumika kuonyesha matukio yanayosimuliwa hayajatokea ingawa yanatarajiwa kutendeka. Usimulizi wa aina hii unajitokeza katika (uk.52) wakati Kasina, mkewe Munene, anapojiambia kuwa:

Mumewe atamrudia baada ya kuhangaika
huku na huku kama mwana mpotevu;
atatapatapa huku na kule kama kongoni,
hatimaye atamjia, tena mbio ... (uk.52)

Kasina anajipa matumaini kuwa mumewe atamrudia kwani alikwisha kumtaliki na kuoia mke mwingine. Hata hivyo, kulingana na simulizi, matumaini yake hayakutimilika wala kusimuliwa tena. Mumewe hakumrudia kama alivyodhani bali alioa wake wengine wawili kwa lengo la kutafuta mtoto wa kiume ambaye angemrithi. Msimulizi ametumia kiambishi cha wakati ujao 'ta' kuonyesha

matukio yanayosimuliwa hayajatokea ingawa yanatarajiwa kutokea. Hivyo usimulizi wa aina hii hutumika kama njia ya kuwapa wahusika matumaini kuhusu matukio ya siku zijazo hasa kutokana na changamoto zinazowakabili katika wakati uliopo.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa matukio katika hadithi yanaweza kusimuliwa kulingana na jinsi yanavyotokea kiwakati au yakakosa kuzingatia kaida ya mfuatano huo kiwakati. Mwandishi amezingatia mbinu rejeshi na mbinu elekezi katika uwasilishaji wa matukio na hali hii imedhihirishwa kupitia mifano mbalimbali katika riwaya teule. Sehemu inayofuata ilishughulikia kigezo cha muda wa matukio.

3.2 Muda wa Matukio

Kulingana na Gennette (1980) muda ni kigezo muhimu cha wakati kinachoonyesha muda ambao tukio limekuwa likisimuliwa. Kipindi hicho kinaweza kuwa kirefu au kifupi. Huhusisha swali, je, tukio limechukua muda mrefu au mfupi kusimuliwa? Hivyo tofauti ya kimsingi inayopaswa kuthibitishwa ni ile inayojitokeza baina ya wakati hadithi na wakati matini. Anafafanua wakati matini kama muda anaochukua msomaji wa kawaida kusoma kifungu au hadithi nzima. Wakati matini unaweza kupimwa kulingana na idadi ya maneno, mistari au kurasa za matini. Swali linalojitokeza kulingana na Kenan (1983) ni Je, matini inaweza kusomwa katika kikao kimoja? Je, wakati matini unahusianaje na wakati hadithi? Je, inachukua muda gani kukisoma kisa fulani?

Wakati wa kusimulia hadithi kwa mujibu wa Gennette (1988) ni muda unaochukuliwa katika usimuliaji wa kisa fulani. Wakati wa hadithi hutegemea urefu wa matini, welewa wa msomaji au ishara ya uelekezaji wa maana katika matini husika. Wasomaji mbalimbali wana mwendo tofauti wa kusoma na kwa hivyo ni vigumu kukadiria mpito wa wakati. Ni kutokana na hali hii ambapo Toolan (1988) anapendekeza hali ya kutumia kile anachokiita ‘kasi’ au ‘mwendo’ kama kigezo muhimu cha kupimia viwango mbalimbali vya mpito wa wakati.

Toolan (1988) anaeleza kuwa mwendo unaweza kuwa uwiano kati ya muda unaochukuliwa kuisimulia hadithi na urefu wa matini inayohusika katika hadithi. Anadokeza kuwa riwaya inaweza kutumia ukurasa mmoja pekee kuwasilisha matukio ya mwaka mmoja au zaidi au ikahusisha kurasa nyingi kusimulia kisa chicho hicho.

Hivyo, kutegemea kigezo cha muda, wakati wa usimuliaji hadithi unaweza kuongezeka au kupunguka katika hadithi. Mwendo wa usimuliaji wa hadithi unaweza kupunguka iwapo matini inayohusika ni ndefu au msimulizi anapostisha usimulizi wa hadithi iliyopo ili kutoa sifa za wahusika au ndoto zao. Gennette (1988) amesainisha muda kwa jinsi nne ambazo ni mtuo, udondoshi, muhtasari, onyesho na uendelezaji. Sehemu hii imechanganua kila kigezo na kuonyesha nafasi yake katika usimulizi wa riwaya.

3.2.1 Mtuo

Manfred (2005) anafafanua mtuo kama hali ambapo usimulizi wa hadithi husitishwa ili kuyapa nafasi maelezo mengine bila kuwepo kwa utendaji

wowote wa wahusika. Mawazo ya Wamitila (2003) yanaafikiana na haya anaposema kuwa mtuo ni maelezo au mawazo ya ziada yanayotumika kuisitiza jambo fulani. Anaeleza kuwa usimulizi kama huu unaweza kuongeza msisimuo na taharuki ya hadithi yenyewe.

Matumizi ya mtuo huufanya wakati wa kusimulia hadithi kuwa mfupi ilhali wakati unaotumika kuelezea matini huwa umerefushwa. Mbinu rejeshi inaweza kutumika katika hali hii kwa kuwa haipeleki hadithi mbele bali huirudisha nyuma na hivyo kuzidisha wakati matini. Usimulizi wa aina hii humfanya msomaji kuzidisha muda wa kuisoma hadithi. Mfano wa mbinu rejeshi unajitokeza katika (uk.36) Kasina:

Anakumbuka vile Munene alivyomtupia
jicho kali baada ya mkewe kujifungua mtoto
wa kike. Alimeza mate kwa shida. Akageuka
na kuubamiza mlango na kuondoka (uk.36)

Msimulizi anamrudisha msomaji nyuma kumwonyesha maisha ya Kasina na Munene kabla ya ndoa yao kuvunjika. Kasina anakumbuka vile Mumewe alivyomtupia jicho alipojifungua mtoto wa kike. Munene alimbeza na kumpuuza Kasina kwani alikuwa anatarajia kupata mtoto wa kiume. Kisa hiki kilikuwa kimetokea miaka mingi iliyopita na kilisababisha kuvunjika kwa ndoa yao hali iliyomfanya Kasina kusunoneka kila kukicha.

Maelezo kuhusu ndoa ya Munene na Katumbi yanasitishwa ili kuyapa nafasi maelezo ya nyuma kuhusu ndoa ya awali ya Munene na mke wake wa kwanza. Hali hii inatumika katika kujenga msingi wa matukio ya sasa. Hali hii inachelewesha usimulizi wa hadithi na kuifanya isiendele mbele. Kigezo cha

muda pia kinaweza kudhihirika katika ndoto za wahusika. Munene katika (uk.110) anaota ndoto akiwa usingizini kwake nyumbani. Ndoto hii ilihusu karamu moja kubwa iliyowahusisha watu wengi. Msimulizi anatumia kuwa Munene:

Alijiona akipaa juu kabisa kisha akaanguka
chini kwa mwanguko mkubwa. Ghafla alitambua
miguu yake ilifanana na ya mnyama,
mikono ilibakia ya binadamu na kichwa chake
kilikuwa na pembe. (uk.110).

Munene anaota ndoto akiwa usingizini. Anajiona akipaa juu kabisa na punde tu anaanguka kwa mshindo mkubwa. Kisha miguu yake inabadilika na kufanana na ya mnyama huku kichwa chake kikiota pembe. Kuwepo kwa ndoto hii ni ishara kuwa hadithi inayosimuliwa haisongi mbele kiwakati kwa vile mhusika amelala bila kutenda lolote. Msimulizi anasitisha usimulizi wa hadithi ili aelezee kuhusu ndoto ya mhusika wake. Hali hii inapelekea wakati wa hadithi kuwa mfupi kuliko wakati wa matini kama anavyoeleza Kenan (2003).

Mtuo pia hujitokeza wakati msimulizi anapositisha usimulizi wa hadithi ili kutoa sifa au maelezo ya ziada kuhusu mhusika fulani kama anavyoeleza Muller (1948). Sifa hizo humwezesha msomaji kupata taswira fulani kuhusu mhusika anayesimuliwa. Kwa mfano katika (uk.32) msimulizi anatoa maelezo kuhusu tabia za mzee mbulu kuwa:

Mzee Mbulu alikuwa mcheshi kabla ya
kufanyiwa hiana na ulimwengu na wali-
mwengu wenyewe na uchangamfu wake
kukunjamana kama kifaurongo kilichoguswa
na mikono ya adui... (uk.31)

Msimulizi anasitisha uendelezaji wa hadithi na kuyapa nafasi maelezo kuhusiana na tabia za mzee Mbulu na jinsi alivyokuwa mcheshi kabla ya kukabiliwa na matatizo chungu nzima. Msimulizi anapositisha hadithi ili kutoa sifa za wahusika wake husababisha wakati hadithi kuwa mfupi kuliko wakati matini. Hali hii inachelewesha usimulizi wa hadithi na kuifanya isisonge mbele. Katika hali hii, msimulizi huweza kuwapa wasomaji nafasi ya kupata ufahamu zaidi kuhusu tabia na mienendo ya mhusika wake hasa anaposimulia kuhusu matukio ya nyuma yanayomhusu mzee Mbulu.

Kulingana na kigezo hiki, hadithi inaweza kusitishwa ili kuyapa nafasi maelezo mengine hivyo utendaji wa matukio ukakosa kuonekana. Hali hii hujitokeza iwapo msimulizi amehusisha matukio ya wakati uliopita, ndoto za wahusika, tabia za mhusika au anapoeleza kuhusu mandhari fulani katika simulizi. Sehemu inayofuata ilichanganua muhtasari kama kigezo kingine cha muda.

3.2.2 Muhtasari

Muhtasari ni ufupishaji wa muda fulani wa hadithi kwa kauli chache kama anavyodokeza Bonheim (1982). Anasema kuwa muhtasari hutumiwa kuharakisha hadithi kwa kuyaondoa maelezo mengine ambayo hayana maana au hayana mchango mkubwa katika hadithi. Kenan (2003) anaafikiana na mawazo haya na kusema kuwa, mwendo au muda wa kusimulia hadithi unaweza kufupishwa kwa kuibana matini au kwa kutumia kauli fupi fupi za matukio. Hali hii husababisha kasi au mwendo wa usimuliaji wa hadithi kuharakishwa. Wakati wa usimuliaji hadithi huwa mfupi ilhali wakati matini

huwa mrefu. Katika (uk.2) msimulizi anaanza usimulizi wake kwa kutueleza kuhusu marehemu babake. Anaeleza kuwa:

Riwaya ianzapo miaka mingi ilikuwa imepita tangu baba afe; hata sura yake ninayo-kumbuka kutokana na picha ya zamani ilikuwa imeanza kunitoweka pole pole... (uk.2)

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kipindi kirefu kimepita baina ya wakati baba ya Lila alipoaga dunia na wakati anapoanza kuisimulia hadithi yake. Anasema kuwa muda mrefu umepita kiasi kwamba alikuwa ameanza kuisahau sura ya babake. Kauli hii ni fupi lakini hadithi inayorejelewa ni ndefu sana na kipindi kirefu kimepita tangu babake afe. Msimulizi hajadhihirisha muda huo wazi bali anasema, ‘miaka mingi ilikuwa imepita.’ Kauli hii imetumika kuufupisha muda wa usimuliaji wa hadithi husika. Muda wa usomaji wa hadithi umepunguzwa kwani kuna maelezo mengi ambayo yamedondoshwa.

Mfano mwingine wa muhtasari unajitokeza katika (uk.12) msimulizi anapoeleza yafuatayo kuhusu Munene wakati wa sherehe za uhuru. Anasema kuwa:

Sherehe za uhuru nchini; mwanzo wa miaka ya sitini taifa huru lilipovunja chupa, ilimkuta Munene akiwa barobaro, aliyetaka kuonyesha ulimwengu mzima kuwa alikuwa mtoto wa chifu... (uk.12)

Kipindi cha sherehe za uhuru katika miaka ya sitini, kilimkuta Munene akiwa barobaro ambaye alitaka kuonyesha ulimwengu kuwa alikuwa mtoto wa chifu. Hadithi inaposimuliwa Munene anadhihirika akiwa na umri wa makamo akiwa

ameoa na kupata watoto. Kifungu hiki kinadhihirisha kuwa wakati wa kusimulia hadithi umefupishwa kwa kauli chache tu, hali inayoharakisha muda wa usimuliaji wa hadithi. Mwanzo wa miaka ya sitini unaweza kuwa kipindi kirefu cha matukio kutendeka hali ambayo imefupishwa kwa kauli chache tu. Hali hii inadhihirika wazi msimulizi anapoeleza kuwa sherehe hiyo ilikuwa katika ‘mwanzo wa miaka ya sitini.’

Mfano mwingine wa muhtasari umetumika katika (uk.25) wakati msimulizi anapotueleza kuwa Munene humwona mwanawe John kama johari adimu; dhahabu aliyoisaka katika machimbo ya majaribio kwa miaka mingi sana. Msimulizi ametumia kauli fupi sana kueleza jinsi Munene alivyochukua muda mrefu katika ndoa akitafuta mtoto wa kiume. Wake zake wa kwanza wawili walijaliwa watoto wa kike; wasichana tu. Munene aliamua kuoia mke wa tatu ambaye angemzalia mvulana.

Msimulizi anatumia kauli fupi mno kama, “majaribio kwa miaka mingi sana” kudhihirisha kipindi kirefu kisichodhihirika wazi. Anaonyesha jinsi ilivyomchukua Munene muda mrefu kupata mtoto wa kiume. Hali hii imetumika kama njia ya kuiharakisha hadithi na kuufanya muda wa usimulizi wa matukio kuwa mfupi.

Kipengele cha muhtasari kimejitokeza wazi katika matukio mbalimbali na ni cha muhimu katika kuharakisha kasi ya hadithi katika riwaya. Msimulizi anapofupisha muda wa hadithi kwa kauli chache huweza kumfanya msomaji kuelewa hadithi kwa wepesi pasipo kumchosha akili kwa usomaji mwingi.

3.2.3 Onyesho

Onyesho kama anavyoeleza Manfred (2005) ni namna ya usimulizi ambao huleta sifa za uigizaji katika matini ambapo wahusika huonekana wakizungumza mbele ya wasomaji wa kazi hiyo. Kigezo hiki hudhihirika zaidi katika matumizi ya usemi halisi hasa katika dayalojia au pengine wakati maneno ya wahusika yanapohusishwa moja kwa moja katika simulizi.

Maneno ya wahusika yanapohusishwa moja kwa moja katika simulizi, hisia zao huwekwa wazi mbele za wasomaji na huonyesha mtazamo wao kuhusiana na maisha katika mazingira waliomo kama asemavyo Kenan (2003). Hali hii huibua utegemevu unaomfanya msimulizi aweze kuaminiwa katika usimulizi wake na mtazamo wake. Maneno ya wahusika huingizwa baina ya sehemu za simulizi ambapo wanaonekana wakishiriki katika mazungumzo mbalimbali. Katika riwaya, msimulizi amehusisha mazungumzo kati ya Lila na babu yake ifuatavyo:

“Mwanangu, huyu kijana atakupeleka utakakompata kijana wa kazi!”

“Mimi nafuatia mambo huko kwenye mlima wa Nzamba...”

“Babu, unajua nini?”

“Niambie, Lila wangu!”

“Tulipokuwa watoto tuliuita mlima wa Mwanamke.”

“Nyie ndio mliojua; yupo mwanamke maarufu aliyeishi huko zama za Wazungu...”(uk.21)

Mazungumzo haya yanatokea wakati msimulizi anapomtembelea babu yake kwake nyumbani. Alimtaka babuye amtafutie kijana wa kazi kisha amsaidie kutafuta mazingira alimofia na kuzikwa babake mzazi. Mbulu alimpa Lila

kijana wake wa kazi ili amsaidie kutekeleza shughuli hizo kwani yeye alikuwa anaelekea katika mlima wa Nzamba kutoa kafara katika madhabahu ya kabila lake.

Mazungumzo haya yanamfanya msomaji kupata ufahamu kuhusu uhusiano uliopo baina ya wahusika hawa wawili. Msimulizi anajiweka mbele ya wasomaji huku akishiriki katika mazungumzo ya moja kwa moja na babu yake. Hali hii inadhihirisha mazungumzo ya kidrama yanayosababisha kuwepo kwa matini ndefu. Mazungumzo ya aina hii yamesababisha muda wa usimulizi wa hadithi kuwa mrefu zaidi. Kenan (2003) anaeleza kuwa mazungumzo baina ya wahusika humfanya msomaji kumwamini na kumtegemea msimulizi katika usimulizi wake kwani huuona kama kwamba ni wa ukweli.

Mfano mwingine wa onyesho unadhiririka katika (uk.88) ambapo Munene na mkewe Deborah wanapogombana hasa baada ya mkewe kugundua kulikuwa na mifuko kadhaa ya kondomu kwenye koti la mumewe. Mkewe anamkabili kwa hasira kuu lakini Munene anazua mazungumzo haya:

“Huyo hakuwa mwanamke, namna gani wewe? Miaka hii yote tuliyoishi hujanjua”
“Basi nani?”
“Waziri, alaa vipi wewe!”
“Si ana nyumba huko jijini?”
“Basi mbona mkalale hotelini?”
“Tulitaka nafasi na muda mzuri wa kuizungumzia mipango yetu.”
“Mbona jina lake halikuandikwa hapa...”
(uk.88)

Mazungumzo haya yanadhihirisha wazi mgogoro uliopo katika ndoa baina ya Munene na mkewe Deborah. Suala la kukosa uaminifu katika ndoa

linaonyeshwa kupitia kwa matendo ya Munene ya uzinifu. Kitendo hiki kinamkera mkewe na kumfanya aonyeshe hisia zake wazi. Katika sehemu hii, kinachosemwa kinaigizwa kwa wasomaji na hivyo kuibua fikra kuwa msomaji anayaona na kuyasikia yale yanayotendeka au kusemwa na wahusika. Onyesho hutekeleza majukumu sawa na yale ya dayolojia na huwa ni fupi ikilinganishwa na simulizi yenyewe.

Mbali na kuonyesha mtazamo wa wahusika na imani zao, dayalojia huweka wazi migogoro na mivutano ya wahusika kuhusiana na maisha yao katika mazingira wanamoishi. Katika dayolojia uwepo wa msimulizi huweza kuondoka ili kuwapa nafasi wahusika mbalimbali kushiriki katika mazungumzo bila hata kutoa maelekezo ya mazungumzo hayo kama anavyodokeza Bonheim (1982). Hali hii huzua taharuki kwa msomaji kuhusiana na matukio mbalimbali. Mazungumzo haya yanadhihirika wazi baina ya Munene na mkewe Katumbi katika (uk.39) Munene anatanguliza mazungumzo kwa kumwambia mkewe:

“Unazaa wasichana kisha unasema hivi?”
“Nazaa wasichana tu. Ehh, au ni kusema hujui?”
“Uwezo wa kuamua nitazaa mvulana au la sino mimi;ni kusema hukusoma habari ya X na Y wewe?”
“Kofi au nini huyo mtoto mwingine sizai; mimi sio kiwanda.”(uk.39)

Dayolojia hii inaweka wazi mivutano baina ya Munene na Katumbi na kuonyesha hisia zao kuhusu suala la kuzaa mvulana. Munene anamlaumu Katumbi kwa kuzaa wasichana tu. Maneno yanayotumika baina yao ni ya

kukera. Mvutano huu unamfanya Munene aamue kumzaba mkewe kofi kali, naye mkewe anaapa kwamba hatazaa mtoto mwingine. Hapa msimulizi amewaacha wahusika wake wasemezane wenyewe kwa wenyewe bila kuingilia kati au kutoa ufafanuzi kuhusu mazungumzo yao. Hali hii inamfanya msomaji kujihusisha na hisia za wahusika moja kwa moja.

Sura hii inadhihirisha kuwa kipengele cha onyesho kimetumika katika sehemu mbalimbali ya riwaya. Wahusika wamedhihirika wakishiriki katika mazungumzo mbalimbali. Maneno na hisia zao yamehusishwa moja kwa moja mbele ya msomaji, hali inayomfanya kuwa na hisia za furaha au chuki kuhusu matukio mbalimbali.

Imebainika kuwa dayolojia itumikapo hufupisha masafa ya kiuajumi baina ya msomaji na ulimwengu wa hadithi. Hivi ni kusema kwamba mazungumzo ya wahusika humleta msomaji karibu na matukio yanayosimuliwa. Ingawa hivyo matumizi mapana ya maonyesho huenda ikasababisha (ingawa si lazima) kuwepo na matini ndefu kama anavyodokeza Bonheim (1982) hali inayoweza kuongeza muda wa usomaji hadithi kwa msomaji.

3.2.4 Udondoshi

Kulingana na Chatman (1978:70) udondoshi ni kigezo cha muda kinachorejelea pale ambapo sehemu fulani ya hadithi imeachwa nje bila kuelezewa. Wananadharia wengine kama Gennette (1980:93-95) na Toolan (1988:56) wanauchukulia udondoshi kama njia mahsusi ya kasi au uharakishaji wa hadithi ambapo wakati matini husitishwa na muda wa kusimulia hadithi huweza kuendelea. Mifano kama hii inadhihirishwa katika sehemu mbalimbali

katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Msimulizi katika (uk.270) anatueleza jinsi alivyosikia habari kuhusu kifo cha Munene ingawa kifo chake hakikuwa kimetajwa wala kuelezewa katika simulizi. Anatueleza ifuatavyo:

Siku mbili kabla ya kuondoka kwake kwenda masomoni Ufaransa, Yunga alinipitia nyumbani. Tulikuwa na mengi ya kuzungumza na siku hiyo ndipo niligundua kuwa Munene alikuwa amefariki dunia (uk.270)

Msimulizi anaonyesha kuwa ilikuwa mara yake ya kwanza kupata ujumbe kuhusu kifo cha Munene. Lila alipashwa ujumbe huo na Yungi wakati alipompitia kwao nyumbani kabla ya kwenda masomoni Ufaransa. Hivyo msimulizi anataja tu kuhusu kifo cha Munene lakini hajatuonyesha kuugua kwake wala kilichosababisha kifo chake. Sehemu hiyo imedondoshwa katika simulizi. Msimulizi pia anatoa taarifa ambayo haikuwa imesikika wala kusimuliwa hapo awali kumhusu kijana Yungi Mwamba. Anaeleza kuwa:

Niligundua jambo jingine linaloutia moyo mavune. Yungi alikuwa mtoto wa Munene kutokana na mimba ya mamake, aliponajisiwa na Munene akiwa msichana mdogo (uk.70)

Maelezo haya yanadhihirisha wazi kuwa msimulizi hakuwa amepata habari kuwa Yungi alikuwa mwana wa Munene. Hatujaonyeshwa kuzaliwa kwa Yungi na maisha yake ya utotoni pamoja na elimu yake. Msimulizi anataja kuhusu masomo ya Yungi anapotueleza tu kuhusu kuonana kwao naye alipokuwa akienda Ufaransa kusoma. Msimulizi alikuwa ametutajia mwanzoni tu jinsi mamake Yungi alivyonajisiwa na Munene katika kipindi cha sherehe za uhuru lakini hakutuonyesha matokeo ya unajisi huo. Anaeleza kuwa:

Munene alikirudia kitendo alichokitenda
akiwa mwanafunzi na kuhongerwa na babake,
akampiga miereka kiumbe aliyekuwa akitoa
usiahi; akamtia goe huku anamzomea...
(uk.12)

Msimulizi hajaonyesha wazi kitendo alichotenda Munene. Isitoshe hajasimulia kuhusu mhusika aliyeathiriwa na kitendo cha unajisi. Sehemu hiyo yote imedondoshwa katika simulizi hali inayoleta taharuki inayomfanya msomaji kuwa na hamu ya kuendelea kusoma ili kupata ufahamu kuhusu mhusika aliyetendewa kitendo hicho pamoja na athari zake.

Kutokana na maelezo haya imedhihirika wazi kuwa udondoshi ni hali mahsusi ya kuongezeka kwa kasi ya wakati au njia ya kuharakisha uendelezaji wa hadithi. Udondoshi umetumika katika sehemu mbalimbali katika riwaya teule kama njia ya kuharakisha kasi ya hadithi. Mbinu hii inapotumika huweza kumwacha msomaji katika hali ya taharuki. Humchochea aendeleo kusoma zaidi ili aweze kupata ufahamu wa kitakachotokea katika maisha ya mhusika anayesawiriwa katika simulizi.

3.2.5 Maoni ya Msimulizi

Maoni ya msimulizi kama asemavyo Bonheim (1982:30-32) ni hali ambapo msimulizi anasitisha usimulizi wa hadithi ili kuyapa nafasi maelezo kuhusu sifa za wahusika, uendelezaji wa matukio na hali ya kitendo cha usimuliaji. Anasema maoni ni kigezo kinachohusiana moja kwa moja na mtuo ambacho kinahusu upenyezi wa msimulizi anapositisha usimuliiaji ili kutoa maoni au maelezo ya ziada kuhusu hadithi. Hali hii husababisha mwendo wa kusimulia hadithi kuwa mrefu zaidi na hivyo kuchelewesha uendelezaji wa hadithi.

Mfano huu unadhihirika wazi katika (uk.55) Munene akiwa katika ulimwengu wa ndoto. Msimulizi anatueleza kuwa:

Alisikia sauti ya kicheko kikitokea kwenye kisogo chake, alipogeuka alishtukia amesimamiwa na jitu lisilokuwa na uso. Lile jitu lilitokomea na kumwacha akitiririkwa na jasho...(uk.56)

Munene alikuwa amelala na ghafla akazama kwenye ulimwengu wa ndoto. Ghafla alisikia kicheko kikitoka kwenye kisogo chake na alipogeuka alitambua kuwa alikuwa amesimamiwa na jitu ambalo lilitokomea baada ya muda na kuamwacha akitokwa na jasho. Msimulizi anapomhusisha Munene katika ndoto akiwa usingizini hatendi lolote, hali inayoifanya hadithi kutosonga mbele katika muktadha wa mahali na wakati. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa wakati matini ni mrefu ilhali wakati hadithi ni mfupi.

Mfano mwingine wa ndoto za wahusika unajitokeza katika (uk.99) Lila anaposhikwa na usingizi mzito akiwa kwao nyumbani K'tambasye. Anaota amekabiliwa na jitu kubwa lililoshika jisu kubwa mkononi. Anasikia sauti nyingi za kike nyuma ya hilo janaume na vigelegele vinavyofuatwa na ngoma za kitamaduni. Ghafla anasikia kicheko cha wanaume kinachoandamana na vilio vya wasichana na wanawake wachanga. Lile jitu linamrushia jisu lakini kwa bahati nzuri linasaki ukutani karibu na mahali anapolala. Baada ya tukio hilo, msimulizi anatulizwa na sauti inayofanana na ya babu yake Mzee Mbulu inayosikika ikisema:

Usiwe na hofu nilikwambia umeanza safari.
Utangamano hauji bila ya utengano. Kuteng-

ana kunazaa kwa uchungu mkali kama wa mtu
anayekata roho... (uk.99)

Lila anapolala na kuota ndoto hatendi lolote. Hivyo, hadithi inayosimuliwa haiendelei mbele hali inayosababisha wakati matini kuwa mrefu na wakati hadithi kuwa mfupi. Ndoto hii inadhihirisha wazi mapambano kati ya wanawake na wanaume katika jamii husika. Hii ni jamii ambapo mwanamke amedunishwa. Wanawake wanaonwa kuwa duni na ambao hawapaswi kujiingiza katika masuala ya kisiasa. Wanaume wanawaandama kwa kila njia ili kuwakomesha wasizinduke na kuzitetea haki zao.

Upenyenzi wa kisimulizi unaweza kujitokeza katika mbinu rejeshi. Katika (uk.126) msimulizi anaturudisha katika matukio ya wakati uliopita. Anaonyesha Kasina akikumbuka jinsi zamani walivyokuwa wakilaani jogoo aliyewika alfajiri kuyatangaza macheo ya siku nyingine wakiwa bado wamekumbatiana, huku kasina ameulalia mkono wa mumewe. Aliendelea kukumbuka siku walipokuwa wakitembea pamoja huku mumewe akiwa amemshikia mwavuli mkubwa kuzuia mianzi ya jua isiathiri urembo wake.

Mawazo haya yanatokea baada ya Kasina kutengana na mumewe hali iliyoyafanya maisha kumtumbukia nyongo. Msimulizi anaturudisha nyuma hasa baada ya Munene kwenda kwa kasina nyumbani na kumzaba makofi kwa kisingizio kuwa alikosa kuwafunza wanawe adabu. Wanza alikuwa amemtusi babake siku hiyo asubuhi. Maelezo haya yanarudisha hadithi nyuma badala ya kuiendeleza mbele kiwakati sawia na ndoto za wahusika.

Maoni ya msimulizi vilevile yanadhihirika wakati msimulizi anapositisha usimulizi wa hadithi ili kuangazia tabia na hisia za wahusika wake. Katika (uk.50) msimulizi anaacha kusimulia kisa kuhusu dhiki alizopitia Katumbi baada ya kupewa talaka na mumewe na kuanza kuangazia kuhusu sifa zake Katumbi. Anasema:

Katumbi ni mwanamke mwenye urazini
mkubwa; huyapima na kuyakadiria mambo
kwa kiasi kikubwa; huyachuja maneno kabla
ya kutamka. Lakini... hupandwa na hasira
kama mtu aliyeumwa na nyoka...(uk.50)

Katika sehemu hii msimulizi amesitisha hadithi ili kuyapa nafasi maelezo kuhusu sifa za mhusika wake. Anaeleza kuwa Katumbi ni mwanamke anayechuja na kupima maneno kabla ya kuyasema. Mbali na kuwa na hekima, anasema kuwa ana hasira za ajabu. Maelezo kuhusu sifa za Katumbi hayaendelezi hadithi mbele kiwakati na kimuktadha. Wakati matini ni mrefu (msomaji anaendelea kusoma) ilhali wakati-hadithi ni mfupi (Katumbi hatendi lolote hivyo hadithi haisongi mbele).

Ni dhahiri kuwa matumizi mbalimbali ya mbinu ya maoni ya msimulizi yanaufanya muda wa kusimulia hadithi kuongezeka. Hata hivyo kigezo hiki ni muhimu kwani humfanya msomaji kupata ufahamu zaidi kuhusu tabia za wahusika mbalimbali. Baada ya kutathmini matumizi ya kigezo cha muda, sehemu hii ilichanganua kipengele cha idadi ya utokeaji wa matukio na kuonyesha nafasi yake katika usimulizi wa riwaya.

3.3 Idadi ya Utokeaji wa Matukio

Toolan (1988:61) anaeleza kuwa hiki ni kipengele cha wakati kinachorejelea uhusiano kati ya idadi ya utokeaji wa matukio katika hadithi (matukio yanatokea mara ngapi) na ni mara ngapi ambapo matukio hayo yanasimuliwa au kutajwa katika matini. Kulingana na Kenan (1983:56-58) si lazima miundo ya sentensi na maneno yafanane tukio linaposimuliwa mara kadha kwa sababu muktadha au hata mahali tukio hilo linapotokea huwa tofauti. Kigezo hiki kinaweza kuainishwa kwa jinsi tatu kama; usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu kama inavyojitokeza hapa chini.

3.3.1 Usimulizi Mosi

Ni aina ya usimulizi ambapo tukio linaweza kutokea mara moja na kusimuliwa mara moja katika hadithi kama asemavyo Toolan (1988:61). Mfano huu unapatikana (uk.11) msimulizi anaposimulia kisa kuhusu jinsi Kivu alivyoendelea kuliendesha baiskeli lake karibu na mahali palipokuwa na vifaru hata baada kuonywa na wanakijiji dhidi ya kufanya hivyo. Alikaidi ushauri aliokuwa amepewa na wanakijiji, hali iliyomfanya kuvamiwa na vifaru hao na kuuawa. Msimilizi anatoa maelezo ifuatavyo kuhusu kifo cha Kivu: Anaeleza:

Akaipiga malapa baiskeli yake, akapita
karibu na vifaru akaivurumisha baiskeli yake;
kifaru mmoja akamwandama; akakizika kipusa
chake kwenye mbavu zake. Akafa shujaa
(uk.11)

Muktadha huu unaonyesha kitendo cha Kivu cha kuendesha baiskeli karibu na vifaru hata baada ya kuonywa na wanakijiji wenzake kwamba angeyahatarisha maisha yake. Tukio la Kivu la kuendesha baiskeli karibu na walipokuwa vifaru

limetendeka mara moja na kusimuliwa mara moja na wala halijasimuliwa tena katika simulizi. Mfano mwingine unadhihirika wakati mzee Mbulu anapomweleza Lila kuwa kaburi la babake lilikuwa limefukuliwa na kichwa chake kukosekana. Anasema yafuatayo:

Tulitambua kuwa lilikuwa limefukuliwa.
Ilibidi tufanye tambiko alikokuwa amelala
lakini kichwa chake hakikuwepo! Hii ilikuwa
mara ya kwanza kusikia kuwa kaburi
limefukuliwa (uk. 105).

Tukio la kufukuliwa kwa kaburi la babake Lila na kichwa chake kutoweka lilifanyika mara moja kisha likasimuliwa mara moja na mzee Mbulu. Jambo hili linamshangaza Lila kwani ndio mara yake ya kwanza kusikia kuwa kaburi la babake marehemu lilikuwa limefukuliwa. Mifano iliyo hapa juu inadhihirisha wazi kuwa tukio linaweza kutokea mara moja na kusimuliwa mara moja pasipo kulisimulia tukio lilo hilo tena katika simulizi.

3.3.2 Usimulizi Rudufu

Kwa mujibu wa Kenan (1983:46) usimulizi rudufu ni aina ya usimulizi ambapo tukio linaweza kufanyika mara moja na likasimuliwa mara kadha katika simulizi. Anasema kuwa tukio linaposimuliwa zaidi ya mara moja si lazima miundo ya kileksia na kisintaksia ifanane. Sentensi na maneno yanaweza kubadilika kwa sababu tukio linaporudiwa huwa linarudiwa katika muktadha tofauti na uliyotangulia kama anavyosema Toolan (1988:62). Mfano kama huu unajitokeza katika riwaya husika (uk.10). Suala la Munene la kuyanyonya maziwa ya mamake akiwa mfu linafanyika mara moja na kusimuliwa zaidi ya mara moja. Msimulizi anasema:

Mamake Munene alifariki usiku kabla ya majira ya wachawi; watu walifika chumbani asubuhi, walimkuta kifuani pa mamake alikochezea, akinyonya maziwa ya mamake aliyekuwa mfu tayari.(uk.10)

Tukio hili ambapo Munene alipatikana akiyanyonya maziwa ya mamake akiwa mfu lilitendeka na likasimuliwa zaidi ya mara moja. Katika (uk.11) mwandishi anatueleza ifuatayo kuhusu Munene:

Na iweje asiwe shujaa kama kitendo kipi kingine cha kishujaa kuliko kunyonya maziwa ya mfu; kuyakamua maziwa kwenye mwili uliotiwa ganzi na mauti... (uk.11)

Tukio la Munene la kunyonya maziwa ya mamake akiwa mfu limerudiwa mara ya pili. Msimulizi anataja kitendo cha unyonyaji maziwa ya mfu kuwa cha kishujaa. Ingawa tukio lile lile limesimuliwa mara ya pili, tofauti iliyopo ni kuwa muktadha wa matukio na muundo wa sentensi ni tofauti. Mfano mwingine unajitokeza katika (uk.54) msimulizi anapoeleza ifuatavyo kuhusu Munene:

Si anajihesabu jasiri tangu hapo aliponyonya maziwa ya mamake mfu? Lakini mambo yalikuwa yamemharibikia... (uk.54)

Kauli, ‘kunyonya maziwa ya mamake mfu’ imetumiwa kuonyesha tukio hili la kunyonya maziwa ya mama mfu lilitokea mara moja na kusimuliwa mara nyingi. Hapo awali Munene alikuwa na ujasiri wa kupambana na mkewe lakini mambo yameanza kwenda mrama. Maneno haya yametumika kama kejeli kwa vile ujasiri wake umegeuka kuwa woga. Kila alalapo hujiwa na ndoto ya kutisha inayomwacha akitetemeka na kutiririkwa na michirizi ya majasho kinyume na matarajio yake kama shujaa aliyenyonya maziwa ya mfu.

Ingawa tukio la Munene la kuyanyonya maziwa ya mama akiwa mfu limesimuliwa tena, tofauti iliyopo ni kuwa muundo wa maneno umebadilika na matukio haya yametokea katika muktadha tofauti na ule wa kwanza. Kulingana na Toolan (1988), tukio linaweza kutokea mara nyingi katika hadithi kisha likasimuliwa mara kadhaa. Tukio moja linapotokea mara nyingi na kusimuliwa mara kadhaa, miundo ya sentensi au maneno yanayotumika huweza kubadilika. Hii ni kwa sababu tukio hilo linaporudiwa kusimuliwa, huwa linatokea katika muktadha tofauti na ule wa awali.

Tukio la wahusika la kujiuma kidomo limetokea mara nyingi na likasimuliwa mara kadhaa katika simulizi. Katika (uk.84) Munene anadhihirika akiuma mdomo wake wa chini alipokuwa akiliendesha gari lake akielekea mjini. Msimulizi anasema kuwa:

Alivuta tabasamu, akauma mdomo wa chini,
akabadilisha gia na kukanyaga mafuta kwa
nguvu. Gari hilo lilimwitikia kwa sauti na
kuongeza kasi yake ya kuikunja barabara
...(uk. 84)

Munene anadhihirika akiuma mdomo zaidi ya mara moja katika simulizi na hali hii ikasimuliwa mara kadhaa katika miktadha mbalimbali. Katika dondoo hii Munene anadhihirika akiuma mdomo kama ishara ya furaha. Alifurahi kwa vile alikuwa akielekea mjini kukutana na inspekta wa polisi ambaye angemsaidia kusuluhisha matatizo yaliyomkabili kuhusu suala la ufisadi. Munene na wanasiasa wenzake walikuwa wamehusika katika kashfa ya ufisadi jijini Kitambasye. Kutokana na hali hii Waziri Kisingo alikuwa anataka wakutane ili amtambulishie Munene kwa inspekta ambaye angemsaidia katika

kuwakomesha waandishi wa habari waliokuwa wamechapisha habari hiyo kwenye gazeti.

Suala hili la kuuma mdomo wa chini linatokea tena katika (uk.134), Munene akiwa katika njia kuu kuelekea mjini kukutana na rafiki yake wa kike, Jessica. Magari yaliyokuwa mbele yake hayakuwa yanasonga, hali iliyomfanya achoshwe na uvutaji mwingi wa moshi uliotokana na magari barabarani. Msimulizi anatumia kuwa:

Munene aliishiwa na subira Akaiuma
midomo, akalaani...pumzi ilimtoka njia
mbilimbili (uk. 134)

Munene anauma midomo tena kama ishara ya hasira kinyume na hapo mbeleni. Amekosa subira kutokana na msongamano wa magari uliofanya achelewe kwenda kukutana na mpenziwe Jessica. Hali hii inamfanya akose kukutana na mpenzi wake Jessica kwa wakati waliokuwa wamekubaliana. Ingawa tukio hili limerudiwa, miundo ya maneno ni tofauti. Hapa msimulizi anaeleza kuwa Munene anaiuma midomo tu bila kutaja sehemu ya mdomo inayoumwa. Katika tukio la awali Munene anadhihirika akiuma mdomo wa chini. Hivyo maneno mengine hayajahusishwa katika muktadha huu. Na kama Kenan (2003) asemavyo, si lazima miundo au maneno yote yawe sawa tukio linaporudiwa katika hadithi.

Suala la kuuma mdomo wa chini limehusishwa na wahusika wengine tofauti na wale waliotajwa awali. Debora, mkewe Munene anadhihirika akijiuma kidomo chake katika (uk.169). Kitendo hiki kimerudiwa ingawa miundo ya maneno ni tofauti na muktadha uliotangulia. Msimulizi amehusisha kiambishi 'ki' cha

kuonyesha hali ya udogo. Kwa mfano, anasema Debora *'alikiuma kidomo'* badala ya kuhusisha maneno katika hali ya wastani kama vile, *'akauma mdomo.'* Kitendo hicho kinatokana na hali ya uchovu na machungu aliyokuwa nayo moyoni baada ya Mumewe kumpuza baada ya kujifungua mtoto wa kike.

Debora alikiuma kidomo chake alipokuwa amesimama kando ya njia akiwa amembeba mwanawe mchanga akisubiri kuabiri gari aelekee nyumbani. Mumewe alikuwa ametokomea na hakurudi hospitalini baada ya kupata habari kuwa mkewe alikuwa amejifungua mtoto wa kike.

Kitendo cha kuuma midomo kinaonekana tena wakati Lila ambaye ni mwandishi wa habari katika gazeti la Mpapure anatekwa nyara na watu wasiojulikana. Lila alikuwa na mwanahabari mwenzake Derby alipofungwa macho kwa vitambara na kupelekwa mahali kusikojulikana. Hali hiyo ilimfanya Lila akumbuke maneno ya babu yake akimwambia kuwa, alikuwa ameanza safari inayoingia kwenye msitu, lakini upande wa pili ulikuwa na mwanga, hivyo aendelee na safari wala asirudi nyuma. Lila anaeleza ifuatavyo:

Ndiyo nyuma singeweza kurudi, nyuma
hatungeweza kurudi... nilikiuma kidomo
cha chini na kukibiginya kiganja cha mkono
wa Derby. Naye akanibiginya pia (uk. 190)

Lila alijiima kidomo kutokana na hofu na hasira aliyokuwa nayo baada ya kutekwa nyara na watu wasiojulikana na kuingizwa katika gari aina ya Landrover. Mfano huu unadhihirisha kwamba tukio linaporudiwa maneno

yaliyotumika yanaweza kuwa sawa au yabadilike kulingana na muktadha uliopo.

Uchanganuzi huu ulibainisha kuwa matukio yanapotokea na kusimuliwa zaidi ya mara moja si lazima maneno yaliyotumika katika muktadha wa awali yafanane na mengine yanayotokea baadaye. Ni dhahiri kuwa uhusiano kati ya matukio na usimulizi wa miktadha yameonekana wazi katika hadithi.

3.3.3 Usimulizi Banifu

Hiki ni kigezo cha idadi marudio kinachoonyesha kuwa tukio linaweza kutokea mara kadha na likasimuliwa mara moja kama anavyodokeza Levesque (2006). Tukio linalosimuliwa huwa limefanyika mara nyingi kisha mara zote zile zikabanwa kwa maneno machache na kusimuliwa mara moja tu. Lila anatueleza jinsi alivyoutazama ule mlima wa mwanamke akiwa safarini kuelekea kwa mzee Mbulu. Anasema hivi:

Niliuangalia ule mlima tena na kuyakumbuka
yale machozi niliyoyaona siku ile. Machozi
ya mlima wa mwanamke. Machozi ya
mwanamke... (uk.18)

Lila alikuwa ameutazama mlima huo mara nyingine katika harakati zake za kumtembelea babu yake. Kwa hivyo alikuwa ameutazama mara ya pili. Marudio ya usimuliaji wa tukio hilo yanaonyeshwa kupitia kwa matumizi ya kauli; ‘niliuangalia mlima tena’ Mfano mwingine unajitokeza wakati Lila anapoketi na Derby ambaye ni mfanyikazi mwenzake katika hoteli ya Minar. Msimulizi anatueleza ifuatavyo:

Nilipoishia kwenda Minar nilikuwa na Derby na mara zote zilifanana. Kulikuwa kumetokea jambo fulani lililomvutia hapo. Alisema mandhari ya ndani ya hoteli hiyo yalimpumbaza...(uk 86)

Maelezo ya msimulizi yanadhihirisha wazi kuwa hiyo haikuwa mara ya kwanza kwao kupazuru mahali hapo. Maneno ‘mara zote zilifanana’ yanatumika kudhihirisha kuwa tukio la kwenda katika hoteli ya minar lilifanyika mara kadha lakini msimulizi anasimulia matukio hayo yote mara moja. Kutokana na maneno ya msimulizi, mandhari ya ndani ya hoteli hiyo yalimpumbaza na kumtuliza moyo Derby hata akasahau yote yaliyokuwa yamemkera.

Hivyo maelezo ya Kenan (2003) kwamba tukio linaweza kutokea mara nyingi na kusimuliwa mara moja yanadhihirika wazi katika riwaya teule. Usimulizi huu ni muhimu sana katika ufupishaji wa matukio kwani huweza kuufanya muda wa usimuliaji uwe mfupi na muda wa usomaji wa hadithi upungue. Mfano mwingine wa tukio kutokea mara kadha na kusimuliwa mara moja unajitokeza tena msimulizi anapofika nyumbani kwa babu yake. Msimulizi anaeleza jinsi babu yake alivyomwangukia mara kadhaa alipowasili pale kwake nyumbani. Anaeleza:

Aliniangalia tena. Alimwinyamwinya midomo yake na kuuliza, “Huyu ni nani anayefanana na mtu nimjuaye?” Hili lilikuwa ni swali la kawaida la babu siku hizo. (uk.19)

Kitendo cha babu cha kumwangukia Lila kilitokea zaidi ya mara moja na hali hii inadhihirika wazi kutokana na matumizi ya maneno, ‘aliniangalia tena’.

Hivyo tukio hilo limetokea mara kadha na kusimuliwa mara moja. Mfano mwingine unajitokeza katika (uk.19) aya inayofuata msimulizi anapoeleza jinsi babu yake alivyomtazama mara nyingine pale kwake nyumbani. Anasema:

Aliniangalia tena, akapinda kichwa, akakaza
macho hata nikatamani kucheka. Akasema,
“Sura inanicheza lakini sauti inanikumbusha
mjukuu wangu niliyemwita Lila...”(uk.19)

Babu anamtazama Lila zaidi ya mara moja na matukio hayo yanasimuliwa mara moja. Hivyo hali ya matukio kutokea mara kadhaa na kusimuliwa mara moja limedhihirishwa kwa njia mbalimbali katika kufupisha na kukuza wa ujumbe wa mwandishi kama ilivyosemwa awali.

Sehemu hii inadhihirisha kuwa msimulizi anasimulia matukio mara moja ingawa matukio hayo yalitokea mara nyingi. Badala ya kusimulia matukio hayo kila mara, anayafumbata katika visa fulani kwa njia inayomfanya msomaji aelewe kuwa matukio hayo yalijiri muda baada ya muda au siku baada ya siku kama anavyoeleza Kenan (1983:46)

3.4 Kiishilio

Sura hii ilichanganua nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya kwa kuzingatia mpangilio wa matukio, muda wa matukio na idadi ya utokeaji wa matukio hayo. Sura ililenga kubainisha iwapo matukio yamesimuliwa kwa kuzingatia mpangilio wa matukio au yamekiuka kaida ya mpangilio huo.; kudhihirisha iwapo mwendo wa wakati wa usimuliaji hadithi umeharakishwa au umepunguzwa katika simulizi. Ilibainika kuwa riwaya imehusisha mbinu rejeshi na elekezi katika uwasilishaji wa matukio. Imedhihirika kuwa baadhi

ya matukio yametokea mara moja kisha yakasimuliwa mara kadhaa, mengine yakatokea mara nyingi na yakasimuliwa mara moja au zaidi. Iidhihirika kuwa matukio yanaposimuliwa zaidi ya mara moja si lazima sentensi na maneno yanayotumika yafanane kwani mahali na muktadha wa matukio yanabadilika. Sura inayofuata ilichanganua kipengele cha uwasilishaji wa usemi na fikra na kuonyesha jinsi kinavyotumika katika riwaya teule.

SURA YA NNE
UWASILISHAJI WA USEMI NA FIKRA ZA WAHUSIKA KATIKA
UENDELEZAJI WA RIWAYA YA DHARAU YA INI

4.0 Utangulizi

Sura hii ililenga kuchanganua uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), mtindo unaotumika kuwasilisha usemi wa wahusika ndiyo unaotumika kuwasilisha fikra zao. Wanatoa madai kuwa mbinu hizi zinapotumika huweza kuibua mifumo mingine ya usemi na fikra kama vile; usemi halisi huru, usemi taarifa huru, fikra halisi huru na fikra taarifa huru katika uwasilishaji wa ujumbe. Sehemu hii ilinua kubainisha aina mbalimbali za usemi na fikra za wahusika; kuonyesha iwapo njia zinazotumika kuwasilisha usemi wa wahusika ni sawa na za kuonyesha fikra zao pamoja na kudhihirisha iwapo matumizi ya usemi na fikra ni njia mwafaka anayoweza kutumia msimulizi katika kubadili mitazamo ya usimulizi.

4.1 Uwasilishaji wa Usemi wa Wahusika

Kwa mujibu wa Leech na Short (1981) Usemi wa masimulizi ni yale yanayosemwa na wahusika mbalimbali katika simulizi. Naye Wamitila (2003) anafafanua usemi kama tamko ambalo lina msemaji na msemzwa na huhusisha mbinu mbalimbali za matamko kama sehemu ya shughuli za kijamii. Wahakiki hawa wanakubaliana kuwa wahusika katika hadithi aghalabu huzungumza kwa kuhusisha usemi halisi ambapo viwakilishi vya nafsi ya kwanza hutumika. Vilevile mwandishi anaweza kuwasilisha unenaji katika usemi wa taarifa kwa kuhusisha viwakilishi vya nafsi ya tatu. Mwandishi wa

riwaya aghalabu hutumia usemi halisi sawia na usemi wa taarifa ambapo anabadili kutoka usimulizi mmoja hadi mwingine kama anavyodokeza Barry (1995). Sehemu hii ilibainisha uwasilishaji wa usemi na fikra mbalimbali za wahusika na kuonyesha matumizi yake katika uendelezaji wa hadithi.

4.1.1 Usemi Halisi

Usemi halisi kama anavyoeleza Manfred (1995) ni maneno yanayosemwa na mhusika katika simulizi na huweza kunukuliwa moja kwa moja kama yalivyotamkwa. Matamshi haya huweza kufungiwa katika alama za mtajo kisha hufuatwa na ushawishi kuonyesha ni nani aliyeyasema. Wahusika katika hadithi huzungumza na katika kufanya hivyo hujihusisha katika usemi halisi ambapo viwakilishi vya nafsi ya kwanza hutumika. Anasema kuwa matumizi ya usemi halisi ni ushahidi wa kuwepo kwa msimulizi karibu na wahusika wanaozungumza katika simulizi.

Mwandishi anapowasilisha usemi taarifa, maneno hayatolewi moja kwa moja kama yalivyosemwa, badala yake yanaripotiwa na msimulizi wa nafsi ya tatu kama anavyoeleza Short (1991). Hali hii humfanya msomaji kuyaona matukio yanayosimuliwa kwa mbali. Anafafanua kuwa mahali na wakati wa matukio katika usemi taarifa ni tofauti na ilivyo katika usemi halisi kwa jinsi ambavyo vionyeshi, viambishi vya wakati na vielezi vya mahali vinavyobadilika. Mifano ya usemi halisi inajitokeza wazi katika riwaya teule (uk.23) wakati mzee Mbulu anapolisimamisha gari la Munene alipokuwa akielekea kwake nyumbani. Munene anamwambia mzee Mbulu maneno haya:

“Mzee unapokunywa mapombe yako huko,
maana najua huna uwezo wa kunywa bia ya

kistaarabu usilete ujinga wako njiani. Mzee hiki ni chuma na kama hukijui kiliacha utani kiwandani huko!” Munene akasema (uk.23)

Munene anamzomea mzee Mbulu kwa sababu ya kulisimamisha gari lake alipokuwa akielekea nyumbani na kudai kuwa alitaka kumwona. Munene alichukizwa na kitendo cha Mbulu, hali iliyomfanya amkeme kwa kiburi. Katika muktadha huu sifa zote za usemi halisi zimejitokeza wazi. Alama za mtajo zinaonyesha kwamba kuna unukuzi wa maneno yaliyotamkwa moja kwa moja kutoka kwa mnenaji. Kiashiria ‘hiki’ kinaonyesha uhusiano wa karibu baina ya mnenaji na kinachosimuliwa.

Mwandishi amedhihirisha matumizi mengine mbalimbali ya usemi halisi. Katika (uk.38) wakati Munene anapomtaka Katumbi amzalie mtoto wa kiume wa kumrithi, Katumbi anamjibu hivi:

“Hilo silo suala muhimu maana hutawajengea shule au hospitali yao wenyewe, lazima utawalazimisha wengine kuubeba mzigo huo.”
Akajibu Katumbi. (uk.38)

Munene anamlazimisha mkewe Katumbi kumzalie mtoto wa kiume hali ambayo imepitwa na wakati ilhali alikuwa amemzalie watoto wanne wa kike. Kwake Katumbi, ulimwengu tunamoishi sasa umebadilika na huwezi kupata watoto wengi kama zamani. Naye mumewe anashikilia kuwa, cha muhimu ni kuwa anaweza kuzaa anavyotaka mradi ana uwezo wa kiuchumi na huo anao. Hali hii inazua mvutano katika ndoa yao.

Maneno ya mhusika yamenukuliwa moja kwa moja kama alivyotamka, hivyo kuhusisha alama za mtajo. Vionyeshi bainishi kama ‘hilo’ na ‘huo’ na

viambishi vya wakati vimetumika kuonyesha uhusiano wa karibu kati ya mhusika na kinachozungumziwa. Usemi halisi huchukua mtazamo wa matumizi ya nafsi ya kwanza, hali inayoashiria kuwepo kwa msimulizi karibu na wahusika wanaozungumza.

Usemi halisi unaweza kujitokeza katika uradidi wa maudhui katika hadithi. Mfano huu unajitokeza wakati waziri Kisingo, ambaye ni rafiki mkubwa wa Munene anapomwambia maneno haya:

“Ndugu, njoo uyaonje matunda ya uhuru!
Ukikaakaa na mkeo kila wakati...Kupumbaa
tu! Mwanaume asiyevinjari nje hudhani kaoa
malaika” (uk.82)

Waziri Kisingo anamshauri Munene kuhusu umuhimu wa kwenda kujifurahisha na wanawake wengine badala ya kukaakaa na mkewe kila wakati. Maneno haya yanamfanya Munene kuhisi kuwa ‘dawa ya mke ni kuo mwingine’, hali inayoathiri ndoa yake kwani anaamua kushiriki katika uasherati.

Maneno yanayosemwa na mhusika yamenukuliwa kama alivyoyatamka kwa kuhusisha alama za mtajo. Usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumika katika kudhihirisha kuwepo kwa msimulizi. Alama za uwakifishaji pia zimetumika kama vile vihisishi, hali inayoashiria hisia za mzungumzaji na kuibua sura ya usemi halisi.

4.1.2. Usemi wa Taarifa

Usemi taarifa ni ripoti ya yaliyosemwa hapo awali na mtu mwingine. Kulingana na maelezo ya Manfred (2005:67) mwandishi huwa anatuonyesha

kilichosemwa na mtu mwingine na matokeo ni kuwa baadhi ya maneno katika usemi wa taarifa yanaweza kubadilika. Mabadiliko haya yanaweza kuwa ya kisintaksia na kileksia kama vile, viwakilishi nafsi na vya wakati, vivumishi vionyeshi na hata vielezi vya mahali bila kupotosha maana ya kauli iliyohusika.

Mhusika anayetoa ripoti huweza kuwakilisha iwezekanavyo maneno yaliyosemwa na mhusika. Katika hali hii alama za mtajo huwa haziwekwi na baadhi ya viakifishi kama viulizi na vihusishi havitumiki. Isitoshe nafsi ya tatu huweza kutumika kwa umoja au wingi kama ilivyotajwa hapo awali. Mfano wa usemi wa taarifa unajitokeza katika (uk.38) wakati msimulizi wa nafsi ya tatu anapotueleza kuwa Katumbi:

Aliwazaa watoto watatu juu kwa juu, moja
baada ya mwingine. Munene alikuwa akimsaka
mvulana, Katumbi naye alikataa kushika mimba
ya nne; akagomea kuugeza mwili wake mgodi
wa kuchimba mvulana. (uk.38)

Msimulizi anasimulia kisa kuhusu jinsi Munene alivyokuwa akimshurutisha mkewe Katumbi amzalie mtoto wa kiume hata baada ya majaribio ya muda mrefu.. Katumbi alikataa katakata kuzaa mtoto mwingine kwa kisingizio cha kupata mrithi. Usemi huu unadhihirisha wazi matumizi ya usemi wa taarifa ambapo msimulizi anatoa ripoti kuhusu mhusika wake. Unenaji huu umesimuliwa katika nafsi ya tatu kwa kuhusisha kiambishi ‘a’, na hali ya wakati uliopita inayowakilishwa na kiambishi ‘li’.

Usimulizi huu wa nafsi ya tatu unadhihirisha umbali wa kimasafa baina ya msimulizi, wahusika na matukio anayosimulia. Isitoshe viashiria vibainishi

vya mbali kama ‘huo’ badala ya ‘hoo’ vimetumika kuashiria kuwa msimulizi si mshiriki wa hadithi anayosimulia. Matumizi ya usemi taarifa yanadhihirisha mtazamo wa nje wa usimulizi ambapo anasimulia hadithi bila kushiriki katika matukio hayo. Mfano mwingine wa usemi taarifa unajitokeza katika (uk.91) msimulizi anaposimulia kuwa:

Munene alimtulizia mzee wake macho kisha
akasogea na kumshtukiza King’o kwa mpigo
mkubwa begani, mpigo huo ulifuatiwa na shuti
kali lililompata kwenye kitokono na kumtuma
huko chini. (uk.19)

Munene anampiga King’o bila huruma na kumbwaga chini kwa hasira baada ya kuwaachilia ng’ombe waingie shambani na kula mahindi. Hapa msimulizi anatoa ripoti kuhusu yaliyotokea kwa kutumia nafsi ya tatu. Matumizi ya viambishi vya wakati uliopita vinatumika hali inayodhihirisha umbali wa kimasafa baina ya msimulizi na wahusika katika hadithi. Isitoshe vivumishi vibainishi vya mbali kidogo kama vile ‘huo’ na ‘huko’ vimetumika kudhihirisha usemi wa taarifa. Usimulizi huu huweza kutokea kwa lengo la kusisitiza juu ya tukio au kuonyesha hisia fulani za wahusika au hata kukuza maudhui. Short (1991)

Mbali na usemi halisi na usemi taarifa mwandishi huhusisha mifumo mingine ya semi iliyo huru zaidi kama anavyodokeza Leech na Short (1981). Sehemu inayofuata imeonyesha jinsi vigezo vingine vya usemi vilivyo huru zaidi kama vile usemi halisi huru na usemi taarifa huru vinavyojitokeza katika riwaya ya *Dharau ya Ini*

4.1.3. Usemi Halisi Huru

Kwa mujibu wa Collier (1992) hii ni aina ya usemi halisi ambapo kishazi tangulizi hakitumiki katika unenaji ingawa alama za mtajo huwa zimedumishwa. Kishazi tangulizi kinapoondolewa katika usemi wa wahusika, athari yake huwa ni kuharakisha dayolojia kati ya wahusika, hali inayopunguza muda wa kusimulia hadithi.

Ingawa hivyo, Barry (1995) anatoa madai kuwa usimulizi kama huu unaweza kuzua utata wa kuelewa ni nani anayesema nini kati ya wahusika mbalimbali iwapo kishazi tangulizi hakipo. Anasema kuwa unenaji kama huu huenda ukamfanya msomaji atoe hukumu isiyo sahihi kuhusu yaliosema na wahusika. Hali kama hii inaweza kupotosha ujumbe uliokusudiwa kwa msomaji.

Short (1991) anaeleza kuwa, usemi wa aina hii hutokea katika sentensi ambazo huonyesha kuwa vitendo vya unenaji vimeshafanyika ingawa msimulizi hajishughulishi na kutoa maana ya kilichosemwa. Wahusika huzungumza kwa zamu bila kuonyesha hasa ni nani aliyesema nini. Katika (uk.55) msimulizi anatuonyesha mazungumzo baina ya Munene na pandikizi la jitu lililomkabili chumbani mwake. Jitu linatanguliza mazungumzo na kusema:

‘Usipige hatua yoyote mbele!’

“Una maana gani wewe?”

“Uliposimama ni upeo!”

“Upeo wa nini?”

“Wa maisha yako!” (uk.55).

Munene anakabiliana na jitu hili lenye jinywa kubwa ajabu katika ndoto. Jitu hili linamhusisha katika mazungumzo ya moja kwa moja na zaidi ya hayo,

anasikia sauti ya kicheko na kuingiwa na hofu lakini sehemu nyingine ya mawazo yake inamhimiza awe jasiri hasa anapokumbuka kuwa ana jadi ya ushujaa.

Mazungumzo haya yanachukua sifa za usemi halisi. Msimulizi amedumisha alama za mtajo ingawa kishazi tangulizi kimeondolewa. Ni dhahiri kuwa msimulizi hajashughulika katika kuyafafanua mazungumzo ya wahusika wake. Udondoshaji wa kishazi tangulizi umetumika kama njia ya kuharakisha mazungumzo kati ya wahusika na kuyafanya kuchukua sifa za usemi halisi huru kama anavyodokeza Barry (1995).

Matumizi ya nafsi ya kwanza na viambishi vya wakati uliopo vinatumika kudhihirisha kuwepo kwa msimulizi karibu na wahusika wake. Usemi halisi huru unadhahirika pia katika (uk.88) ambapo Munene na mkewe wanahusika katika ugomvi baada ya mkewe kugundua kulikuwa na mifuko ya kondomu katika mfuko wa koti lake. Hali hii inaendeleza mazungumzo yafuatayo:

“Huyo hakuwa mwanamke; namna gani wewe? ”

“Basi nani?”

“ Waziri, alaa vipi wewe!”

“Si ana nyumba huko kijijini?”

“Basi mbona mkalale hotelini?” (uk.88)

“Tulitaka nafasi ya kuizungumzia mipango yetu.”

Haya ni mazungumzo baina ya Munene na mkewe baada ya Deborah kugundua risiti ya kukodi chumba cha watu wawili kijijini Kitambasye. Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa vitendo vya unenaji vimefanyika lakini msimulizi hajishughulishi na kutoa maana ya kilichosemwa au hata kuyafafanua.

Katika muktadha huu alama za mtajo zimetumika na kishazi tangulizi kimeondolewa hivyo kuharakisha kasi ya hadithi. Mbinu hii ya usemi halisi huru ni muhimu katika kufupisha mazungumzo marefu yasiyokuwa na umuhimu ingawa pia yanaweza kumpotosha msomaji akakosa kubainisha wasemaji na maneno yao ifaavyo. (Leech na Short, 1981).

Mfano mwingine unajitokeza katika (uk.115) wakati Wanza anapomtembelea babake kwao nyumbani asubuhi mapema. Wanza alitaka kujua sababu zilizomfanya mumewe awekwe katika kituo cha polisi. Anasema:

“Nimekuja kukuona unieleze kwa nini umesema mume wangu awekwe kituoni!”

“Kwa nini mume wako yuko kituoni, hakukueleza mumeo huyo?”

“Ehh ulimgeuza mtoto wa kupigwa baada ya ng’ombe wako kula mahindi?”

“Atafungwa...”

“Nani atafungwa?”

“Huyo mzee umwitaye mumeo...!”(uk.115)

Wanza alikuwa amerauka asubuhi mapema na kuenda kwa babake kutaka kujua kilichomfanya ampeleke mumewe katika kituo cha polisi mahali alipolala usiku kucha. Munene alikuwa amempiga King’o vibaya baada ya kugundua alikuwa ameacha ng’ombe waingie shambani na kuyala mahindi. Kipigo hicho kilimkasirisha King’o hali iliyompelekea kulipiza kisasi kwa kumpiga Munene bila huruma hali iliyomfanya Munene kumpeleka King’o katika kituo cha polisi.

Mazungumzo yao yanadhihirisha hali ya kutokuwepo kwa kishazi tangulizi katika hali inayoupa unenaji wao sifa za usemi halisi huru. Alama za mtajo

pamoja na alama za uakifishaji kama vile viulizi na vihisishi vimedumishwa. Mazungumzo haya yanatokea moja kwa moja bila ya msimulizi kuyaingilia wala kujishughulisha kufafanua wanachosema.

Unenaji wa nafsi huru ni muhimu kwa kutoa muhtasari wa mazungumzo marefu yasiyo muhimu na huweza kuchangia katika ufupishwaji wa muda wa kusimulia hadithi kama asemavyo Short (1991). Anasema kuwa mwandishi anapotumia usemi halisi huru, huweza kuwashirikisha wasomaji katika mazungumzo ya wahusika na hisia zao hali inayomfanya msomaji aone tukio hilo katika mtazamo wake. Hali hii inaashiria kuwa huu ni usemi halisi huru.

Kama ilivyotajwa hapo awali, muundo huu unaweza kuzua utata kwa msomaji katika kutofautisha baina ya wahusika wanaozungumza hasa kutokana na ukosefu wa kishazi tangulizi. Hata hivyo kulingana na Collier (1982: 168) aina hii ya unenaji ni muhimu katika kuharakisha mazungumzo ya wahusika ili kuipa nafasi hadithi kusonga mbele. Baada ya kuchanganua kigezo cha usemi halisi huru sehemu inayofuata ilichanganua usemi taarifa huru na kuonyesha nafasi yake katika riwaya teule.

4.1.4. Usemi wa Taarifa Huru

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), usemi taarifa huru ni zao la kufanyia mabadiliko usemi wa taarifa kwa kuondoa baadhi ya maneno yanayoashiria usemi taarifa na pengine kuyawakilisha na yale ya usemi halisi. Sifa yake ya kimsingi ni kuwa viambishi vya wakati, vibainishi na vielezi vya mahali vinavyohusishwa na usemi taarifa huwa vimeondolewa.

Mawazo ya Wamitila (2008) yanaafikiana na ya Short (1991) anapoeleza kuwa muundo wa usemi taarifa huru huchukua sifa zinazofungamana na za usemi halisi. Usemi huu huweza kutambulika kutokana na kuwepo kwa mwingiliano baina ya matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya tatu na njeo ya wakati uliopita na nafsi ya kwanza inayohusisha njeo ya wakati uliopo.

Aina hii ya unenaji imetawala hadithi ya *Dharau ya lni* msimulizi anaposimulia matukio mbalimbali. Mfano huu unajitokeza wakati Kivu, babake Munene alipoamua kuendesha baiskeli karibu na vifaru licha ya kuonywa kuwa ni hatari. Msimulizi anasimulia ifuatavyo kumhusu Kivu:

“Paraga mtini”, aliambiwa. Akasema atapanda akipita sehemu waliokuwa vifaru wameinama wanakula. “Unacheza na moto wewe?” Akakumbushwa...akavurumisha baiskeli kifarummoja anamwandama...Hatimaye kifarumzika kipusa chake kwenye mbavu zake! Akafa shujaa. (uk.11)

Msimulizi anasimulia kisa kuhusu jinsi Kivu alivyokosa kusikiza mawaidha ya wanakijiji ya kutoendesha baiskeli karibu na vifaru, hali iliyosababisha kifo chake. Dondoo hii inadhihirisha mfumo wa usemi wa taarifa ulio huru kwani kishazi arifu kimeondolewa na hivyo kuruhusu kuwepo kwa viwakilishi na njeo ya wakati uliopita ‘li’ kuweza kufungamana na vile vya usemi halisi. Mukadha huu umehusisha njeo ya wakati uliopo inayowakilishwa na viambishi vya wakati uliopo ‘na’, hali timilifu ‘me’ ambavyo aghalabu huhusishwa na usemi halisi. Vilevile viwakilishi vya wakati uliopita vimetumika kama vile ‘li’ katika neno ‘waliokuwa’ na ‘ka’ katika kitenzi ‘akavurumisha’

Matumizi mengine ya usemi taarifa huru yanajitokeza katika (uk.53) wakati msimulizi anaposimulia kuhusu mienendo ya Wanza. Anaeleza kuwa:

Hazikupita siku mbili kabla ya Wanza kumtembelea mamake. Mamake alihitaji huduma ya aina hii lakini watu kijijini hawalioni hili. Waulize watakwambia moja tu; ukiona mke anayeshinda kwao kila siku ujue huna mke...(uk.53)

Wanza alikuwa akimtembelea mamake kila mara. Hali hii iliwafanya wanakijiji kulalamika bila kujua kuwa mamake alihitaji kuonwa kila mara kutokana na shida zilizomkabili. Katika dondoo hili, msimulizi amehusisha baadhi ya sifa za usemi halisi katika usemi wa taarifa kwa kuyaondoa maneno mengine yanayoashiria usemi taarifa. Viwakilishi vya wakati uliopo kama kikanushi 'ha' katika neno 'hawalioni' na vivumishi vibainishi vya mahali karibu kama vile 'hili' vimehusishwa katika usemi taarifa. Usemi wa taarifa huhusisha matumizi ya njeo ya wakati uliopita inayochukua kiambishi 'li' lakini katika dondoo hii mambo ni kinyume. Mwingiliano uliotumika wa usemi halisi na usemi taarifa umesababisha kuwepo kwa mfumo wa usemi taarifa huru.

Matumizi ya usemi taarifa huru kama wanavyosema Leech na Short (1981) yanazua ukinzano wa kile kinachozungumziwa hasa kuhusiana na wakati wa usemi na utokeaji wa matukio hayo. Wanasema kuwa, uteuzi wa viwakilishi na njeo ya wakati huwa unategemea muundo wa usimulizi unaotumika katika hadithi. Hivyo ni dhahiri kuwa matumizi haya ya usemi taarifa huru yameweza kuzua ukinzano. Wanasema kuwa:

Ukinzano hutokea katika usemi wakati ambapo sauti ya msimulizi inaingilia kati ya msomaji na maelezo kuhusu tabia na hisia za wahusika hali inayosababisha kuwepo na sifa za usemi taarifa huru... (Leech na Short, 1981)

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa mbinu iliyotumika ya usemi halisi huru imeweza kuibua ukinzano kwani wakati wa unenaji na utokeaji wa matukio haufungamani na usemi wa msimulizi kuhusu wahusika wake. Usimulizi huu unaweza kuzua utata kwa msomaji katika kubainisha matukio mbalimbali.

Mfano mwingine wa usemi taarifa huru umetumika katika (uk.27) msimulizi anaposimulia kuhusu uhusiano kati ya Munene na mwanaye John. Anaeleza kuwa:

Munene kila mara alikuwa mbele na mara John naye akaiga mluzi huo; Munene anageuka na kuangalia jinsi tabia yake inavyodhihirika. Anaitika na kufurahi moyoni. Mkufu unakamilika! (uk. 27)

Msimulizi anaeleza jinsi John anavyopenda kuiga tabia za babake. Jambo hili linamfurahisha babake hasa anapoona jinsi tabia yake inavyodhihirika kupitia kwa mwanawe. Usemi taarifa huru unatumika kufanikisha kinaya kuhusu Munene na mwanaye. Usemi huu unadhihirika kupitia matumizi ya njeo ya wakati uliopo na ya wakati uliopita.

Usemi taarifa huru umeyapa nafasi matumizi ya mitazamo miwili, yaani mtazamo wa mwandishi kuhusu mienendo ya mhusika mkuu na ule wa mhusika kuhusu mwanawe. Vilevile usemi wa aina hii unaweza kutumika

kutoa fasiri tofauti katika ya mazungumzo wahusika kulingana na majukumu wanayotekeleza. Sehemu inayofuata ilichanganua matumizi ya fikra kama kipengele kingine cha usimulizi.

4.2 Uwasilishaji wa Fikra za Wahusika

Kulingana na Short (1991) hii ni mbinu ya usimulizi inayodhihirisha mivutano ya kimawazo inayotokea katika akili ya mhusika katika hadithi. Mbali na unenaji, mwandishi wa riwaya huwasilisha fikra za wahusika wake katika matukio mbalimbali ya hadithi. Ingawa ni vigumu kuona kinachopita katika akili ya mhusika, msimulizi anaweza kuhusisha matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia ili kubainisha vitendo na fikra za mhusika fulani katika hadithi (Hogan,2003). Aghalabu uzungumzi nafsia humfichulia msomaji fikra na mawazo ya ndani ya mhusika, hofu yake, matarajio yake na huweza kuwa mojawapo ya mbinu zinazotumiwa na mwandishi kumkuza mhusika katika hadithi. Uzungumzi nafsi huzuka wakati sauti ya msimulizi inapozidi kupungua hali inayoipa nafasi fikra za wahusika katika matukio mbalimbali. Wahusika huonekana wakijizungumzia katika matukio mbalimbali.

Palmer (2004) anakubaliana na mawazo ya Short (1991) anaposema kuwa, njia zinazotumika kuwasilisha fikra ni sawa na zile za unenaji. Tofauti iliyopo ni kuwepo kwa matumizi ya sifa za kisarufi kama vile viulizi, alama za mtajo, njeo ya wakati pamoja na viwakilishi nafsi. Anasisitiza kuwa, ikiwa viambishi viwakilishi vya nafsi ya kwanza na vya wakati uliopo vimetumika basi hudhihirisha kuwa usemi halisi umetumika, hali inayopelekea kuwepo kwa matumizi ya fikra halisi.

Kwa upande mwingine, iwapo viwakilishi vya wakati uliopita pamoja na viwakilishi vya nafsi ya tatu vimetumika, huonyesha matumizi ya usemi wa taarifa, hali inayosababisha kuwepo kwa fikra taarifa katika simulizi. Mwandishi anaweza pia kubadilisha njia za uwasilishaji wa fikra ili kuchukua mfumo wa fikra halisi huru na fikra taarifa huru. Katika sehemu inayofuata kigezo cha fikra halisi kilichanganuliwa ili kuonyesha matumizi yake katika riwaya teule.

4.2.1.Fikra Halisi

Haya ni mawazo yanayotokea katika akili ya mhusika katika simulizi kama anavyoeleza Short (1981), fikra halisi hutokea kupitia kwa uzungumzi nafsia, hali inayomfanya msimulizi amfichulie msomaji mawazo ya ndani ya mhusika, hofu zake pamoja na matarajio yake katika matukio mbalimbali ya hadithi. Kama ilivyosemwa awali, njia zinazotumika kuwasilisha usemi wa wahusika ndizo zinazotumika kuwasilisha fikra zao. Muundo wa kutumia fikra halisi unadhihirika wazi katika sehemu mbalimbali za riwaya teule. Msimulizi anaonyesha mzee Mbulu akijiuliza moyoni kuhusu maswali ifuatavyo:

“Kumbe wanaamka mapema hawa kiasi hiki?
Kinawaamsha nini? Wana nini cha kuhan-
gaikia majira haya?” alijiuliza (uk.28)

Mzee Mbulu anajiuliza maswali haya baada ya kumwona Munene na mwanawe John wakiteremka kuelekea alipokuwa. Mbulu alikuwa amerauka mapema akitarajia kutimiza haja yake ya kutafuta majani ya kutengeneza dawa za kuuza. Moyoni alijua huu ndio wakati uliofaa wa kuijia haja yake kabla

wenye shamba hawajaamka. Hivyo maswali anayojiuliza mawazoni ni ishara ya hofu ya kupoteza kitu alichothamini sana, yaani mapato yake.

Alama za mtajo, viulizi na viwakilishi vya wakati uliopo vimetumika kudhihirisha kuwa mbinu ya fikra halisi imetumika. Mhusika anadhihirika akijiuliza maswali bila kunena. Maneno yanayotumika yamefungiwa katika alama za mtajo kuashiria ameyaweka wazi mawazo ya mhusika wake mbele za msomaji kupitia mbinu ya fikra halisi. Mbinu hii inamfanya msomaji kuelewa hisia za mhusika kuhusu matukio.

Mfano mwingine wa fikra halisi unajitokeza katika (uk.78) Mumbe anapotembea kuelekea kwa mwalimu aliyekuwa na gazeti lililokuwa na taarifa kumhusu bintiye, Lila. Alijawa na mawazo kuhusu bintiye kama ifuatavyo:

“Mwanangu ameianza safari, wamenieleza!
Safari aliyoianza ni tofauti; ni kama mwendo
wa kaa-inakwenda mbele na nyuma. Ina
matatizo mengi lakini mkwea mlima hana
budi kuyakabili majabali...” Maneno yake
hayo yalimsimamia Mumbe akilini njia
nzima (uk.78)

Fikra hizi ni dhihirisho kuwa Mumbe ana hofu kwa ajili ya mienendo ya Lila ambaye ni mwanawe. Anahofia kuwa mienendo ya Lila ya kujihusisha na masuala ya ufisadi wa wanasiasa jijini Kitambaye ungemtia matatani. Kulingana na ulimwengu anamoishi Lila, mwanamke amedunishwa na hapaswi kujishughulisha na masuala ya kisiasa. Msimulizi anaeleza kuwa maswala kama ya kisiasa yalipaswa kushughulikiwa na wanaume pekee. Hata hivyo mawazo haya yanampa Mumbe matumaini kuwa kilio cha haki hakiwezi kudumu milele.

Msimulizi anadhihirisha mivutano ya kimawazo inayompitia Mumbe akilini. Anapowasilisha fikra za mhusika wake, anabadilisha mtazamo wa usimulizi kutoka usimulizi wa nafsi ya tatu hadi usimulizi wa nafsi ya kwanza. Mawazo ya Mumbe yanafungiwa kwa alama za nukuu kama ishara ya mbinu ya fikra halisi kama anavyodokeza Manfred (2005:66). Mfano mwingine wa fikra halisi unajitokeza katika (uk.82) Munene anapojiambia maneno haya kuhusu mkewe:

“Si neno, mwanzo hata hiyo mimba naona
inanichukia kama wasemavyo watu, mke
dawa yake ni mwingine,” alijiambia (uk.82)

Fikra hizi zinamjia Munene baada ya kushauriwa na waziri Kingo waende kujiburudisha katika ‘Royale Casino’ jijini mwao. Waziri huyu alikuwa amemtahadharisha kuwa angeendelea kukaaka na mkewe kila siku angepumbaa tu. Ushauri wa Kingo ulimfanya Munene abadili mtazamo wake kuhusu mkewe na kuamua kumwacha mkewe aliyekuwa mjamzito.

Mawazo ya Munene yamefungiwa kwenye alama za mtajo kuashiria kuwa ni fikra zake mwenyewe na wala si za mtu mwingine. Vilevile kuwepo kwa matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza ni dhihirisho kuwa msimulizi amehusisha fikra halisi. Msimulizi anamwezesha msomaji kupata fikra na hisia za Munene kuhusu ndoa yake hivyo kujishirikisha na hisia zake. Mbali na fikra halisi mwandishi ametumia mfumo mwingine wa fikra halisi ulio huru katika kuwasilisha matukio.

4.2.2. Fikra Halisi Huru

Fikra halisi huru kama wanavyoeleza Leech na Short (1981) ni mbinu ya usimulizi ambapo fikra za mhusika huonyeshwa kwa kutumia usemi halisi.

Kama ilivyosemwa hapo awali, njia za kuwasilisha fikra za wahusika ni sawa na zile za kuwasilisha usemi wao. Tofauti iliyopo ni kwamba katika uwasilishaji wa fikra halisi huru, kishazi tangulizi na alama za mtajo huwa zimeondolewa hali inayoifanya fikra kuwa huru zaidi (Sternberg, 1982).

Riwaya ya *Dharau ya Ini* imedhihirisha wahusika wakijizungumzia kwa kutumia nafsi ya kwanza na hivyo kutuonyesha mawazo yao kwa njia ya moja kwa moja. Fikra halisi huru inajitokeza katika (uk.42) baada ya Wanza kumwaibisha mumewe King'o mbele ya wageni wake. King'o anajisemea ifuatavyo:

Mwanamke asipokumbushwa hili huishia kuota pembe kama huyu! (uk.42)

King'o anajisemea maneno haya alipokuwa akielekea kule alikonuia kutafuta viboko vya kuirudisha hadhi yake kama mwanaume. Wanza alikuwa amemwamrisha mumewe mbele ya wageni wake aende jikoni akawashe moto na awapikie wageni hao chai. Kitendo hicho kilimuudhi King'o kwani mkewe alikiuka tamaduni za jamii zinazohitaji mke kumhudumia mume wake.

Maneno yanayotumika yanadhihirisha wazi matumizi ya fikra halisi huru kutokana na muundo wake. Hapa alama za mtajo hazijatumika ili kuyafungia mawazo ya mhusika. Msimulizi ametumia viwakilishi vya nafsi ya tatu na viwakilishi vya wakati uliopo pamoja na viashiria vya karibu katika kuyawasilisha mawazo ya King'o. Mfano mwingine wa fikra halisi huru unajitokeza katika (uk.53) wakati Wanza anapojisemea maneno yafuatayo:

Kumpenda mwanaume kiasi hiki ni utumwa,
alijisemea Wanza (uk.53)

Mawazo haya yanampitia Wanza akilini hasa baada ya kumkagua mamake na kutambua jinsi alivyodhoofika mwili kutokana na mawazo yaliyomla ndani kwa ndani. Kasina anasononeka kutokana na ukiwa wa mapenzi baada ya kutalikiwa na mumewe. Msimulizi amehusisha fikra halisi bila kuzingatia alama za mtajo pamoja na viakifishi vingine. Fikra halisi huru pia inadhihirika katika (uk.107) wakati Munene anapojisemea maneno haya:

Ukutilia maanani hofu zote na maneno yote
ya wanawake utaishia kufa kwa mshtuko.
Mara ngapi majani yaangukialo paa usiku
yamekuwa msingi wa hofu ya kuingiliwa na
wezi, aliwaza akilini (uk. 107)

Haya ni mawazo ya Munene kuhusu mkewe Debora. Mara nyingi Deborah alikuwa anamwamsha mumewe usiku na kumuuliza kama amewasikia wezi wanaovunja nyumba kumbe yalikuwa majani tu! Mumewe hangemwamini kamwe. Munene aliamua kuyapuza maneno ya mkewe na kuanza kumwona mkewe kama mtu anayejawa na wasiwasi usiokuwa na msingi. Hivyo hangemwamini kamwe.

Msimulizi anawasilisha fikra za Munene kwa kuingiza nafsi ya pili ili kumshirikisha msomaji katika hisia za wahusika wake. Ni dhahiri kuwa alama za mtajo zimeondolewa mawazo ya Munene yanapowasilishwa mbele ya msomaji hali inayoashiria kuwa ni fikra halisi huru. Fikra za Munene zinaonyesha jinsi anavyojipumbaza ili kuukimbia uhalisi wa maisha yanayomzingira.

Sehemu hii imebainisha wazi kuwa fikra za wahusika zimetumika kama msingi wa ukuzaji wa ujumbe katika hadithi. Sauti zilizo ndani ya fikra halisi ndizo zinazotumika kuendeleza simulizi. Ni dhahiri kuwa kishazi tangulizi na alama za mtajo zimeondolewa wakati mawazo ya wahusika yanaonyeshwa mbele za msomaji.

4.2.3 Fikra za Taarifa

Fikra za taarifa kama asemavyo Sternberg (1982: 93-94) ni mawazo ya wahusika yanayowasilishwa kwa njia ya usemi wa taarifa. Anaeleza kuwa fikra hizi huwasilishwa kwa nafsi ya tatu ambapo viwakilishi vya wakati uliopita hutumika. Aina hizi za fikra zimedhihirika katika sehemu mbalimbali za riwaya teule. Msimulizi amefaulu kuwasilisha mawazo ya Katumbi kuhusu hali ya ndoa yao na Munene. Anaeleza kuwa:

Katumbi alimwazia Munene tena. Akahisi pali-
kuwa na tomo fulani kwenye banda lake la uhai
ambalo alihitaji kuliziba; Akaukumbuka ule
ulevi uliokubuhu. Mara ngapi alipomshauri
kuwa pombe ingeweza kuiathiri afya yake...
(uk.50)

Katumbi anawaza kuhusu mumewe na kukumbuka jinsi alivyokuwa akilewa kupita kiasi kabla ndoa yao kuvunjika. Mkewe alikuwa akimwonya dhidi ya kushiriki ulevi kwani ungeathiri afya yake lakini hakusikia. Msimulizi amewasilisha fikra za kasina kwa nafsi ya tatu. Viwakilishi vya wakati uliopita vimetumika, hali inayosababisha kuwepo kwa fikra taarifa. Mwandishi anapowasilisha fikra za mhusika anamwezesha msomaji kuona mambo na

matukio kwa mtazamo wa mhusika huyo. Mfano kama huu pia unajitokeza (uk.93) msimulizi anaposimulia kuhusu fikra za Wanza. Anaeleza kuwa:

Katika akili ya wanza kulikuwa na mivutano mingi sana. Hisia za mapenzi na welewa zilivutana kwa kiasi kikubwa na hisia za ukali na ufidhuli. Ndio, kwa kiasi kikubwa alikuwa binadamu aliyemiliki binadamu wawili. (uk. 93)

Msimulizi anamfuata mhusika wake kwa makini na kufichua hisia zake. Anaeleza kuwa ndani ya fikra za Wanza kulikuwa na mivutano ya hisia baina ya mapenzi na ukali na ufidhuli. Msimulizi anatueleza kuwa kwa mara ya kwanza, Wanza alimwinamia mumewe na akampiga pambaja kisha akayaachilia machozi yake yaliyopukutika kupukupu. Hali hii ni kinyume na matarajio kwani wengi walimjua kama Wanza aliyejawa na ukali na ufidhuli.

Fikra za wanza zimewasilishwa kwa kutumia nafsi ya tatu pamoja na viwakilishi vya wakati uliopita. Kupitia mawazo ya Wanza, msimulizi amemwezesha msomaji kuziona fikra za mhusika huyu na kuelewa mivutano inayotokea katika maisha yake. Licha ya kwamba alijulikana kama mwanamke mwenye ukali na ufidhuli, anamhurumia mumewe baada ya kujeruhiwa na babake.

Fikra taarifa huenda sambamba na usimulizi wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi ana sifa za kiungu za kuweza kujua fikra za wahusika wake. Hivyo anaelewa kwa kina mawazo ya mhusika wake na kuyaona mambo kwa mtazamo wa mhusika huyo kuliko msimulizi wa nafsi ya kwanza kama anavyodokeza Wamitila (2002: 40).

Katika riwaya husika msimulizi anamfuata mhusika wake kwa makini na kuripoti anayoyafikiria kwa kutumia viwakilishi vya nafsi ya tatu. Mfano huu unadhihirika katika (uk.46) msimulizi anapotueleza kuwa, njia nzima Munene alishindwa kutulizana akili kwa kuwaza:

Picha ya yule mzee, ile taswira isiyopotea, ambayo imemjia mara kadha ndotoni ilimsimamia mbele kama jinamizi. Ni kweli alijihesabu jasiri na shujaa lakini kila mara alipopambana na mzee huyo alijiwa na unyonge wa ghafla uliomlemaza skrubu za u-simba na u-Munene wake huo (uk.46)

Msimulizi anayaweka wazi mawazo ya Munene na hofu aliyokuwa nayo kuhusu Mzee Mbulu. Msimulizi anasema kuwa picha ya mzee huyo ilikuwa inamjia mara kadha akiwa ndotoni; na kila alipokabiliana naye alijiwa na udhaifu wa ghafla uliomlemaza na kuondoa ujasiri wake. Katika kauli hii, viwakilishi vya nafsi ya tatu na kiambishi cha wakati uliopita 'li' vimetumika, hali inayopelekea kuwepo kwa fikra taarifa. Kupitia fikra za Munene, msimulizi anamwezesha msomaji kuelewa mtazamo wake kuhusu tabia za mzee Mbulu. Kutokana na fikra na hisia za Munene, ni dhahiri kuwa msimulizi wa nafsi ya tatu ana uwezo wa kuyaona mawazo na saikolojia ya wahusika wake na kuyaweka wazi mbele ya wasomaji.

Kama ilivyotajwa awali, njeo ya wakati na viwakilishi nafsi huweza kutumika kubaini aina ya usemi na fikra za wahusika katika hadithi. Ikiwa viwakilishi nafsi ya tatu na viambishi vya wakati uliopita vimetumika, basi hudhihirisha kuwa usemi taarifa umetumika, hali inayopelekea kuwepo kwa fikra taarifa. Mwandishi amedhihirisha jinsi uwasilishaji wa fikra taarifa unavyoweza

kuwepo kwa matumizi ya mfumo wa fikra taarifa huru kama ilivyochanganuliwa hapa chini.

4.2.4. Fikra za Taarifa Huru

Kulingana na Wales (1989: 189), fikra taarifa huru ni mawazo ya wahusika ambayo huwekwa wazi mbele za msomaji ili kuonyesha hisia na tabia zao kuhusu matukio mbalimbali. Anaeleza kuwa mfumo huu ni tofauti na wa fikra taarifa kutokana na upekee katika muundo wake. Fikra taarifa huru zinapowasilishwa, njeo ya wakati hubadilika kutoka wakati uliopita hadi wakati uliopo na kiwakilishi cha nafsi ya tatu hubadilika na kuchukua mfumo wa nafsi ya kwanza. Vilevile kishazi arifu huwa kimeondolewa huku viakifishi viulizi na vihusishi vikihusishwa. Msimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* anatuonyesha fikra za Kasina katika (uk.66) kwa kuhusisha fikra taarifa huru. Anamwagalia kitinda mimba wake aliyekuwa amemtembelea kwake nyumbani kisha anajiambia maneno ifuatavyo:

Hawa watoto wa siku hizi mbona hivi? Mzazi
gani atashindwa kumtambua mwanawe?
Labda kachochewa na dada yake. Hapana,
haiwezekani anayoyasema, alijiambia (uk.66)

Mwandishi anatuonyesha fikra zinazomjia Kasina baada ya binti yake kitinda mimba kumwambia kuwa babake alikosa kumtambua walipokutana naye. Alishuku kuwa bintiye alikuwa akimdanganya kwani hakuona vile babake mzazi ambaye ni damu yake angekosa kumtambua.

Muktadha huu umechukua umbo la fikra taarifa huru. Mawazo haya ya Kasina kuhusu bintiye yamewasilishwa kwa njia ya maswali kwa kuzingatia alama za

viulizi. Sifa nyingine ni kuwa njeo ya wakati uliopita imebadilika na kuchukua mfumo wa wakati uliopo kama anavyosema Wales (1989). Mfano mwingine unajitokeza mwandishi anapodhihirisha fikra zinazompitia King’o akilini hasa baada ya kupigwa kichapo cha mbwa na mwajiri wake. Anawazia ifuatavyo:

Jana nimeshindwa kulala kwa sababu ya binti
yake kisha leo ni huyu. Mwana na babake!
Hapana! (uk.91)

Mawazo yanayodhihirishwa hapa juu ni ya King’o, mumewe Wanza. Alikuwa anawazia jinsi mkewe alivyomgombeza usiku kucha na isitoshe, baada ya hapo mwajiri wake ambaye ni mkwewe akampiga kichapo cha mbwa akiwa kazini.

King’o alikuwa amewaachilia ng’ombe wakaingia shambani na kuyala mahindi. Kitendo hicho kilimwacha King’o akifikiria kwa ghadhabu kubwa hatua ambayo angechukua.

Msimulizi anapowasilisha fikra za King’o, amehusisha sifa zote za fikra halisi ambapo viakifishi viulizi na viwakilishi vya wakati uliopo vimetumika. Njeo ya kitenzi imebadilika kutoka wakati uliopita na kuchukua wakati uliopo. Haya yanadhihirishwa zaidi kwa matumizi ya vihisishi na viwakilishi vya wakati uliopo kama vile ‘na’ na ‘me’.

Fikra taarifa huru vilevile zinaweza kujitokeza katika matukio ambayo tayari yanasimuliwa kwa nafsi ya kwanza ambapo matumizi ya wakati uliopo yanadhihirika kama anavyosema Barry (1995). Hivi ni kusema kwamba si lazima kuwe na mabadiliko kutoka njeo ya wakati uliopita hadi njeo ya wakati

uliopo tu. Bali miundo yote miwili inaweza kusababisha kuwepo kwa fikra taarifa huru. Hali kama hii inajitokeza katika (uk.242) wakati maswali yafuatayo yanapomjia Wanza akilini:

Labda nimwambie? Labda niseme ni nini?
Nimwambie kuwa ninajiwa na hofu siku hizi
nisiyojua ni ya nini? (uk.242).

Lila anajiuliza maswali baada ya mkuu wa shirika la habari la Mpapure kutaka kujua ni nini kilichokuwa kinamsumbua Lila. Fikra za Lila zinaashiria hisia za woga pamoja na ugumu wa kumfichulia Silverstein ukweli kuhusu jinsi alivyotekwa nyara na watu wasiojulikana akiwa na mwenzake Derby. Walikuwa wamechapisha taarifa zilizohusu suala la ufasadi uliyohusisha baadhi ya mawaziri serikalini. Utekaji nyara huo ulikuwa njia ya kuwakomesha wasiingilie masuala ya kisiasa kama wanawake.

Mawazo ya lila yamewasilishwa kwa kuhusisha viwakilishi vya nafsi ya kwanza pamoja na njeo ya wakati uliopo. Viulizi na vivumishi vionyeshi vya karibu vimetumika. Kiashiria ‘hizi’ kinaashiria wakati uliopo kinyume na sifa za fikra taarifa zinazotumia viwakilishi vya wakati uliopita pekee. Isitoshe, katika (uk.105) msimulizi anaonyesha wazi fikra zinazopitia Lila akilini baada ya kupata habari kuwa kaburi la babake lilikuwa limefukuliwa. Lila anajiuliza:

Kwa nini liwe la baba? Je, huyo aliyefanya
hivyo alikuwa na nia gani hasa? Ni kwa nini
mama hakunieleza jambo kubwa kama hili?
Mkondo wa mawazo ulipiga kwa nguvu na
kutishia kuzibomoa kuta za akili na kujito-
keza usoni na machoni (uk. 105)

Fikra hizi zinaamjia Lila alipokuwa amemtembelea babu yake katika harakati zake za kutafuta alikofia na kuzikwa babake. Lila anashangazwa na taarifa za babu yake kuwa kaburi la babake lilikuwa limefukuliwa na kichwa chake hakikuwepo. Hivyo msimulizi amedhihirisha wazi mawazo ya mhusika wake kwa msomaji ili aweze kupata ufahamu zaidi kuhusu hisia zake.

Muktadha huu unadhihirisha matumizi ya fikra za taarifa huru hasa kutokana na kuwepo kwa muundo wa viulizi na viashiria vya karibu. Hali hii inaonyesha kuwa baadhi ya maneno ya asili yanayoashiria usemi taarifa yamebadilika na kuchukua mfumo wa usemi halisi. Kwa mfano kiashiria ‘hili’ kimetumika badala ya ‘lile’ kuonyesha uhusiano wa karibu kimasafa na mnenaji hivyo inafaa kitumike katika usemi halisi.

Mfumo wa uwasilishaji wa unenaji hauafikiwi tu kwa uwepo wa sifa rasmi za kiisimu bali unaweza kuhusisha matumizi ya miktadha mingine isiyo ya kiisimu kama wanavyodokeza Leech na Short, (1981). Hivyo mwandishi anapowasilisha fikra za mhusika kwa njia yoyote ile huwa anamhusisha msomaji kuyaona matukio kwa mtazamo wa mhusika huyo.

Kulingana na maoni ya Short (1991), kuna uwezekano wa msomaji kuyaelewa mawazo na mtazamo wa mhusika hata bila kuwasilisha fikra zake moja kwa moja. Hivi ni kusema kwamba msimulizi anaweza kuwasilisha fikra za mhusika wake kwa njia isiyo halisi au isiyoonekana wazi mbele ya msomaji kwa mfumo wa taarifa.

Mfano wa fikra ambazo hazijawasilishwa moja kwa moja mbele za msomaji zinapatikana katika (uk.242). Msimulizi anaeleza kuwa, jioni Lila alipotoka kazini akili yake ilimlaumu kwa kutomwambia mkurugenzi kuhusu jambo lililokuwa likimsumbua. Pia anaendelea kusema kuwa uhusiano wake na wafanyikazi wa *Mpapure Holdings* ulikuwa mzuri lakini alihisi kuwa kati yake na mwenyekiti palikuwa na uhusiano wa kihisia kama uliokuwako kati ya mtoto na baba.

Anachosema Lila ni picha mwafaka ya kile anachofikiria ingawa mawazo na hisia zake haziwekwi wazi mbele ya msomaji. Hivyo kupitia mawazo na hisia za mhusika msimulizi anamhusisha msomaji katika kuyaelewa matukio kwa mtazamo wa mhusika huyo hata kama mawazo yake hayajawasilishwa moja kwa moja mbele ya msomaji.

Kimsingi, matumizi mwafaka ya uwasilishaji wa unenaji na fikra ni njia anayotumia mwandishi katika kubadili mtazamo wa usimulizi. Hali hii imedhihirika wazi katika riwaya teule. Msimulizi amehusisha mitazamo mbalimbali ya usemi na fikra katika uendelezaji wa hadithi. Isitoshe, muundo huu wa uwasilishaji wa hadithi umeweza kuondoa ule uzoefu wa mtazamo uliozoelewa na kuifanya hadithi iwe na upekee na mvuto zaidi kwa msomaji.

4.3 Kiishilio

Sura hii ilichanganua uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Ililenga kubainisha aina mbalimbali za usemi na fikra za wahusika na kuonyesha matumizi yake katika uendelezaji wa ujumbe. Sehemu hii imeonyesha kuwa njia zinazotumika kuwasilisha usemi ndizo zinazotumika kuwasilisha fikra za

wahusika. Imebainika kuwa matumizi mbalimbali ya usemi na fikra ni njia mwafaka inayoweza kutumika kubadili mitazamo ya usimulizi. Mwandishi ametumia usemi na fikra halisi ambazo zimechukua mtazamo wa ndani unaohusisha nafsi ya kwanza. Usemi na fikra taarifa nazo zimechukua mtazamo wa nje kwa kuhusisha usimulizi wa nafsi ya tatu katika upitishaji wa ujumbe. Sura inayofuata ilishughulikia muhtasari, matokeo, mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti. Imegawanywa katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza imezingatia muhtasari wa utafiti. Sehemu ya pili imejikita katika matokeo ya utafiti. Mchango wa utafiti umeshughulikiwa katika sehemu ya tatu. Sehemu ya nne nayo imeangazia changamoto zilizokabili utafiti na sehemu ya tano ikazingatia mapendekezo ya utafiti.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti uliofanywa ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007) na Wamitila. Utafiti huu ulilenga kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi, kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi na kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Naratolojia.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa tasnifu na kuonyesha pengo lililopo hasa lililokusudiwa kuzibwa na tasnifu hii. Suala la utafiti, maswali ya utafiti, upeo wa utafiti, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, njia za kukusanya data, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na msingi wa nadharia ya naratolojia yalizingatiwa katika utafiti huu. Katika kuyaafikia malengo ya utafiti, riwaya ya *Dharau ya Ini* iliteuliwa kwa misingi kuwa imehusisha matumizi mapana ya mbinu za usimulizi ambazo zingetosheleza malengo ya utafiti huu.

Sura ya pili ilichanganua sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi. Sehemu hiyo imejikita katika uonekanaji wa msimulizi na nafsi ya usimuliaji, mahusiano ya wakati wa usimulizi, majukumu ya msimulizi mbalimbali vya usimulizi. Kazi hii ilinua kudhihirisha iwapo msimulizi amejitokeza waziwazi au amejificha akakosa kuonekana wazi mbele ya msomaji katika matukio anayosimulia. Ilikusudia kuonyesha iwapo msimulizi amehusisha nafsi zote tatu za usimulizi katika uwasilishaji wa matukio.

Mahusiano mbalimbali ya wakati wa usimuliaji wa hadithi yalichunguzwa ili kuonyesha iwapo matukio yamesimuliwa kabla ya kutendeka, baada ya kutokea au yanapoendelea kutendeka ili kuonyesha uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi. Vilevile mtafiti alibainisha majukumu mbalimbali ya msimulizi mbali na usimuliaji wa hadithi. Viwango vya usimulizi vilichanganuliwa ili kubainisha iwapo vinaenda sambamba na viwango vya hadithi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*.

Utafiti uligundua kuwa riwaya teule imehusisha msimulizi wa ndani, anayejitokeza wazi mbele ya msomaji katika sehemu mbalimbali za hadithi na katika sehemu zingine kuna msimulizi wa nje, asiyeonekana wazi mbele ya msomaji. Riwaya husika imehusisha nafsi zote tatu za usimulizi katika uwasilishaji wa matukio. Utafiti ulibainisha majukumu mbalimbali ya msimulizi katika hadithi. Iidhihirika wazi kuwa kazi ya msimulizi sio tu usimuliaji wa hadithi, bali anaweza kutekeleza majukumu mengine kama vile kuyagawa maarifa aliyonayo kwa wahusika wake na wasikilizaji, hali inayojenga mawasiliano bora.

Isitoshe utafiti ulitambua kuwa msimulizi amehusisha viwango mbalimbali vya hadithi ambavyo vinaenda sambamba na usimulizi wa hadithi. Kuna hadithi ya kimsingi, hadithi kuu na vijihadithi vingine vinavyoshehenezwa katika hadithi hizo mbili. Hadithi hizi zilizoegemezwa zimetumika katika kufafanua matukio mbalimbali, hali inayomwezesha msomaji kupata ufahamu zaidi kuhusu kinachosimuliwa katika hadithi.

Sura ya tatu ililenga kuchanganua nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya. Utafiti ulijikita katika vigezo vitatu vikuu; mpangilio wa matukio, muda wa matukio na idadi ya utokeaji wa matukio hayo. Utafiti ulinua kubainisha iwapo matukio yamesimuliwa kwa kuzingatia mpangilio wa matukio au yamekiuka kaida ya mpangilio huo katika usimuliaji wa hadithi; kudhihirisha iwapo mwendo wa wakati wa usimuliaji hadithi umeharakishwa au umepunguzwa katika simulizi na kuonyesha athari zake kwa msomaji.

Utafiti ulidhamiria kuonyesha iwapo matukio yanapotokea na yakasimuliwa zaidi ya mara moja ni lazima miundo na maneno yaliyotumika yawe sawa. Ildhihirika kuwa riwaya teule imehusisha mbinu rejeshi na elekezi katika uwasilishaji wa matukio. Kupitia kigezo cha muda, ilibainika kuwa mwendo wa usimuliaji hadithi umerefushwa hali inayoongeza muda wa usomaji. Hii ni kwa sababu msimulizi amesitisha hadithi katika sehemu mbalimbali ili kuyapa nafasi maelezo ya ziada kuhusu wahusika wake na mazingira yao. Usimulizi kama huu huweza kumwathiri msomaji kwani hrefusha muda wa usomaji wa hadithi kwa msomaji. Ildhihirika kuwa baadhi ya matukio yametokea mara moja kisha yakasimuliwa mara kadhaa, mengine yakatokea mara nyingi na

yakasimuliwa mara moja au zaidi. Utafiti huu ulionyesha kuwa matukio yanaposimuliwa zaidi ya mara moja si lazima sentensi na maneno yafanane kwani mahali na muktadha wa utokeaji wa matukio hayo ni tofauti.

Sura ya nne ilichanganua uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Iilenga kubainisha aina mbalimbali za usemi na fikra za wahusika. Sehemu hii ilinua kubainisha iwapo matumizi mbalimbali ya uwasilishaji wa usemi na fikra ni njia mwafaka anayoweza kutumia mwandishi katika kubadili mitazamo ya usimulizi. Vilevile utafiti ulikususudia kudhihirisha iwapo mwandishi amehusisha njia za uwasilishaji wa usemi na fikra zilizo huru zaidi na kuonyesha iwapo kuna mabadiliko yoyote ya kisarufi yanayotokea mifumo hiyo inapotumika.

Utafiti ulionyesha kuwa mwandishi amehusisha aina mbalimbali za usemi na fikra katika uwasilishaji wa matukio. Ilibainika kuwa msimulizi amehusisha usemi halisi hali inayoifanya hadithi kuchukua mtazamo wa ndani ambapo viwakilishi vya nafsi ya kwanza vimetumika. Kwa upande mwingine ametumia usemi wa taarifa kwa kuhusisha viwakilishi vya nafsi ya tatu na kuifanya hadithi kuchukua mtazamo wa nje ambapo msimulizi hashiriki katika matukio anayosimulia.

Hivyo utafiti umedhihirisha wazi kuwa matumizi mbalimbali ya usemi na fikra ni njia mwafaka anayoweza kutumia mwandishi katika kubadili mitazamo ya usimulizi. Ilibainika kuwa njia zinazotumika kuwasilisha fikra ni sawa na zile zinazotumika katika usemi. Ilionekana kuwa mwandishi amehusisha njia za uwasilishaji wa usemi na fikra zilizo huru Zaidi, hali inayoweza kuwepo

kwa mabadiliko ya kisarufi katika miktadha mbalimbali. Uwasilishaji huu umempa mwandishi nafasi ya kuonyesha ubunifu na upekee wa kisimulizi kwa wasomaji

Vilevile utafiti uligundua kuwa mbinu ya uwasilishaji wa usemi na fikra huru zimetumika kama njia ya kuharakisha dayolojia baina ya wahusika, hali inayopunguza muda wa usimuliaji wa hadithi. Ingawa hivyo, matumizi haya ya usemi na fikra taarifa huru yanaweza kumfanya msomaji atoe hukumu isiyo sahihi kumhusu mhusika fulani kama ilivyotajwa awali. Muundo huu unaweza kuzua utata wa kuelewa ni nani amesema nini kati ya wahusika wanaozungumza kishazi kitangulizi kinapoondolewa. Sura ya tano imeshughulikia hitimisho la tasnifu. Hitimisho hili limetoa utangulizi wa muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Isitoshe, sura hii imeeleza matokeo na kutoa mapendekezo ya utafiti yanayoweza kufanywa siku zijazo.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Malengo ya utafiti yalikuwa ni kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi katika riwaya, kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi na kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi. Utafiti ulibainisha kuwa riwaya ya *Dharau ya Ini* imehusisha sifa na mitazamo ya usimulizi katika sehemu mbalimbali. Utafiti uligundua kuwa riwaya imehusisha msimulizi wa ndani anayeshiriki katika matukio anayosimulia. Hivyo anajitokeza wazi mbele ya msomaji katika sehemu

mbalimbali za hadithi. Katika sehemu zingine kuna msimulizi anayesimulia hadithi akiwa nje ya matukio hayo hivyo hatambuliki wazi mbele ya msomaji.

Vilevile msimulizi amehusisha nafsi zote tatu za usimulizi katika sehemu kubwa ya kazi yake, akibadilisha moja baada ya nyingine kutegemea mazingira, wahusika na matukio. Usimulizi wa nafsi ya pili pia umetumika msimulizi anapomshirikisha msomaji katika matukio anayosimulia au wakati anapohusisha matukio katika ulimwengu wa kindoto. Utafiti ulibainisha aina tatu za usimuliaji kwa kuzingatia nyakati tatu kuu ambazo ni wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao kwa lengo la kuwakuza wahusika wake katika hadithi.

Utafiti ulibainisha majukumu mbalimbali ya msimulizi katika hadithi. Mbali na usimulizi wa hadithi msimulizi amedhihirika akikatiza hadithi ili kutoa maoni yake kwa msomaji kuhusu sifa za wahusika na matukio mbalimbali. Vilevile anamshirikisha msomaji katika usimulizi wake kama njia ya kumhamasisha na kuivuta makini yake ili kumwandaa katika kukisoma kisa kingine tofauti anachosimulia ndani ya hadithi kuu.

Msimulizi pia anajitokeza wazi na kuwaelekeza wahusika wake na wasomaji kwa kuwapa maoni ya hekima yanayohusiana na kisa anachosimulia. Mwandishi anapotoa maoni yake, anamwelekeza msomaji kwenye mtazamo wake na kumchochea ili aendelee kuisoma riwaya. Vilevile utafiti ulitambua kuwa msimulizi amehusisha viwango mbalimbali vya hadithi vinavyoenda sambamba na usimulizi wa hadithi. Kuna hadithi ya kimsingi na hadithi kuu

kisha kuna vijihadithi vingine ambavyo vimeshehenezwa katika hadithi hizo na kila mojawapo ya hadithi hizo imesimuliwa na msimulizi wa kiwango tofauti.

Utafiti ulichanganua nafasi ya wakati katika usimulizi wa riwaya teule. Sura hii ilijikita katika vigezo vitatu; mpangilio wa matukio, muda wa matukio na idadi ya utokeaji wa matukio hayo. Utafiti ulibainisha kuwa riwaya teule haijazingatia kaida ya mfuatano wa matukio katika uwasilishaji wa ujumbe. Mbinu rejeshi na elekezi zimetumika katika uwasilishaji wa matukio. Kupitia kigezo cha muda, ilibainika kuwa mwendo wa wakati wa usimulizi umerefushwa hivyo kuongezea muda wa usomaji wa hadithi.

Kupitia kigezo cha idadi ya utokeaji wa matukio, ilidhihirika kuwa baadhi ya matukio yametokea mara moja kisha yakasimuliwa mara kadhaa, mengine yakatokea mara nyingi na yakasimuliwa mara moja au zaidi. Matukio hayo yanaposimuliwa zaidi ya mara moja maneno au sentensi zinazotumika hubadilisha miundo yake kisarufi bila kupotosha maana. Utafiti ulibainisha umuhimu wa kigezo hiki katika kazi ya fasihi kwani huweza kuonyesha uhusiano kati ya mara ngapi tukio fulani lilitendeka katika hadithi na mara ngapi tukio hilo limesimuliwa au kutajwa katika matini.

Katika sura ya nne utafiti ulichanganua uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika. Utafiti ulibainisha aina mbalimbali za usemi na fikra za wahusika. Ilionekana kuwa msimulizi amehusisha usemi halisi katika uwasilishaji wa ujumbe. Hali hii inaifanya hadithi kuchukua mtazamo wa ndani ambapo viwakilishi vya nafsi ya kwanza vimetumika. Vilevile usemi wa taarifa

umetumika kwa kuhusisha viwakilishi vya nafsi ya tatu na kuifanya hadithi kuchukua mtazamo wa nje.

Hivyo sura hii imedhihirisha wazi kuwa matumizi mbalimbali ya usemi na fikra za wahusika, ni njia mwafaka anayoweza kutumia mwandishi katika kubadili mitazamo ya usimulizi. Ilibainika kuwa njia zinazotumika kuwasilisha fikra ni sawa na zile zinazotumika katika usemi wa wahusika. Ilionekana kuwa mwandishi amebadilisha njia za uwasilishaji wa usemi na fikra ili kuchukua mfumo ulio huru zaidi kama vile usemi halisi huru, usemi taarifa huru, fikra halisi huru pamoja na fikra taarifa huru katika uendelezaji wa hadithi. Tofauti imetokea katika mabadiliko ya kisarufi kutegemea muktadha wa usemi wa wahusika.

Ilibainika kuwa usemi na fikra za wahusika zimetumika kama njia ya kuharakisha dayolojia baina ya wahusika, hali inayopunguza muda wa usimuliaji wa hadithi. Mwendo wa usimuliaji unapoharakishwa huweza kupunguza uchovu mwingi katika usomaji wa hadithi. Ingawa hivyo, matumizi haya ya usemi na fikra taarifa huru yanaweza kumfanya msomaji atoe hukumu isiyo sahihi kumhusu mhusika fulani. Muundo huu unaweza kuzua utata wa kuelewa ni nani amesema nini kati ya wahusika wanaozungumza kishazi kitangulizi kinapoondolewa.

5.3 Mchango wa Utafiti

Mchango mkuu wa utafiti huu ni kuwa utamsaidia msomaji kuelewa muundo wa riwaya teule kwa kina hasa kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi. Hali hii vilevile itamwezesha kupata ufahamu zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa

katika simulizi. Utafiti utaweka msingi maalum utakaofaa katika kuwaelekeza waandishi wengine kuhusisha mbinu mbalimbali za usimulizi katika utunzi wao. Isitoshe, utafiti utatoa jinsi nyingine ya kuichanganua riwaya kwa kuhusisha nadharia ya Naratolojia mbali na mbinu zingine zinazozoelewa kama zile za kimtindo, kimaudhui na za lugha. Mbali na hayo, wahakiki wa fasihi ya Kiswahili watapata ufahamu zaidi wa jinsi ya kubainisha mbinu za usimulizi katika riwaya na tungo zingine za kisasa.

5.4 Changamoto Zilizokabili Utafiti

Utafiti ulikumbwa na changamoto mbalimbali. Kulikuwa na uhaba wa vitabu vya Kiswahili hasa katika kurejelea yaliyoandikwa kuhusu mada ya usimulizi. Ilimbidi mtafiti asome vitabu na makala ya kingereza na kuyatafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Tafsiri aghalabu huathiri maana asilia kwani haiwezi kutoa maelezo ya kimsingi kwa baadhi ya maneno na sentensi, hali inayoifanya kupoteza kupoteza fahiwa yake halisi. Vilevile kulikuwa na ugumu hasa katika kupata visawe vya baadhi ya maneno yaliyotumika katika makala hayo yaliyoandikwa kwa lugha ya kiingereza.

5.5 Mapendekezo

Utafiti ulichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya ini* (2007) na Wamitila. Utafiti ulilenga kubainisha sauti za usimuliaji na viwango vya usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* , kuonyesha nafasi ya wakati katika usimulizi na kudhihirisha uwasilishaji wa usemi na fikra za wahusika katika uendelezaji wa hadithi. Hivyo kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kuchunguza

mbinu za usimulizi kwa kuzingatia vipengele vingine vya usimulizi mbali na vilivyozingatiwa katika kazi hii.

Utafiti huu ulichanganua usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya ini*. Hivyo, tafiti zaidi kuhusu muundo zinaweza kufanywa ili kuchanganua matumizi ya mbinu za usimulizi katika tungo zingine za fasihi kama vile tamthilia na hadithi fupi. Isitoshe tafiti zingine zinaweza kufanywa katika maandishi ya magazetini, vyombo vya habari au hotuba za kisiasa. Vilevile, utafiti unapendekeza uchunguzi ufanywe kwa kuangazia riwaya zilizoandikwa kuanzia mwaka wa 2010 hadi sasa. Hii ni kwa sababu tajiriba za kifasihi hubadilika kulingana na wakati. Tafiti hizo zinazopendekezwa zingefanywa, zingewezesha kazi ya fasihi kurutubishwa na kukuzwa hasa kwa kuzingatia mbinu za usimulizi katika fasihi andishi.

5.6 Kiishilio

Sura hii imezingatia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na changamoto zilizokabili utafiti huu. Pamoja na hayo utafiti umetoa mapendekezo kwamba tafiti zaidi zifanywe kuhusu kipengele cha muundo kwa kuzingatia usimulizi katika tungo zingine ili kuirutubisha kazi ya fasihi andishi.

MAREJELEO

- Arege, T. 2012. "Narration in Swahili Narrative Poetry : An Analysis of Utenzi wa Rasi 'L Guli.'" Ph.D Thesis. University of Nairobi. (Haijachapishwa)
- Bal, M. 1981. "Narrative Embedding." *Poetics Today* 2.2: 41-59.
- Bal, M. 2004. *Narrative Theory: Critical Concepts in Literary and Cultural Studies*. London: Routledge.
- Barry, P. 1995. *Beginning Theory*. New York: Manchester University Press.
- Barthes, R. 1975. *An Introduction to the Structural Analysis of Narrative*. New Literary History. Cambridge: University Press.
- Bonheim, H. 1982. *The Narrative Modes. Techniques of the short story*. Cambridge: Brewer.
- Booth, W. 1961. *The Rhetoric Fiction*. Chicago: U of Chicago P.
- Bremond, C. 1970. "Morphology of the French Folktale." *Semiotica* 2: 347-275.
- Chatman, S. 1978. *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca and London: Cornell University Press.
- Collier, G. 1992. "Style at Interface: Speech-tags." *REAL: Yearbook of Research in English and American Literature* 8: 33-107.
- Dolezel, L. 1973. *Narrative Modes in Czech Literature*. Toronto: University of Toronto P. Gordon, C. (1992) "Style at the Interface: "Speech -Tags." Year book of Research in English and American Literature.
- Fludernik, M. 1993a. *The Fictious of Languages and Languages of Fiction: The linguistic representation of speech and consciousness* : London Routledge.
- Fludernik, M. 1993b. *Second Person Fiction: Narrative 'you' as Addressee and/or Protagonist*". London: Routledge.
- Fludernik, M. 1996. *Towards a 'Natural' Naratology*. London: Routledge.
- Fokkema, D. & I B Sch. 1995. *Theories of Literature in the 20th C. Structuralism, Marxism, Aesthetics, Semiotics*. London: C. Hurst & Company.

- Gaita, J. 1998. "Narrative Process in the Kiswahili Novels of Kezilahabi and S.A. Mohamed." M.A Thesis. Kenyatta University. (Haijachapishwa).
- Gennette, G. 1980. *Narrative Discourse*. Oxford: Blackwell.
- Gennette, G. 1988. *Narrative Discourse. Revisited*. New York: Cornell University Press.
- Gromov, M. 2004). "Post Modernistic Elements in recent Kiswahili Novels." *The journal of Literature, University of Nairobi*.
- Guillimette, L. na Levesque, C. 2006. *Narratology*. Quebec: Herbert Publishers.
- Hogan, P. 2003. *The Mind and its Stories: Narrative Universals and Human Emotion*. Cambridge: UP
- Jahn, M. 2005. *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. Cologne: University of Cologne.
- Jebet, P. 2013. "Mchango wa Mbazi za Biblia katika ukuzaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili." Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Jones, E. 1994. *Critical Theory and African Literature Today*. London: James Curry Ltd
- Kenan, R. 1983. *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Methuen.
- Kenan, R. 2003. *Narrative Fiction*. 2nd ed. London: Routledge.
- Kesero, C. 1997. "Techniques of Narration and its role in Communication of Meaning in Nurudin Farah's Novels." M.A. Thesis. Kenyatta University
- Khamis, S. 1999. "Defamiliarisation and Experimentation in the Kiswahili Novel." *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Khamis, S. 2007. "Utandawazi au Utandawizi" Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili inavyodai." *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Volume 70.
- Kinara, G. 2012. "Maudhui ya UKIMWI katika Ua la Faraja na Kala Tufaha." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

- King'ei, G. 1999. "Historia na Maendeleo ya Riwaya." *ChemiChemi*. Volume 1. 1999. Nairobi: Kenyatta University press.
- Kurtz, R. 1998. *The Post Colonial Kenyan Novel*. Trenton, New Jersey and Asmara, Ethiopia: Africa World Press.
- Lanser, S. 1981. *The Narrative Act: Point of View in Prose Fiction*. Princeton UP.
- Leech, G & Short, M. 1981. *Style in fiction: A Linguistic introduction to English Fictional prose*. London : Longman.
- Mbatiah, M. 1997. "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi." *Mulika* NO. 24. Dar es Salaam.: TUKI.
- Mbatiah, M. 2016. *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- McHale, B. 1978. "Free Indirect Discourse: A Survey of Recent Accounts." *PTL: Journal for Descriptive Poetics and Literature*.
- Njogu, K. & Chimera, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Omutimba, C. 2015. "Usimulizi katika Riwaya za Adili na Nduguze, Walenisi na Babu Alipofufuka." *Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta*. (Haijachapishwa)
- Ong'ondi, B. 2005. "Uhakiki wa Usimulizi katika Riwaya ya Walenisi." *Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi*. (Haijachapishwa)
- Palmer, A. 2004. *Fictional Minds*. Lincoln: U of Nebraska P.
- Prince, G. 1982. *Narratology. The Form and Functioning of Narrative*. Berlin: Morton.
- Raban, J. 1968. *Technique of Modern Fiction*. London: Edward Arnold.
- Ricour, P. 1985. *Time and Narrative*. Volume. 2. London: The University of Chicago Press.
- Shitemi, J. 2011. "Usimulizi katika Utenzi wa Siri Li Asirali." *M.A Chuo Kikuu cha Nairobi*. (Haijachapishwa).

- Short, M. 1991. *Speech Presentation, the Novel and the Press. The Taming of the Text: Explorations in Language, Literature and Culture*. London: Routledge.
- Stanzel, F. 1984. *A Theory of Narrative*. Cambridge University Press.
- Sternberg, M. 1982. "Point of View and Indirections of Direct Speech" *Language and Style*. Pittsburgh: Pittsburgh UP.
- Todorov, T . 1977. *Structural Analysis of Narrative. The Norton Anthology of Theory & Criticism*. (eds). New York: W.W. Norton & Company.
- Toolan, M. 1988. *Narrative : A Critical Linguistic Introduction*. London Routledge.
- Toolan, M. 2001. *Narrative: A Critical Linguistic Introduction*. 2nd ed. London: Routledge.
- TUKI .1981. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI .2006. *English – Kiswahili Dictionary*. Dar- es- Salaam. TUKI.
- Wales, K. 1989. *A Dictionary of Stylistics*. London: Longman.
- Wamitila, K. 2002. *Uhakiki wa Fasihi. Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. 2003. *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. 2007. "Narrative Structure and Metaphor: Towards a new aesthetics of the Kiswahili Novel." *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wamitila, K. 2007. *Dharau ya Ini*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.
- Wamitila, K. 2008. *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.